**19 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini – Tarehe 19 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika: (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**MHE. SHALLY J. RAYMOND – K. n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Mwenyekiti na kwa mujibu wa Kanuni ya 43 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023/2024, Tathimini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 651

### Kuongeza mafao kwa askari wastaafu

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza mafao kwa askari wastaafu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii huongeza kiwango cha pensheni ya kila mwezi ya wastaafu mara baada ya kufanya tathmini na kujua uendelevu wake na uwezo wa kulipa mafao kwa wanachama wake. Tathmini hiyo hufanyika kila baada ya miaka mitatu kwa kipindi kifupi, miaka mitano kwa kipindi cha kati na miaka kumi kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya Ulipaji Mafao Namba 11(1) za mwaka 2018 zinaelekeza Mfuko wa *PSSSF* kuongeza pensheni kwa kuzingatia mfumuko wa bei na uendelevu wa mfuko kila baada ya miaka mitatu. Hata hivyo, ninayo furaha kukuarifu na kuarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi sasa wastaafu wote wa Serikali walishaboreshewa pensheni zao za kila mwezi ambapo kiwango

cha chini ni shilingi 100,000 inaendelea kulipwa tofauti na hapo ilivyokuwa awali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanayoridhisha.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; je, Serikali imejipangaje kuhusu kulipa mafao ya wastaafu ambao hawajapata mafao hayo nikitolea mfano Wafanyakazi wa Shirika la Ndege Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, ni hatua gani mnachukua kwa waajiri ambao hawalipi michango ya wanachama kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)**: Mheshimiwa Spika ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na malipo au ucheleweshaji wa mafao tayari kwenye hatua hiyo tumeshavuka. Mpaka sasa mifuko yetu *PSSSF* pamoja na *NSSF* tayari tumekwishakuanza utaratibu wa ulipaji kupitia mfumo wa teknolojia ya TEHAMA ambapo wanachama wote wanapewa hata taarifa sasa kupitia simu za mkononi au simu ya kiganjani na yeyote yule ambaye amekuwa amecheleweshewa kupata mafao yake tumekuwa tukichukua hatua hasa katika kuhakikisha kwamba tunapata nyaraka zao sahihi na kwa wakati ili waweze kuweza kulipwa.

Kwa hiyo, wachache sana ambao wanapata changamoto hizo kwa sasa na ikitokea changamoto hizo zinatokea tumekuwa tukiwaomba aidha kupitia Mheshimiwa Waziri ambaye alizunguka Mikoa karibia nchi nzima kwa kupitia kikanda kwenye majiji

alikutana na wastaafu na tumekuwa tukipokea na tuna *desk* maalum la kupokea changamoto hizo. Kwa hiyo, kama zipo nimuombe Mheshimiwa Mbunge anifikishie ikiwa ni pamoja na za *ATCL* kwa taarifa tulizonazo ofisini tayari wapo walikwishakulipwa zaidi ya wafanyakazi 500 na wale wachache ambao walikuwa wana changamoto ilikuwa ni kuhusiana na taarifa sahihi hazikuweza kuwasilishwa ofisini ili waweze kulipwa. Kama watakuwa wamepata nyaraka na taarifa sahihi tuko tayari kuweza kuwalipa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la waajiri kutokuwasilisha michango kwa wakati. Mifuko hii inazo sheria ambayo inaianzisha na katika sheria hizi zinaeleza ni kosa kwa mwajiri kutokuwasilisha michango kwa wakati katika mifuko hii kwa ajili ya wanachama na ikitokea hivyo hata mahakamani Bunge lako tukufu lilitunga sheria hii kwa kujua umuhimu wa watu hawa ni katika mfumo wa *summary suit*. Kwa hiyo, unapelekwa mahakamani, hakuna kujitetea na tunachua hatua.

Kwa hiyo, kama kuna maeneo ambayo watakuwa wamechelewesha michango kwa kweli nitoe rai kupitia Bunge lako tukufu kwamba tunawataka waajiri wote nchini kutekeleza hilo, kupeleka michango kwa wakati ya wanachama ili wasisumbuke, lakini pia sisi pia kutupunguzia mashauri yaliopo mahakamani, mpaka sasa tuna mashauri zaidi ya 26 na tumechukua hatua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jambo hilo ni changamoto kubwa sana huko kwa wapiga kura, mmelipunguza kwa sehemu kubwa, lakini bado ni changamoto, wanapoenda mfuko badala ya kuwalipa pesa, unawaambia kafuatilie mwajiri wako hakuleta, wakati kazi ya kufatilia siyo wa mwajiriwa. Kwa sababu yeye hawezi kumuuliza umepeleka ama hujapeleka. Ni kazi ya yule mwenye mfuko ama ni kazi ya mfuko kufutilia kwa yule ambaye alipe. *(Makofi)*

Nadhani hilo ninyi muendelee kulifatilia kwa upande wa mifuko, je, waajiri wanapeleke? Kama hawapeleki ichukulieni hatua mifuko, lakini huyu mwajiriwa asipate tabu anapostaafu alipwe pesa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fakharia Shomar, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante; kwa kuwa suala la wastaafu kama hilo liko sawasawa na walioko Zanzibar, je, Wizara yako inatoa faraja gani kwa wale walioko Zanzibar wanaokawia kupata mafao yao au hawapati kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shomar kama alivyoeleza kuhusiana na kwamba changamoto zilizo upande wa Bara ni sawa na zile zilizopo upande wa Zanzibar. Kwa kuwa hii ni Serikali ya Muungano na tunafanyakazi kwa *collective responsibility* ninaomba kulichukua swali hili na tutawasiliana na Mamlaka za Zanzibar ili kuhakikisha wastaafu wetu hawapati tabu baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, pia nilieleze Bunge lako tukufu kwamba nimechukua na kupokea mwongozo wako kuhusiana na changamoto ambazo wanazipata. Lakini pia nitumie nafasi hii kwa sababu tumeshachukua hatua sana kuhusiana na kuwapeleka mahakamani, wakati mwingine mashauri pengine yanachelewa na watu wetu wanazidi kuumia.

Sasa naomba nifanye hatua moja na kwa Mheshimiwa Waziri kama hatua tuliokwishakuichukua kama unaniruhusu nitaje namba ya simu ambayo wakituma ujumbe pale mara moja wanaweza kupata huduma, lakini pia tuna ma–*desk* yetu kwenye zile ofisi tumezi–*establish* sasa kwa ajili ya kuwapa huduma wastaafu wetu na ni kwa kupiga simu tu ama kwa kuwasiliana kupitia *WhatsApp* na tunachukua hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukifanya mzaha wa hawa wastaafu na changamoto ambazo zimekuwepo tutachukua hatua kwa mameneja wetu wa mikoa ili kama hawezi kuwahudumuia Watanzania basi waje wengine wanaoweza kuwahudumia na hili ni agizo langu kwa mikoa yote wahakikishe

hakuna malalamiko ya wastaafu na mameneja tutawapima kwa kiwango cha wanaolalamika kuhusu wastaafu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya watajie namba maana ikitajwa hapa itakuwa na uzito, watajie namba wastaafu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, namba ni 0715939902. Ni 0715 939902, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tamima Haji Abass swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali imejipangaje kutoa uelewa kwa watumishi wanaotarajia kustaafu hasa kuhusu kikokotoo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeendelea kutoa elimu ya kuhusiana na kikokotoo na kwa msingi huo mifuko yetu imeshirikiana na Chama cha Waajiri *(ATE)* katika kutoa elimu, lakini pia Shirikisho la Wafanyakazi *(TUCTA),* lakini pia tumekuwa tukiwafikia hata kwenye makundi kulingana na kada zilizopo za ajira. Kwa hiyo, hata hao ambao ameeleza Mheshimiwa Mbunge tutawafikia na swali la utoaji wa elimu kuhusiana na kikokotoo ni endelevu ili waweze kuona faida ambayo wanaweza kuipata kutokana na kikokotoo hiki kipya, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wengi wamekuwa wanapata adha ya kufanya uhakiki wa mara kwa mara kuthibitisha kwamba bado wako hai, *proof of life* na wanahitajika kwenda makao makuu ya Wilaya au ama katika taasisi ambazo walistaafu kwa ajili ya kwenda kufanya hiyo *proof of life*?

Je, ni mkakati gani ambao Serikali mtachukua kuhakikisha kwamba kunakuwa na mfumo wa kisasa wa kuweza kufanya hiyo *proof of life* badala ya usumbufu ambao unaendelea kwa hivi sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndugulile kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na changamoto sana ya wastaafu wetu kwenda kuambiwa kwamba anaenda kuhakikiwa taarifa na kadhalika, lakini tuliliona hilo na tukaanzisha mfumo maalum wa kuwahitaji wao kuwa na namba zao za mawasiliano za kiganjani, lakini pia kuanzisha *portal* maalum ya kutoa taarifa za wanachama na hatua ya pili tuliyoichukua ni kwamba kuhakikisha sasa taarifa hizi zinaenda *on monthly basis* kuhakikisha kwamba taarifa zake kwa wakati wote zinapatikana kwa Mfumo wa TEHAMA. Kwa hiyo, tumejihimarisha kwenye TEHAMA na tunafanya vizuri na sasa tumekwishakuanza kuwahudumia vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wapo walimu ambao michango yao ilikuwa haikupelekwa na watumishi, lakini wakaambiwa wajilipie wenyewe, wamejilipia wenyewe, wana risiti mkononi, lakini marekebisho ya mafao yao hayakufanyika.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na walimu hao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa Mwanachama ambaye alikuwa amesajiliwa kihalali na sahihi kabisa, lakini pia kuna mwajiri ambaye alikuwa na wajibu wa kulipa michango hajatekeleza wajibu wake na badala yake mwanachama akalazimika kujichangia mwenyewe, hilo kwanza siyo sahihi na linahitaji ufuatiliaji.

Kwa hiyo ,niombe nipate takwimu sahihi za wanachama hao ambao walifanya hivyo na bado pia hawajaweza kutendewa haki, tulichukue kama ofisi na kwenda kulifanyia kazi, kwa sababu sina takwimu sahihi nitaomba nipate majina lakini pia na takwimu zao ili niende nikafanye ushughulikiaji wa jambo hili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake

Na. 652

**Uhitaji wa vifaa tiba katika Hospitali za Wilaya zinazojengwa**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya vifaa tiba katika Hospitali za Wilaya zinazojengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali ilitenga shilingi bilioni 7.1 kwa ajili ya vifaa tiba vya kinywa/meno na macho kwa hospitali 71. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 15.5 kwa ajili ya vifaa tiba kwenye hospitali 31 zinazoendelea na ujenzi kila moja imetengewa shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali zote nchini ili kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini katika Mkoa wetu wa Katavi katika Jimbo la Nsimbo tuna *x-ray* ambayo Serikali imetupatia lakini *x-ray* hiyo imeshindwa kufanyakazi kutokana na kwamba hatuna mtaalam wa mionzi.

Je, ni lini Serikali itatupatia mtaalam wa mionzo ili *x-ray* iweze kufanyakazi kwa kuwahudumia wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili; katika Wilaya ya Tanganyika Kata ya Ilangu wananchi ususani kinamama

wajawazito wamekuwa wakifata huduma mbali sana kutokana na kwamba hawana kituo cha afya; je, ni lini Serikali itatujengea kituo cha afya katika Kata hiyo ya Ilangu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Martha Mariki, la kwanza hili la wataalamu wa mionzi, hivi karibuni katika mwaka huu wa fedha Serikali imeajiri watumishi wa kada ya afya 8,000 na tayari katika matangazo yale wakati yanatolewa ilikuwa tunatafuta watalamu wa mionzi ya *x-ray* 69. Lakini nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba katika ajira hizi walipatikana watumishi 61 tu na hizi nafasi nyingine zilizosalia tutazitangaza upya ili kuweza kuwapata watalam hawa wa mionzi na tuweze kuwapeleka maeneo mbalimbali nchini ambapo Serikali imewekeza fedha nyingi katika ununuzi wa vifaa tiba ikiwemo mitambo ya mionzi na kule Nsimbo napo tutapaangalia kwa ajili ya kuwapeleka watalamu hawa wa mionzi.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la Kituo cha Afya katika Kata ya Ilangu iliyopo kule katika Wilaya ya Tanganyika, tutatuma timu ya wataalaam kwa ajili ya kwenda kufanya tathimini katika Kata ya Ilangu, kuona idadi ya watu waliokuwepo pale na vile vigezo vinavyotakiwa vya umbali kwenda kufata huduma ya afya na kadhalika na baada ya tathimini hiyo kufanyika tutapata taarifa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kuweka katika mipango yetu kuhakikisha kwamba wananchi wa Kata ya Ilangu wanapata huduma ya afya iliyobora kwa kupata kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa kituo cha afya cha Kata ya Nyang'hwale kinatoa huduma zaidi ya miaka 30 kuhudumia kata zifuatazo; Kata za Shabaka, Kaboha, Busolwa, Nyabulanda, Nyijundu, Mwingiro

hakina huduma ya *x-ray* je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hiyo ya *x-ray* kwenye Kituo cha Afya cha Nyang'hwale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia imeweka kipaumbele katika kuhakikisha wananchi wake wanapata afya iliyobora kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya afya vilevile kwenye vifaa tiba na katika bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 112 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ikiwemo vifaa vya mionzi kama vile *x-ray* na pale tutapoanza ununuzi wa vifaa hivi tiba tutaweka kipaumbele kwa ajili Kituo cha Afya cha Kata ya Nyang'hwale anapotoka Mheshimiwa Amar kule. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma Xaday, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka vifaa tiba vya kisasa katika Hospitali ya Wilaya ya Hanang kama *ventilator, anesthesia machine* na *diathermy* ili koboresha huduma za afya ya mama na mtoto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba hospitali zote za Wilaya zinakuwa zina vifaa tiba vya kisasa na tayari tumeshapeleka fedha kwa wenzetu wa *MSD* kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. *MSD* imeanza kupeleka vifaa hivi katika Hospitali za Wilaya mbalimbali hapa nchini. Nitakaa na Mheshimiwa Hhayuma kuweza kuona Hospitali ya Wilaya ya Hanang ipo katika awamu

ipi ya kupokea vifaa tiba hivi vya kisasa katika Hospitali ya Wilaya ya Hanang.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kituo cha Afya cha Ngw'angw'ali na Ngulyati Wilaya ya Bariadi kina upungufu wa vifaa tiba; je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba vya kutosha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu upelekaji wa vifaa tiba Bariadi kama nilivyotoka kusema hapa awali, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 112 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kote nchini na katika hivyo tutahakikisha yale maeneo yenye uhitaji mkubwa yanapata vifaa tiba hivi ikiwemo kule Bariadi alikokutaja Mheshimiwa Midimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Hospitali ya Mji wa Mafinga inahudumia watu wengi sana pale, nini mkakati wa Serikali kuongeza vifaa tiba vya kisasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali hii ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha kwamba vifaa tiba vya kisasa vinakuwepo katika hospitali zote za Wilaya na vilevile katika vituo vyetu vya afya vya kimkakati. Katika kuhakikisha hilo linafanyika Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 112 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba hivyo vya kisasa na tutahakikisha pia Hospitali ya Mji wa Mafinga nayo inaongezewa

vifaa tiba kama ilivyofanyiwa katika mwaka wa fedha huu tunaomaliza sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu sasa aulize swali lake.

Na. 653

**Kuigawa Shule ya Msingi Mwanhuzi – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuigawa Shule ya Msingi Mwanhuzi kwa kuwa shule hiyo ina wanafunzi 1,400?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Shule ya Msingi Mwanhuzi ina changamoto ya mlundikano wa wanafunzi. Katika kutatua changamoto hiyo katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali kupitia Mradi wa *BOOST* imepeleka shilingi milioni 348.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya katika Kata ya Mwanhuzi. Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo, changamoto hii itakuwa imetatuliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Shule husika ililetewa fedha shilingi milioni 80 kwa ajili ya kujenga bweni la watoto wenye mahitaji maalum, je, ni lini Serikali italeta fedha za kukamilisha bweni hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Komanya amekuwa akifuatilia sana shule hii ya Mwanhuzi na alinieleza nilipokutana naye ofisini kwamba ndipo alipotokea yeye kwenye kata hiyo na atahakikisha kwamba fedha hii shilingi milioni 348 inapatikana, kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Leah kwa hili.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la nyongeza la bweni ambalo lilianzwa kujengwa katika shule hii hii ya Msingi ya Mwanhuzi. Serikali ilipeleka shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa bweni kwa watoto wenye mahitaji maalum katika shule hii na sio shule hii pekee yake bali ilipeleka nchi nzima kwa ajili ya ujenzi wa mabweni haya, lakini baada ya kupeleka fedha hizi ujenzi ule haukukamilika na changamoto hii tunaifahamu na timu ya wataalam ilitumwa kwa ajili ya kufanya tathmini kwenye mabweni yote na mabwalo yote ambayo yalipelekewa fedha na hayakukamilika. Baada ya tathmini hiyo kufanyika sasa tupo katika mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka kukamilisha ujenzi wa mabweni haya na mabwalo haya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Aida Khenani.

Na. 654

**Kusamehe kodi katika Sekta ya Elimu na Afya**

**MHE. AIDA J. KHENANI K.n.y. MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isisamehe kodi na kuondoa baadhi ya tozo katika Sekta ya Elimu na Afya ili kuvutia taasisi binafsi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa misamaha ya kodi katika Sekta ya Elimu na Afya kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332:-

(i) Wafanyabiashara wanaojihusisha na utoaji wa huduma za afya na elimu wanasamehewa kulipa kodi ya makampuni yanayotangaza kupata hasara kwa mfululizo wa miaka zaidi ya mitatu;

(ii) Mchango wowote anaofanya mfanyabiashara kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Elimu anajirejeshea kama gharama wakati wa kutengeneza faida;

(iii) Taasisi yoyote iliyoanzishwa kwa ajili ya kujishughulisha na uendelezaji wa elimu na afya au kutoa huduma za umma kwenye Sekta za Afya na Elimu imepewa hadhi ya *charitable organization* na kupata unafuu wa kodi.

(b)Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148:-

(i) Msamaha wa kodi umetolewa katika ujenzi wa majengo kwa ajili ya kutoa huduma za afya na elimu kwa jamii;

(ii) Bidhaa na huduma zinazoingizwa nchini na Serikali au kununuliwa katika soko la ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika Sekta ya Afya na Elimu zimesamehewa Kodi ya *VAT*; na

(iii) Madawa na vifaa vya utabibu na huduma za afya zilizoorodheshwa katika *para 7* la jedwali la kwanza la misamaha zimesamehewa Kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miongozo na taratibu za usimamizi wa kodi ili kuimarisha biashara na kuvutia wawekezaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, natambua msamaha ambao umetajwa na Serikali, lakini pamoja na msamaha unaotolewa wa kodi unakuwa sawa kwenye hizi taasisi lakini wanapotoa hizi huduma, wanatoa kwa gharama tofauti tofauti. Serikali ipo tayari kutoa mwongozo sasa katika hizi gharama zinazotelewa kwenye hizi taasisi binafsi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani bado kuna changamoto ya Kodi ya Forodha kwa vifaa tiba pamoja na dawa.

Je, Serikali iko tayari kutoa hizi kodi zote kama ilivyotangaza kwenye magari yanayotumia umeme ili kutoa kipaumbele kwa afya za Watanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa taasisi ambazo zinafanya biashara zinastahiki kutoa kodi inayostahiki kwa mujibu wa sheria, ambazo zinatoa huduma tu zinapata hadhi ya *charitable organization* na zitapata unafuu wa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, Serikali inatambua umuhimu uliopo katika elimu na afya, tunaendelea kuboresha miongozo mbalimbali ya kodi ili kila wakati tuweze kufikia malengo ya utoaji huduma bora kwa wananchi wetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 655

**Kuiwezesha SUMA JKT iweze kukopa**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuiwekea SUMA JKT mazingira rafiki ili iweze kukopa na kutekeleza miradi yake kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT wanaruhusiwa kukopa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kama ilivyo kwa mashirika mengine ya Serikali. Hivyo shirika litatakiwa kuwa na hali nzuri ya kifedha inayothibitisha uwezo wa taasisi kukopa na kulipa.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na

Misaada ya mwaka 2020 umeelekeza hatua muhimu za kuzingatia kwa Wizara au Taasisi ya Serikali ikiwa inaomba mkopo, dhamana na msaada, kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa naomba kuuliza Serikali, je, iko tayari kuwa na mpango mahsusi wa kuisadia SUMA JKT katika kuhakikisha kwamba tunajitosheleza katika suala zima la chakula na mafuta ya kula? Mipango mahsusi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kuangalia vipengele mahsusi vya kusaidia mashirika yake na mashirika mengine, lakini ushauri wake pia tumeuchukua na tunaenda kuufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 656

**Ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha *Standard Gauge***

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kilometa 1,000 za reli ya *Standard Gauge* kati ya Mtwara - Mbamba Bay na Songea – Ludewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili wa ujenzi wa kilometa 1,000 za reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara hadi Mbamba Bay na matawi yake ya kuelekea Liganga na Mchuchuma. Aidha, taarifa hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali, ilionesha kuwa mradi huu unaweza pia kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership - PPP)*.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kumuajiri Mshauri wa Kifedha *(Transaction Adviser)* ili aweze kufanya mapitio ya upembuzi uliokamilika mwaka 2016 kwa lengo la kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mwekezaji kwa utaratibu wa ubia *(PPP)*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mradi huu ni sehemu ya mpango ambao upo kwenye Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya nchi yetu Awamu ya Tatu ambao mwezi Julai unafikia hatua ya miaka mitatu ya utekelezaji. Ni maandalizi gani ya awali ambayo Serikali imeyafanya kuonesha kwamba ina dhamira ya dhati kujenga mradi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mradi huu ni sehemu ya mradi funganishi wa *Mtwara Development Corridor* ambayo makubaliano ya mradi huo ulifanyika Lilongwe - Malawi Novemba, 2004 na marais wanne wa hizi nchi nne.

Je, ni lini Serikali sasa kama mnufaika mkuu utarudisha utaraibu wa marais hao wanne kukutana na kuweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi huu wa reli pamoja na miradi mingine ndani ya *Mtwara Development Corridor? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mbunge wa Masasi Mjini, Mheshimiwa Idelphonce Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa mradi huu na Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara na kwa swali la kwanza anapenda kujua maandalizi ya awali ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali tumeanza maandilizi ya awali, kwanza tumeanza vikao ndani ya Serikali pamoja na kufanya vikao na wadau mbalimbali na hivi ninavyosema tutakuwa na kikao kingine ambacho kimeitishwa na Mamlaka ya Bandari nchini kitakachofanyika tarehe 22 hadi 23 pale Mtwara na Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa katika mkutano huu kwa sababu ndio unaenda kuifungua *Mtwara Corridor* yote na wadau wengine ni pamoja na *RAS* kwa maana ya Mamlaka ya Mkoa wa Lindi, Mtwara yenyewe pamoja na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa ajili ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi, ni kwamba mradi huu kwa kuwa kwanza kuna makampuni zaidi ya matano kutoka nchi mbalimbali kutoka nchi ya Uingereza, Canada, Marekani, Afrika Kusini, Croatia, Morocco wameonesha nia katika uwekezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* na kwa maana hiyo, changamoto kubwa ilikuwa katika kikwazo ambacho kilichokuwepo kupitia Sheria ya *PPP* ambayo

Bunge lako tukufu wiki iliyopita imepitisha na kufanya mabadiliko madogo kwenye sheria hiyo.

Kwa hiyo, tunaamnini mapatano na mikutano itakayofuata sasa katika makampuni kutoka nchi hizi watakuja moja kwa moja kuwekeza kwa kuwa tayari tulishaanza kufanya nao mikutano hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema kwamba hivi karibuni Bunge lako tukufu limefanya marekebisho ya Sheria ya *PPP* ili kuwezesha miradi kama hii kutekelezwa kwa urahisi.

Je, Serikali inatoa kauli gani sasa katika kuharakisha utekelezaji wa mradi huu ambao unasubiriwa kwa hamu kwa wananchi wa maeneo hayo husika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chikota kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina hamu kubwa sana katika kutekeleza mradi huu na ndio maana Serikali imeanza pia kulipa fidia. Nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zaidi ya takribani shilingi bilioni 15 katika kulipa huu mradi wa Liganga na Mchuchuma. Kwa hiyo, Serikali inaona umuhimu mkubwa wa mradi huu na ndio maana pia tumeitisha vikao hivi mara moja mara baada ya kubadilisha sheria yetu ya *Public Private Partnership* kwa maana ya ubia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwamba kazi ya mshauri ilifanyika toka mwaka 2016 ikiwa ni pamoja na uthamini kwenye eneo ambalo reli hii itakwenda kupita.

Ni lini sasa Serikali itaanza kulipa fidia kwa wananchi waliopo kwenye eneo ambalo reli hii ambapo mradi unaenda kutekelezwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimekwisha kusema kwamba upembuzi yakinifu ulikwishafanyika tangu miaka hiyo ya 2016 na Serikali hatua iliyofikia sasa ni kumuajiri *Transaction Advisor* kwa maana ya Mshauri wa Kifedha ambaye ndiye atakayetupa miongozo yote hadi kulipa fidia, lakini pia kupitia mthamini mkuu kwa sababu hili jambo lilishafanyika miaka mingi kwa vyovyote vile kutakuwa na haja ya kurudia kupitia daftari ambalo lilikuwa limeandaliwa kipindi hicho, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, samahani, Mheshimiwa Omari Kigua nilikuona umesimama.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, miaka mitatu iliyopita Serikali katika mpango wake wa maendeleo ilijielekeza kwamba itajenga *SGR* kwa reli hii ya kuanzia Tanga – Moshi - Arusha hadi Musoma. Je, mpango huo bado upo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kigua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali itajenga reli hiyo ya Dar es Salaam – Tanga - Moshi mpaka Arusha, lakini kwa sasa tuna awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilikuwa ni kujenga reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na awamu ya pili kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma. Mara tutakapokamilisha hizi ndipo tutakapokuja katika hii reli ya kutoka Dar es Salaam – Tanga - Moshi mpaka Arusha na mpango huo uko vilevile.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo kwamba Serikali ina nia hiyo, lakini kwa sasa tunakamilisha hizi ambazo tumekwishaanza, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zaytun Swai.

Na. 657

**Ujenzi wa barabara ya Karatu – Mbulu – Singida**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Karatu – Mbulu – Singida kilometa 190?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Karatu – Mbulu – Singida ni sehemu ya barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – *Sibiti River* – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilometa 389. Serikali imeanza

ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii ambapo sehemu ya Mbulu – Garbabi kilometa 25 kazi zinaendelea, sehemu ya Labay – Hydom kilometa 25) mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 19 Mei, 2023 na sehemu iliyobaki itajengwa kupitia Mpango wa *EPC + F* wa barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – *Sibiti River* – Lalago – Maswa ambapo mkandarasi amepatikana na mkataba wa kuanza ujenzi umesainiwa tarehe 16 Juni, 2023, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Daniel Awack nashukuru sana Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini barabara ya kutoka Redio Habari Maalum kwenda Hospitali ya Wilaya ya Arumeru itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, sijamsikia vizuri Mheshimiwa barabara aliyoitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, rudia jina la barabara.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini barabara kutoka Redio Habari Maalum kwenda Hospitali ya Wilaya ya Arumeru kilometa tatu itajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo tunayafanyia kazi sana ni pamoja na kupeleka barabara za lami kwenye maeneo yanayotoa huduma za jamii kama hospitali.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Ujenzi pamoja na wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tutashirikiana kuhakikisha kwamba hii barabara ambayo ni fupi sana kilometa tatu inafanyiwa usanifu na kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa na mimi swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magugu – Mbuyu wa Mjerumani – Mbulu ni barabara muhimu sana kwa wakazi wa Mbulu na Babati, lakini kipande cha Mbuyu wa Mjerumani – Mbulu ni hatarishi sana kwa kipindi cha mvua.

Sasa ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Daraja la Magala hadi Mbulu imeshakamilishwa kufanyiwa usanifu wa kina na tayari daraja tumeshajenga. Tunachofanya sasa hivi kwenye hii barabara ni kujenga kwa kiwango cha zege maeneo yote hatarishi na hasa kwenye *escapement,* lakini wakati huo tukiwa tunatafuta fedha kujenga barabara yote hii kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Mombo – Soni – Lushoto ni barabara nyembamba sana, ni mlimani, ni kona kali na

imewekewa mpango kwa ajili ya kupanuliwa. Nataka kujua, je, mpango huo bado upo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakiri na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyotaja ya Mombo hadi Soni ni barabara ya lami ilijengwa zamani na ni nyembamba sana na ipo kwenye miinuko. Ni kweli kwamba Serikali ina mpango wa kuiboresha kwa maana ya kuipanua, kupunguza kona na kupunguza ile miinuko ili barabara hii iwe salama kwa watumiaji wote wanaoitumia kutoka Mombo kwenda Lushoto na Mlalo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Bagamoyo, Kibaha Mjini na Kisarawe wamepewa ahadi ya ujenzi wa barabara yao ya lami ya Makofia – Mlandizi – Kisarawe kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi hii inayoendelea.

Je, ni lini itaingia kwenye kusainiwa mikataba kama ilivyofanywa barabara za juzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo yetu na hasa inayounganisha barabara ya Bagamoyo na hii barabara ya Morogoro. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kitu cha kwanza ambacho kitafanyika kwanza ni kulipa fidia kwa wananchi ambao tayari walishaainishwa ili

waweze kupisha barabara na tumetenga fedha kwa mwaka ujao kwa ajili ya kuanza hiyo barabara ya Makofia – Mlandizi kwenda Mzenga huko Kisarawe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 658

**Barabara ya Ulyankulu – Urambo – Ussoke – Tutuo – Sikonge – Mbeya – Mpanda**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaendeleza barabara ya Mpanda - Kahama ili ifike Ulyankulu - Urambo - Ussoke - Tutuo - Sikonge hadi Mbeya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANROADS* inaendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hizi kwa awamu kwa kiwango cha lami ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya kutoka Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu hadi Kahama urefu wa kilometa 457 umekamilika na sehemu ya barabara kutoka Urambo hadi Ussoke kilometa 45 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara za Ulyankulu hadi Urambo na Tutuo hadi Ussoke na baada ya kukamilika kwa usanifu huo Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo katika kuchochea uchumi wa wananchi wa Urambo, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ikitokea Kahama – Ulyankulu – Urambo – Ussoke – Tutuo – Sikonge ili waendelee wasafiri mpaka Mbeya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kadri tunavyofungua nchi na kuunganisha miji barabara aliyoitaja ni muhimu sana hasa kwa sababu itapunguza sana urefu wanaosafiri watu wa kutoka Kahama na hata watu wanaotoka njia ya Kigoma ambao kama wanaenda Mbeya hawana sababu ya kupita Mjini Tabora. Ndio maana tumesema tunaendelea kuhakikisha kwamba tunafanyia usanifu hiyo barabara ya kutoka Ulyankulu hadi Urambo na kipande cha Ussoke hadi Tutuo ili kuwapunguzia wananchi hawa umbali mrefu wa kusafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachotakiwa sasahivi tunatafuta fedha sasa ili barabara hii ifanyiwe usanifu na ijengwe kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kufungua hilo eneo la Wilaya ya Urambo, lakini pia na kuunganisha na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara ya kutoka Mbamba Bay hadi Lituhi imo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, Serikali imefikia wapi katika suala hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja ina sifa mbili, kwanza ni barabara ya ulinzi lakini pia ni barabara

ambayo inaambaa ambaa na ziwa kutoka Mbamba Bay kwenda Lituhi. Barabara hii tulishafanya usanifu na sasa kinachotafutwa ni fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami ambapo itaunganisha Bandari ya Mbamba Bay ambayo tayari kuna lami, lakini na Lituhi ambako sasa Mheshimiwa Mbunge anakubali tunajenga kuanzia Amani Makolo mpaka Bandari ya Ndumbi. Kwa hiyo, kipande kilichobaki hapo tukishaunganisha tutakuwa tumekamilisha barabara za lami na itakuwa ni rahisi sana kufanya ulinzi, lakini pia kufungua Wilaya ya Nyasa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 659

**Kufikisha umeme kwenye vijiji – Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, lini zoezi la kufikisha umeme katika vitongoji, vijiji na mitaa ambayo haina umeme litakamilika Wilayani Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili ambapo vijiji vyote visivyokuwa na umeme vitafikiwa na huduma hiyo. Aidha, vijiji saba tu vya Wilaya ya Kakonko visivyokuwa na umeme vitakamilika kuwashiwa umeme ifikapo tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha uhakiki wa vitongoji 36,101 visivyo na huduma ya umeme na kuandaa mradi kabambe wa kusambaza umeme katika vitongoji vyote unaoitwa *Hamlet Electrification Project (HEP)* vikiwemo vitongoji 196 vya Wilaya ya Kakonko. Mradi huu utatekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa mwaka 2023/2024 Jimbo la Buyungu Wilayani Kakonko litapatiwa fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji 15 vya kuanzia, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lipo tatizo la umeme kukatika-katika hali inayosababisha vifaa vya umeme vinavyotumiwa na wananchi kuharibika.

Nini mkakati wa jumla wa Serikali kuhakikisha kwamba tatizo hili linaisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja Wilayani Kakonko kwa ajili ya kueleza mazuri sana haya ya Serikali ambayo Serikali inaendelea kuyafanya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Kamamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakiri kwamba bado kuna maeneo yanayo tatizo la kukatika umeme na maeneo mengine kukatika ni kwingi, maeneo mengine ni kudogo, maeneo mengine tumepunguza kwa sehemu kubwa. Eneo analolisema linayo *line* ya siku nyingi ya kilometa zaidi ya 280 inayohudumia maeneo ya Kakonko, Buhigwe, Kasulu na Kibondo ambayo sasa imeunganishwa na *line* ya Gridi ya Taifa inayotokea Nyakanazi kwenda mpaka maeneo hayo yenye kilometa takribani 25.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii ambayo tunamaliza tumefunga kifaa kinachoitwa *Auto Voltage Regulator* ambacho

kinaongeza nguvu ya umeme unaosafiri kwa muda mrefu ili angalau umeme uweze kufika mwingi kwa wadau mbalimbali. Katika bajeti inayokuja tumetenga pesa kwa ajili ya kwenda kuirekebisha na kuifanyia marekebisho makubwa hii *line* ikiwa ni pamoja na kubadilisha miti iliyochakaa, kubadilisha vikombe, lakini pia kubadilisha maeneo kidogo ya waya ambayo yamekuwa yakisababisha umeme kukatika kwenye maeneo haya.

Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi kinachokuja cha mwaka wa fedha unaokuja katika kipindi kifupi ataona mabadiliko ya kurekebisha hii *line* ili iache kuwa inaathirika sana na matatizo ambayo yamekuwa yakitokea.

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo la pili, mimi niko tayari kwenda pamoja na yeye kuwaambia wananchi mipango mizuri kabisa ya Serikali, lakini pia na kusisistiza wao kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ambayo inapeleka umeme katika maeneo hayo, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mkoa wa Simiyu una jumla ya vitongoji 2,649 lakini vitongoji 1,713 havijafikiwa na umeme; je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji hivyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa vitongoji vyote 36,101 vya Tanzania Bara ambavyo havina umeme, na tayari mradi umetengenezwa tunaouita kwa kifupi *HEP – Hamlet Electrification Project* na tunatarajia mwaka wa fedha wa 2024/2025 tutaanza kuutekeleza na utaigharimu Serikali jumla ya kama shilingi trilioni 6.7.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuanzia katika mwaka wa fedha unaokuja Mkoa wa Simiyu, lakini kwenye majimbo yote mbalimbali yatapata vitongoji angalau 15 kwa kila jimbo. Kwa

hiyo, nimuombe Mheshimiwa Lucy kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi anakotokea washirikiane ku-*identify* vile vitongoji 15 vya kuanzia ili kupunguza changamoto, lakini katika ule mwaka mwingine tutaanza sasa kupeleka umeme katika vitongoji vyote ambavyo vinahusika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hii bajeti tuliyopitisha ya juzi ni kama mlishauriwa kuangalia ukubwa wa majimbo, siyo? Maana jimbo lenye kata nne kwa mfano, linafanana na lenye kata 36, lenye kata 39, hapo itakuwaje hapo wote wanapewa 15 vijiji na mitaa ama? Maana mlituahidi, sasa hili ni jibu unatoa leo, mnaenda kuangalia na ukubwa wa majimbo au ukubwa wa majimbo utakuja 2024/2025?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa bajeti tuliyokuwanayo sasa na kwa uhalisia uliokuwepo tumeona kipindi hiki cha kuanzia iwe ni vitongoji 15 kwa kila jimbo kwa sababu ni mwaka wa fedha mmoja, lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025 hivi vitongoji 36,101 vyote tunatarajia kuvipatia fedha. Kwa hiyo, kipindi hicho sasa tutaanza na wale wenye mahitaji makubwa zaidi tukielekea kwenye mahitaji madogo zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya kila majibu yanayotolewa na Serikali naona yanapigwa makofi. Sasa sijaelewa hawa ndio wenye majimbo yenye kata nne ama vipi? Sijajua, lakini Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, mimi leo nauliza je, ni lini sasa mtatupa jibu la uhakika la kutokukatika-katika umeme kwenye Jimbo letu la Temeke? Kwa sababu, mwaka 2021 hapa mlituambia mwezi wa Disemba umeme utakuwa sawasawa, mwaka 2022 mwezi Aprili utakuwa sawasawa, sasa ni mwaka 2023, je, ni lini? Tunaomba jibu la uhakika umeme kutokukatika-katika Temeke.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu za kukatika umeme kwenye maeneo mbalimbali zinatofautiana. Wako ambao umeme unakatika kwa sababu miundombinu yao imepita kwenye maeneo ya mapori na inasongwa sana na miti. Wako wenye maeneo mengine umeme unakatika sana kwa sababu wako kwenye maeneo yenye radi na mvua kali kwa hiyo, zile radi zinaathiri vile vifaa.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mengine kama ya mjini ambako miundombinu imezidiwa na matumizi ya wananchi, lakini pia yako mambo mengine shughuli za kibinadamu za kugonga nguzo kwa magari na vitu kama hivyo vinavyosababisha matatizo hayo yatokee.

Nimuahidi Mheshimiwa Kilave kwamba kwenye mradi wetu wa Gridi Imara kwanza tunaongeza uwezo wa mitambo yetu wa kupeleka umeme kwenye maeneo mbalimbali, na yeye ni shahidi kwamba kwenye maeneo ya Temeke tumeanza kupitisha miundombinu chini kwa maana ya *underground* ili tupunguze zile habari za malori na magari mengine kugonga zile nguzo.

Mheshimiwa Spika, sasa mradi huu wa Gridi Imara pamoja na miradi mingine ambayo tunayo ambayo tayari umeshaona inatekelezwa tunatarajia itakapokamilika katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili ijayo maeneo mengi sana matatizo ya kukatika kwa umeme yatakuwa yamekwisha, lakini yapo matatizo mengine madogo madogo ya transfoma imezidiwa kwa sababu wakazi wameongezeka kama maeneo ya Kariakoo na vitu kama hivyo, tunavifanyia kazi kwa kadri vinavyotokea. Tunaomba tuendelee kushirikiana kupeana taarifa pale changamoto zinapotokea ili tuweze kuzifanyia kazi.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi, Mkoa wa Katavi kwa ujumla una shida kubwa ya umeme kwa ujumla kwa sababu majenereta yaliyopo yameshindwa kuhimili idadi ya watu wanaotumia umeme. Serikali ina mpango gani wa dharura wa kupeleka jenereta litakaloenda ku-*support* umeme kwenye Mkoa wa Katavi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali katika mpango wa muda mrefu tunajenga sasa *line* ya kutoka Tabora – Ipole – Inyonga mpaka Mpanda Mjini kwa ajili ya kuhakikisha kwamba gridi imeufikia Mkoa wa Katavi, lakini katika njia za muda mfupi kama alivyouliza naomba baada ya hapa tutashauriana naye ili tuone tatizo ni kubwa kiasi gani na tuone ni wapi tunakoweza kupata mashine ya dharura ya kwenda kuongeza nguvu katika Mkoa wetu wa Katavi ili kipindi ambacho tunakamilisha upelekaji wa gridi basi wananchi waendelee kupata huduma ya umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 660

**Wanafunzi wote kupata Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanafunzi wote waliomaliza kidato cha sita wanapata mkopo wa elimu ya juu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu mwaka hadi mwaka ili kuongeza wigo wa wanufaika. Bajeti ya mikopo iliongezeka kutoka shilingi bilioni 570 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 654 mwaka 2022/2023. Pia mwaka 2022/2023 shilingi bilioni tatu zilitengwa kwa ajili ya *Samia Scholarship* iliyonufaisha wanafunzi 593 waliohitimu kidato cha sita wenye ufaulu wa juu kwenye masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kupanua fursa za mikopo kwa wahitimu wa kidato cha sita, Serikali imeingia mkataba wa mahusiano na Benki ya NMB ili kutoa mikopo yenye riba nafuu ya asilimia tisa kwa wazazi/walezi kwa ajili ya kugharamia elimu ya watoto wao katika ngazi ya elimu ya juu na kati. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fursa za mikopo ya elimu ya juu kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuhakikisha kila mhitimu wa kidato cha sita mwenye sifa anapata mkopo kwa ajili ya kugharamia elimu ya juu, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na hayo majibu yanayoridhisha kiasi, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hawa wanafunzi wanaokwenda kusoma katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, naomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwa sababu hawa wa maendeleo ya jamii wanaegemea kwenye upande wa afya na elimu; je, wako katika kundi la kupata mikopo au ni wale wa *VETA* na vyuo vingine vya afya tu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba inatoa mikopo kwa wanafunzi wote wa elimu ya juu pamoja na wale wa elimu ya kati. Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatarajia kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa wa elimu ya kati kama ilivyosomwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka ujao wa 2023/2024 Serikali inatarajia kuanza kutoa mikopo kwa wananfunzi wa elimu ya kati katika kada za ualimu, afya pamoja na sayansi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kupanua wigo wa kutoa mikopo hii katika kada nyingine kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na uwepo wa bajeti, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa fursa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanafunzi wenye ulemavu ambao wanafanikiwa kufika hatua hii ya elimu ya juu ni ndogo sana yaani idadi ya wanafunzi ambao wanafanikiwa kufika hatua hii ya eleimu ya juu ni ndogo sana, na kwa kuwa kundi hili linakabiliwa na changamoto nyingi za kimaisha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo hii ya elimu ya juu kama ruzuku kwa kundi hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba miongoni mwa vigezo au sifa za upataji wa mikopo, mojawapo ni kwa wenzetu wenye mahitaji maalum wakiwepo watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, kwanza tumeanza na kipaumbele kwa hawa, lakini tunatoa kama mikopo.

Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mbunge yeye anataka tufanye kama ruzuku, naomba tulichukue pendekezo lake hili au ushauri wake huu twende tukaufanyie kazi, tufanye tathmini ya wangapi hawa watu wenye ulemavu, na tuweze kuangalia namna bora ya kufanya, kama tulivyofanya kwenye *Samia Scholarship,* Mheshimiwa Rais alitoa fedha hizi zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya watoto waliofanya vizuri. Nadhani na hili la watoto wenye ulemavu linawezekana, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Nicholaus Ngassa.

Na. 661

**Athari za mafuriko katika Jimbo la Igalula**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA K.n.y. MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza: -

Je, nini mpango wa kuweka miundombinu ya kuhifadhi maji ya mvua badala ya kusababisha mafuriko Kata za Loya na Miswaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bwawa katika Kata ya Miswaki, lakini taarifa za kitaalam zilionesha eneo hilo kutokukidhi. Usanifu wa bwawa uliofanyika katika eneo la Kata ya Kizengi ulileta matokeo mazuri na Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa bwawa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kukamilika kwa bwawa hilo kutaboresha huduma ya maji kwenye vijiji kumi vya Kata za Loya, Miswaki na Kizengi. Aidha, wananchi wanaofanya shughuli za kilimo maeneo ya mabondeni wanashauriwa kuhama kipindi cha mvua kubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza niishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa Igalula kwa kuanza kujenga bwawa kwa ajili ya kutatua changamoto, lakini tatizo hili pia lipo Igunga kwenye Kata za Itumba, Lugubu na Nguvumoja. Maji yamekuwa yakijaa kwa sababu ule ni ukanda wa Bonde la Mbeya ambalo linakwenda mpaka Igalula.

Je, ni lini Serikali itafanya kwa wananchi wa Jimbo la Igunga katika kutatua changamoto hii? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Jimbo la Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kupokea shukrani kwa Serikali kutekeleza wajibu wake, na kwa maeneo ya kata ulizozitaja kwenye Jimbo la Igunga Mheshimiwa Mbunge na yenyewe pia tutaendelea kuwaletea wataalam waweze kufanya usanifu na tuweze kuchimba mabwawa maeneo yote ambayo yatasaidia kuondosha na kupunguza mafuriko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, katika Kata za Fukayosi na Makurunge katika Jimbo la Bagamoyo, *DAWASA* Chalinze wamesambaza miundombinu ya maji mwaka wa pili sasa lakini maji hayatoki.

Je, ni lini sasa maji katika maeneo haya yatatoka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba niwe nimelipokea, nikalifanyie ufuatiliaji kwa nini maji hayatoki na usambazaji umefanyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa tatizo la maji kutiririka hovyo wakati wa mvua ni tatizo kubwa sana kwa maeneo ambayo yako kwenye milima ukiwemo Mkoa wa Kilimanjaro.

Ni lini sasa Serikali italeta muswada hapa Bungeni ili nyumba zote zinazojengwa ziwekewe vikinga maji na kutumia maji yale ya mvua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuleta muswada niseme nimelipokea, lakini sisi kama Wizara tayari tumejipanga na kuona kwamba mabwawa tutakayoyachimba tutaweka kwenye maeneo yote ambayo ni korofi kwa sasa, na tumshukuru Mheshimiwa Rais

ameweza kutupatia vitendea kazi, tumeshanunua seti tano kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, lakini hilo alililoliongea Mheshimiwa Mbunge naomba niseme nimelipokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 662

**Changamoto za wachimbaji na wasafirishaji madini Mgodi wa Kebaga**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua kero zinazowakabili wachimbaji na wasafirishaji wadogo wa dhahabu Mgodi wa Kebaga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kebaga kilichopo Wilaya ya Tarime kina madini ya dhahabu ambayo wachimbaji wadogo wanachimba.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wachimbaji hao wanafanya shughuli zao ipasavyo, Wizara kupitia Tume ya Madini imeanzisha kituo kidogo cha ununuzi wa dhahabu katika eneo la Kebaga ambapo wachimbaji huuza madini yao. Aidha, Tume ya

Madini hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha wachimbaji na wachenjuaji wa dhahabu wanafanya kazi hizo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Madini na kushughulikia kero zozote zinazowasilishwa na wachimbaji wa mgodi huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mgodi wa Kebaga wachimbaji wadogo ambao wanachimba pale wanapata wakati mgumu wa kuuza dhahabu kwa sababu wataalam wanaokwenda kufanya tozo zile za dhahabu wanachelewa kwenda pale, hawana siku maalum ya kwenda kufanya tathmini.

Je, lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa siku zile za kwenda kuhakiki ili kutoa nafasi kwa wachimbaji wale kuuza madini yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, upo ushuru unaokusanywa pale na hakuna risiti za *EFD* ambazo zinatolewa, wanapewa risiti za kawaida; je, huu ni utaratibu ambao unakubalika na sheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kuchelewa kununuliwa kwa madini ya wachimbaji wadogo, ninapenda kurejea majibu yangu ya msingi kwamba kwa kufahamu umuhimu wa shughuli za uchimbaji wa madini pale, tumeanzisha kituo kidogo cha ununuzi wa madini na mchimbaji yeyote ambaye ameshachimba madini yake akifika pale tathmini hufanyika na biashara hufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kwamba kunakuwa na ucheleweshaji katika kuwahudumia hawa wachimbaji wadogo na wanatoa risiti ambazo ni za karatasi, kama changamoto hiyo ipo, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki tukutane na tuwasiliane na *RMO* kule tujue changamoto hiyo hutokana na nini ili tuweze kuishughulikia kikamilifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 663

**Serikali kuwawezesha wadau wa michezo kuzalisha vipaji**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha wadau wa michezo kuwekeza katika kuzalisha vipaji vya michezo hasa mpira wa miguu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na kwa ridhaa yako, naomba nitumie sekunde chache kuwapongeza vijana wetu wa Timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* kwa ushindi wa goli moja kwa bila walioupata dhidi ya Niger jana, ushindi ambao unatuweka katika nafasi nzuri na uwezekano mkubwa wa kuweza kupata nafasi ya kushiriki katika Fainali za Mataifa ya Afrika zitakazochezwa mwakani kule Senegal. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo niliwaahidi jana ile milioni 10 yao ya goli la mama kutoka kwa shabiki na mwezeshaji namba moja wa timu ya Taifa itawafikia leo kwa sababu mama hana kona kona, akishaahidi lazima litekelezwe, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abubakari Asenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuwezesha wadau kuwekeza kwenye uzalishaji wa vipaji vya michezo hasa mpira wa miguu imefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kuweka miongozo mahususi ya uanzishwaji na uendeleshaji wa shule maalum za kuibua; kukuza na kuendeleza vipaji *(sports academies);* kuweka mfumo madhubuti wa usajili wa *academia* na vituo vya michezo; kupunguza kodi kwenye vifaa vya michezo kama vile nyasi bandia na viambata vyake; kutoa utaalamu na ushauri katika ujenzi wa miundombinu ya michezo; na kuandaa mashindano ya UMISETA kwa shule za sekondari na UMITASHUMITA kwa shule za msingi ili kuwashindanisha, kuibua na kuendeleza vipaji vyao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninashukuru Serikali kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuna *academies* za mchezo wa mpira wa miguu kama vile *Kilombero Soccernet Academy* ambazo zimesajiliwa rasmi na ziko pale Wilaya ya Kilombero, lakini zina uhaba mkubwa wa vifaa.

Je, kwa dharura, Wizara haioni kwamba inaweza ikachukua hatua za kutafuta vifaa, hata kama ni mipira, *jersey,* ikazipelekea hizi *academies* ambazo zimesajiliwa rasmi na *TFF*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilimwomba Mheshimiwa Naibu Wazri mipira 100 ya vijijini na aliniahidi atanipatia; je, lini

tunakwenda kukabidhi mimi na yeye mipira hiyo Ifakara na kukiamsha pale Ifakara Mjini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa ili usimweke Naibu Waziri mazingira magumu, hilo la pili naomba mkajibiane ukishatoka hapa kwa sababu lilikuja kwako kwa namna ambayo sisi hatuijui hapa ndani, naomba utamjibu peke yake. Hilo la kwanza tujibu wote tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kama nilivyosema kwa sasa Serikali inachoweza kufanya kutokana na upatikanaji wa fedha ni kupunguza kodi kwenye vifaa vya michezo kama vile nyasi bandia na viambata vyake. Haya mengine kwa kadri fedha zitakavyopatikana tutaendelea kuvi-*support* vituo hivi na kuhakikisha vinapata nguvu kupitia Serikalini vilevile, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda. Nilikuwa nimewaona mkiwa mmesimama, lakini muda wetu wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na Serikali kuwapa majibu. Na ninayo matangazo hapa mbele. Tutaanza na tangazo la wageni halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika, nao ni wageni wangu; kwanza, ni wageni wangu kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN),* wachapishaji wa Magazeti ya *Daily News,* HabariLeo na *Daily News Digital,* na hawa ni Ndugu Tuma Abdallah ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Christopher Majaliwa ambaye ni Meneja Huduma za Habari na Lugha za Kigeni, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Felix Mushi ambaye ni Kaimu Mkurugenzi, Kurugenzi ya Uendelezaji Biashara, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Oscar Mbuza ambaye ni Afisa Uhusiano, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine pia ambao wanatoka *Bank of Africa (BOA)* na hawa ni Ndugu Adam Mihayo ambaye ni Mkurugenzi Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Derick Lugemala ambaye ni Mkurugenzi Masuala ya Fedha, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Nandi Mwiyombella, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wanakwaya 45 kutoka *TAG Kinondoni Revival Church* Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kwaya hiyo, Dkt. Yotham Mackenzie, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wanakwaya 15 kutoka Kanisa la *TAG Sahara Spiritual Centre,* Mabibo Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Jane Massawe ambaye ni Mama Mchungaji, lakini pia yupo Ndugu Elininsia Gwambene ambaye ni Mwenyekiti wa Wanawake na Anna Mushi ambaye ni Makamu Mwenyekiti, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na huyu ni Ndg. Nicholas Blake Raynolds anafahamika zaidi kama Bongo Zozo, huyu ni Balozi wa Hiari wa Utalii Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Haya, ahsante sana. karibu sana Bungeni na tunakushukuru sana kwa namna unavyoitangaza Tanzania na unafanya kazi nzuri, unazi-*support* pia timu zetu zikisafiri huku na huko, huwa tunakuona. Kwa hiyo tunakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao ni wetu sisi sote; tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Patrobass Katambi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kutoka Chama cha Wazazi/Walezi, ambao ni Vijana na Watoto Wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa

na Mgongo Wazi Tanzania *(Association for Spinal Bifida and Hydrocephalus Tanzania (ASBAHT),* karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Geophrey Pinda ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Kavuu, Mkoa wa Katavi, karibuni sana. Sijui wako upande gani, sijawaona. Ahaa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na huyu ni Mkurugenzi wa *Skymax Company Ltd.* na Muanzilishi wa *business cards* za kidigitali kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo na hawa ni Waamuzi Wastaafu wa Michezo kutoka Dodoma Mjini, karibu sana. *(Makofi)*

Naambiwa wastaafu halafu naona pale wengine umri mdogo sasa sijajua wamestaafu kwa namna ipi lakini karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Daniel Sillo kutoka Babati Mjini Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni Mwandishi wa Habari kutoka Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Abdallah Chikota ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Angelina Malembeka kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye anatoka Bukoba, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 29 wa Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambao ni Wajumbe wa *CHMT*-Hospitali ya Manispaa ya Mpanda Mjini Mkoa wa Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 86 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni Viongozi wa UWT Kata na Wilaya na Madiwani Viti Maalum kutoka Hanang, Mkoa wa Manyara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Lucy Sabu ambao ni wajumbe wa UVCCM kutoka Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni Mashujaa wa SMAUJATA kutoka Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Neema Lugangira ambaye ni Ndugu Eleonor Silva, *CEO* wa *Unite Parliamentary Network for Global Health* kutoka Lisbon, Portugal huyu ameambatana na Arshiya Singh, Mansoor Amri na Phelister Wegessa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Kundo Mathew ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na hawa wameongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bariadi kutoka Mkoa wa Simiyu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 30 kutoka Kituo cha Kulelea Watoto Yatima cha *DHI Nureyn Islamic Foundation* cha jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Hawa ni wageni wetu ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Rose Busiga kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tarehe 19 Juni, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kupokea sadaka ya mchele iliyoletwa na Mbunge Mstaafu, Mheshimiwa Haroon Pirmohamed. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada mchele huo utagawiwa katika eneo la *basement* karibu na geti la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kila mtu aende yeye mwenyewe kuchukua sadaka hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alishasoma hoja yake hapa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 na sasa ni wakati wa kumsikiliza Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ili aje awasilishe maoni ya Kamati halafu tutaendelea na uchangiaji baada ya hapo.

Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

**MHE.DANIEL B. SILLO- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ikisomwa pamoja na kifungu 9(1)(a) na (b) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuonesha kwa vitendo nia yake thabiti ya kuwaondolea Watanzania umaskini na kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uthubutu wake katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii umekuwa msingi imara katika kutekeleza kauli mbiu yake ya "Kazi Iendelee."

Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake. Vilevile inatambua juhudi za Makamu wa Rais katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuendeleza kampeni za upandaji miti nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Waziri Mkuu atakuwa na madaraka ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo naomba nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika umethibitisha kwamba Bunge ni mahali pa kutoa hoja zenye mashiko na ushahidi na si mahali pa upotoshaji wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa; taarifa hii imegawanyika katika maeneo kumi na mbili kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla kwa mwaka 2022, hali ya uchumi wa dunia; kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili, 2023 inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2021. Ukuaji huu ni chini ya makadirio ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.4 na ulisababishwa na athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha ukame kwa baadhi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa za hali ya uchumi wa dunia na uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

Kwanza, kwa kuwa mfumuko wa bei duniani mwaka 2022 uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.7 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2021. Vilevile mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia wastani wa asilimia 14.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2021. Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya jinsi ya kukabiliana na mfumuko wa bei unaotokana na uagizaji wa bidhaa nchini ili kutokuathiri uchumi wa Taifa.

Pili, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi kweye Sekta ambazo Tanzania ina nguvu ya ushindani *(competitive advantage)* ili kuendelea kukuza uchumi kwa kiwango kinachotarajiwa. Sekta hizo ni Utalii, Kilimo, Mifugo na Madini.

Tatu, kwa kuwa Tanzania imefanikiwa kupata masoko ya mazao ya chakula katika nchi mbalimbali Barani Afrika na kwa kuwa bei ya mazao ya chakula hususan nafaka katika soko la dunia inatarajiwa kupanda katika mwaka 2023 kutokana na kupungua kwa bidhaa hizo katika soko la dunia. Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya nafaka nchini kwani uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba kati ya tani milioni 9.49 za nafaka zinazozalishwa nchini ni tani 13,062 tu ndio huongezewa thamani.

Nne, kwa kuwa soko la bidhaa Tanzania limefanya mauzo ya bidhaa mbalimbali katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 ambapo tani milioni 107.06 za bidhaa mbalimbali zenye thamani ya shilingi bilioni 223.26 zimeuzwa. Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya mazao na bidhaa zitakazokuwa zinauzwa katika soko hilo pamoja na kuongeza idadi ya wanunuzi wanaoshiriki katika kununua bidhaa mbalimbali katika soko hilo.

Vilevile kutoa elimu kwa wakulima juu ya umuhimu wa kuuza bidhaa zao katika soko hilo pamoja na kuangalia namna ya kuunganisha mfumo wa Stakabadhi Ghalani katika Soko la *TMX* kwani bidhaa zinazouzwa *TMX* zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya juu kuliko za Stakabadhi Ghalani. Hatua hizi zitawaongezea wakulima kipato pamoja na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Tano, Kamati inashauri ujenzi wa maghala mapya uendane na ukarabati wa maghala yaliyopo, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza ujenzi wa vyumba vya baridi *(cold rooms)* kwa ajili ya kuhifadhai samaki, mbogamboga, matunda na maua kwa ajili ya kuuza nje ya nchi pamoja na kuongeza leseni za ujenzi wa maghala ya mazao ya kilimo kwa watu binafsi.

Sita, katika mwaka 2022/2023 thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua ilikuwa dola za Marekani milioni 289.6

ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 378.6 mwaka 2021/2022 sawa na upungufu wa asilimia 23.5. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kufufua mashamba ya maua, mbogamboga na matunda yaliyopo Wilaya ya Arumeru katika Mkoa wa Arusha. Ufufuaji wa mashamba haya utaliingizia Taifa mapato ya kigeni pamoja na kurejesha ajira zaidi ya 2000 zilizopotea.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022; katika mwaka 2022 Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021. Katika mwaka 2022 thamani halisi ya Pato la Taifa ilifikia shilingi trilioni 141.873 ikilinganishwa na shilingi trilioni 135.4 mwaka 2021. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika kipindi husika kumechangiwa na athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Changamoto hizi zimepelekea kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa katika soko la dunia, kuathirika kwa mnyororo wa ugavi pamoja na kupanda kwa gharama za bidhaa za msingi kama vile mafuta na ngano.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania inaonyesha kwamba katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/2023 uchumi wa Tanzania ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/2022. Ukuaji huu wa uchumi unaashiria kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa ajira na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa shughuli za kiuchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa na kubaini kwamba Sekta ya Kilimo pamoja na kuwa imechangia asilimia 26.2 katika Pato la Taifa, ukuaji wa sekta hii sio wa kuridhisha kwani Sekta hii imekua kwa asilimia tatu ukilinganisha na ukuaji uliotarajiwa wa asilimia tano. Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba Sekta ya Kilimo inajikita zaidi katika uzalishaji wa mazao ya chakula yanayohitajika nchini pamoja na mazao ya biashara yanayohitajika katika soko la dunia, hatua hii itaongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi pamoja na kupunguza nakisi ya urari wa biashara.

Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ongezeko la bajeti ya Sekta ya Kilimo hadi kufikia shilingi bilioni 970.8 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati inaamini kwamba ongezeko hili linaenda kufanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei; kupanda kwa bei za baadhi ya bidhaa na huduma muhimu ikiwemo chakula na nishati kulisababisha athari za mfumuko wa bei kwa matabaka ya kipato cha chini, kati na juu kuongezeka hadi asilimia 4.7, asilimia 5.8 na asilimia 3.8 mtawalia mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 2.4, asilimia 2.4 na asilimia tatu mtawalia mwaka 2021. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuchochea uzalishaji wa ngano pamoja na mafuta ya kula nchini katika kukabiliana na mfumuko wa bei. Kielelezo namba mbilim kinaonesha Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei kutoka mwezi Aprili, 2022 hadi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni; kutokana na tatizo la uhaba wa dola za Marekani linaloikumba dunia kwa sasa, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuanzisha mchakato wa kununua na kutunza dhahabu kama akiba ya fedha za kigeni. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupata fedha za kigeni kutoka kwa mabenki ya ndani na nje kwa njia ya *currency swap*, kudhibiti soko la fedha za kigeni lisilo rasmi pamoja na kuweka mikakati ya maboresho kwenye soko la fedha za kigeni. Lengo la hatua hizo ni kuwianisha thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni kwenye soko la jumla la fedha za kigeni kuwa sawia na ile iliyopo kwenye soko la rejareja.

Mheshimiwa Spika, biashara ya nje; uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi kufikia mwezi Januari, 2023 urari wa malipo kwa sekta ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 5,261.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,659.3 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kujielekeza zaidi katika kuchochea uzalishaji wa mazao yanayoongoza kuuzwa katika soko la nje kama vile

korosho, katani na pamba ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kupunguza nakisi ya urari wa malipo ya jumla.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali; uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi mwezi Aprili, 2023 deni la Serikali lilikuwa ni shilingi trilioni 79.1 ukilinganisha na deni la shilingi trilioni 69.26 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.9. Ongezeko la deni limetokana na sababu mbalimbali kama zinaovoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba deni letu ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Serikali iendelee kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni. Hii ni kwa sababu deni la Taifa hulipwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima *(first charge)* katika matumizi ya Serikali;

ii. Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati *(semi concessional loans)* ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara;

iii. Mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwe katika miradi ambayo itakamilika na kuanza kuzalisha mapato katika kipindi cha muda mfupi; na

iv. Kuboresha mikakati ya kukusanya mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya umaskini nchini; Kamati inatambua kuwa maendeleo ni pamoja na kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula. Hivyo Serikali iendelee kusimamia vyema sera yake ya elimu bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023; bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023 ni ya pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022-2025/2026 ambapo Serikali ilipanga kukusanya na kutumia shilingi trilioni 41.48 kutoka vyanzo vya nje na ndani. Kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa shilingi trilioni 27.01, misaada na mikopo ya masharti nafuu yalikuwa shilingi trilioni 4.65, mikopo ya ndani ilikuwa shilingi trilioni 5.78 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi trilioni 3.03. Hadi kufika Aprili, 2023 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi trilioni 32.43 kutoka vyanzo vyote ikiwa ni sawa na asilimia 78.18 ya bajeti nzima. Uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato katika kila chanzo ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali za Mitaa; hadi kufikia Aprili, 2023 mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 788.8 sawa na asilimia 78.12 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 1.01. Aidha, Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Halmashauri zenye uwezo mkubwa wa kukusanya mapato, lakini huwekewa ukomo na Wizara ya Fedha na Mipango ulio chini ya uwezo wa Halmashauri husika kukusanya. Vilevile Kamati imebaini bado kuna changamoto ya ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo. Hivyo Kamati inaamini mfumo wa *TAUSI* ambao unasaidia kutambua vyanzo vya mapato vya Halmashauri husika na hivyo kusaidia kukadiria uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato yake.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitarajia kupewa shilingi trilioni 4.65 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali ilikuwa imepokea shilingi trilioni 4.61 sawa na asilimia 99.14. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.5 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti; shilingi bilioni 85.4 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta; na shilingi trilioni 2.22 ni misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwa kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano na Washirika wa Maendeleo *(Development Cooperation Framework)* pamoja na kuimarisha ushirikiano na uhusiano wa kimataifa. Ni kutokana na jitahada zake ndio maana tumeweza kufikia ufanisi wa asilimia 99.14.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya ndani Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ukopaji katika soko la ndani hauathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma ili washiriki katika kununua dhamana za Serikali kwani katika katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na muitikio mdogo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi; katika mwaka 2022/2023 Serikali ilikusudia kutumia shilingi trilioni 41.48, kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 26.47 na shilingi trilioni 15.01 ni matumizi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 36.02 ya bajeti nzima. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 32.43 sawa na asilimia 78.18 ya lengo la mwaka. Fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa shilingi trilioni 20.94 sawa na asilimia 79.1 na shilingi trilioni 11.49 ni matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 76.55. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji huu wa bajeti, ni wazi kwamba hadi kufika tarehe 30 Juni, 2023 bajeti ya Serikali itakuwa imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023/2024; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ulitengewa jumla ya shilingi trilioni 15.01, sawa na asilimia 36.18 ya bajeti ya Serikali ambapo shilingi trilioni 12.31, sawa na asilimia 82 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 2.7, sawa na asilimia 18 ni fedha za nje. Mpango huu ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji; hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Serikali ilitumia jumla ya shilingi trilioni 11.49 ambayo ni sawa na asilimia 76.5 ya bajeti iliyokuwa imetengwa ya shilingi trilioni 15.01 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake ya kuliletea Taifa maendeleo kwa wananchi wake. Muhtasari wa utekelezaji wa miradi katika sekta mbalimbali ni kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya mifugo na uvuvi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kukosekana kwa malisho ya mifugo na hivyo kusababisha wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine ili kutafuta malisho;

(ii) Kutokuwa na mbegu na mifugo bora;

(iii) Ukosefu wa ithibati katika machinjio na hivyo kuuza nyama nayozalishwa nchini nje ya nchi;

(iv) Biashara ya utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani;

(v) Kukosekana kwa chakula cha samaki;

(vi) Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kuvuna rasilimali zilizopo bahari kuu;

(vii) Kuendelea kuagiza samaki kutoka nje ambapo mwaka 2022 samaki wenye thamani ya shilingi milioni 268 waliagizwa kutoka nje;

(viii) Uvuvi haramu unaopelekea Serikali kukosa mapato stahiki na kuharibu ikolojia ya viumbe hai wanaoishi kwenye maji; na

(ix) Upungufu wa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija katika sekta hizi Kamati inapendekeza masuala yafuatayo yafanyiwe kazi:-

(i) Kuongeza idadi ya Maafisa Ugani na kuwajengea uwezo ili kuongeza utolewaji wa huduma za ugani.

(ii) Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mifugo kama vile Kampuni ya Ranchi za Taifa, Bodi ya Maziwa na Nyama kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi pamoja na kurahisisha utaratibu wa utolewaji wa vibali na usajili.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji; upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka asilimia 70.1 kwa vijijini na asilimia 84 mijini mwaka 2020 hadi asilimia 77 kwa vijijini na asilimia 88 mijini mwaka 2022. Pamoja na juhudi hizi ni vema Serikali ikaongeza usimamizi katika miradi yake inayoitekeleza ili ilete tija inayokusudiwa. Serikali kuharakisha mchakato wa manunuzi wa miradi ili ikamilike kwa wakati pamoja na kudhibiti upotevu na wizi wa maji ambao unasababisha hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Utalii; Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake kubwa katika kuitangaza nchi yetu kupitia Filamu ya *Royal Tour.* Jitihada hizi za Mheshimiwa Rais zimeongeza idadi ya watalii wa nje kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 na kufikia idadi ya watalii 1,454,920 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Vilevile watalii wa ndani walikuwa 2,363,260 ikilinganishwa na watalii wa ndani 788,933 waliotembelea vivutio vya utalii nchini mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 199.55. Aidha, mapato yatokanayo na Utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.31 mwaka 2021 hadi dola za Marekani bilioni 2.53 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 93.

Mheshimiwa Spika, jedwali Na. 2 linaonesha idadi ya watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa za Taifa na mapato halisi kwama 2018 hadi 2022.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya mazingira; moja ya sababu iliyochangia kushuka kwa uchumi wa dunia na Tanzania ni mabadiliko ya tabianchi. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kuiwezesha nchi yetu kutengewa jumla ya dola za Marekani milioni 33.59 kwa kipindi cha miaka minne (2022/2023 - 2025/2026) kwa ajili ya miradi ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kutoka Mfuko wa *Global Environmental Facility*. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini Sekta ya Mazingira inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Matumizi ya nishati zinazoongeza hewa ya ukaa na sio nishati jadidifu.

(ii) Ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza nishati ya kuni na mkaa na shughuli nyingine za binadamu.

(iii) Matumizi ya bidhaa mbalimbali zenye madhara katika mazingira kama plastiki ngumu.

(iv) Shughuli za binadamu ikiwemo kilimo na uvuvi.

(v) Utupaji wa taka hovyo ambazo zina madhara kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya takwimu za matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi; Kamati inaishauri Serikali kuzingatia matumizi ya takwimu za kidemografia zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo. Kamati inaamini kwamba endapo Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo vitafanyika kwa kufuata takwimu za Sensa ya Watu na Makazi hususani kwa kuwaweka watu katika makundi mbalimbali kama vile makundi ya nguvu kazi na makundi tegemezi, Taifa litakuwa na Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo ambayo italeta matokeo chanya katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo ili kuchochea ukuaji wa uchumi kwa mikoa mbalimbali; matokeo ya sensa yanaonesha kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 5,383,728 sawa na asilimia 8.7 ya watu wote Tanzania Bara ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza

uliokuwa na watu 3,699,872 sawa na asilimia 6.0. Vilevile Mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi ndogo ya watu wapatao 889,946 sawa na asilimia 1.4 ya watu wote Tanzania Bara. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara kwa mwaka 2022 ulikuwa wastani wa watu 68 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 65 mwaka 2021. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,865 kwa kila kilometa ya mraba ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na wastani wa watu 391 kwa kila kilometa ya mraba.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba idadi kubwa ya watu na msongamano mkubwa wa watu katika mikoa iliyotajwa inasababishwa na kupatikana kwa huduma za kijamii na miundombinu bora pamoja na fursa za kiuchumi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kutumia sera za kibajeti ili kuchochea maendeleo katika mikoa yote nchini. Hatua hii itapunguza watu kuhama kutoka mikoa mingine na kuelekea katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, utozaji wa kodi ya majengo kwa maendeleo ya nchi; utakumbuka kwamba kwa mujibu wa mabadiliko ya kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha Namba 3 ya mwaka 2021 kila jengo la kawaida lililopo ndani ya kiwanja litalipiwa shilingi 12,000 na shilingi 60,000 kwa kila sakafu ya ghorofa, kwa Halmashauri za Wilaya na miji midogo, nyumba za ghorofa zinatozwa shilingi 60,000. Kwa utaratibu huu mpya kila mnunuzi wa umeme atakatwa shilingi 1,000 kwa mwezi kwa nyumba ya kawaida na shilingi 5,000 kwa kila sakafu ya ghorofa. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kutumia takwimu za majengo zilizopatikana kupitia sensa ili kutoza kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, hoja mahsusi; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(4), (5) na (6) na Kanuni ya 124(1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Bajeti ilipokea jumla ya hoja mahsusi 22 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 na hoja mahsusi tano kwa mujibu wa Kanuni ya 124. Taarifa hii inatoa muhtasari wa mashauriano baina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Uongozi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja zitokanazo na majadiliano ya Kamati kwenye utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2023/2024; hoja zilizopokelewa kutokana na majadiliano Bungeni zilikuwa ni hoja tano. Hoja hizo ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali na utekelezaji wa baadhi ya hoja hizo umeonekena kupitia hatua za kikodi zilizochukuliwa na Serikali kupitia hotuba bajeti kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hivyo Kamati inatitaka Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kabla ya kuanza utaratibu wa kutoa vibali vya kuagiza mafuta nje kujiridhisha na takwimu za uzalishaji ndani ya nchi. Kutokufanya hivyo kunaweza kusababisha taharuki katika upatikanaji wa mafuta ya kula hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya utekelezaji wa mifuko maalumu ilizozingirwa *(ringfenced funds);* Kamati ya Bajeti ilifanya mapitio ya bajeti za mifumo maalum ambayo ni Mifuko ya Barabara ambapo kwenye Mifuko ya Barabara Kamati imebaini kwamba fedha za mfuko hazikidhi mahitaji ya kugharamia matengenezo ya barabara kikamilifu. Uwezo wa mmfuko kwa miaka mitano iliyopita umekuwa chini ya wastani wa asilimia 50 ya mahitaji halisi ya fedha za kugharamia matengenezo. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa urefu wa mtandao wa barabara usioendana na ongezeko la bajeti kwa ajili ya ukarabati. Hivyo kumekuwa na barabara zilizoharibika kwa kiwango kikubwa na kuhitaji matengenezo makubwa. Kutokuzitengeneza barabara hizo kwa wakati kutaathiri biashara ya usafiri na usafirishaji pamoja na matumizi ya bandari zetu. Hivyo Kamati inaishauri Serikali iangalie mkakati mbadala wa ugharamiaji endelevu wa barabara zetu kama vile kutumia hatifungani za miundombinu pamoja na kushirikisha sekta binafsi kwa mfumo wa ubia.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme vijijini; moja ya changamoto iliyokuwa inawakabili Wakala wa Nishati Vijijini ni mikataba isiyoruhusu mabadiliko ya bei na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Kufuatia ushauri wa Kamati, Serikali ilifanya

marejeo ya mikataba 39 kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na gharama zilizotokana na mabadiliko ya mikataba zilifidiwa na fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Programu ya Upanuzi wa Huduma ya Nishati Vijijini na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Reli; katika kipindi cha miaka miwili (2021/2022 hadi Machi, 2023) akaunti ya mfuko ilikuwa na shilingi trilioni 1.04. Aidha, katika kipindi hicho Shirika lilipata idhini ya kutumia shilingi trilioni 1.01. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 388.48 zilitumika katika mwaka 2021/2022 na shilingi bilioni 621.87 zimetumika katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia fedha hizi kujenga reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na kukarabati miundombinu ya reli ya kati ili iendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utendaji kazi na utekelezaji wa bajeti kwa baadhi ya Mashirika, Kampuni, Wakala na Mamlaka za Umma; kifungu cha 9(f) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kukutana na Mashirika ya Umma ili kuangalia mizania yao ya fedha pamoja na kuangalia endapo mashirika hayo yanafuata misingi ya fedha za umma na ya sheria nyingine za nchi. Ili kutekeleza takwa hilo la kisheria Kamati ilifanya tathimini ya utendaji kazi wa Mashirika, Kampuni, Wakala na Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza lilikuwa Shirika la Maendeleo ya Taifa *(TPDC);* Kamati ilibaini kwamba kati ya makampuni 22 yaliyopatiwa idhini na Serikali ya kuwekeza kwenye vituo vya gesi, makampuni 20 yameonesha nia ya kuwekeza kwenye vituo vya kujazia gesi katika Jiji la Dar es Salama na makampuni mawili yalionesha nia ya kuwekeza nje ya Jiji la Dar es Salaam. Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha makampuni kuwekeza nje ya Mkoa wa Dar es Salaam ili kupanua wigo wa matumizi ya gesi asilia kwenye mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja; kwa kuwa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja ndio mfumo rasmi na pekee unaotumiwa na Serikali katika kuagiza bidhaa ya mafuta ya petroli, ni vyema basi mfumo huu

ukatambuliwa kisheria. Kifungu cha 168(1) cha Sheria ya Petroli Sura 392 kimetumia maneno "*efficient procurement*" ambayo hayajatafsiriwa kwenye sheria. Aidha, kifungu cha 168(2) kinampa Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni za mfumo huo kama sheria inavyoelekeza. Kamati inaishauri Serikali ili kuondoa mwanya wa matumizi mabaya ya maneno "*efficient procurement*" kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Petroli ili kutoa tafsiri ya maneno "*efficient procurement*" kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana; kumekuwa na ushiriki hafifu wa wanunuzi wakuu ambao ni mifuko ya hifadhi ya jamii uliotokana na maboresho yaliyofanywa katika sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuunganisha mifuko na kuundwa kwa *Public Sector Social Security Fund - PSSSF*. Ushiriki wa *PSSSF* haujawa mkamilifu kama ilivyokuwa hapo awali na hivyo kupunguza ukwasi kwenye soko la hisa. Takwimu zinaonesha kuwa mifuko hii haijashiriki kununua hisa kwa takribani miezi 39. Kamati inaishauri *PSSSF* kuongeza ushiriki kwenye masoko ya mitaji ili kuchangamsha Soko la hisa nchini. Vilevile Kamati inashauri *PSSSF* kuangalia mikakati yake ya uwekezaji ili kuhakikisha kuwa inafanya uwekezaji ulio na tija.

Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa *(Medical Store Department);* Bohari ya Dawa inakabiliwa na changamoto ya mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 592.9 kwa ajili ya kununua na kuhifadhi dawa kwenye maghala pamoja na ujenzi wa maghala ili vituo vya afya viweze kuhudumiwa pale vinapohitaji dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Mipango kupitia hotuba ya bajeti ya Serikali Kuu ameahidi katika mwaka wa fedha 2023/2024 kuipatia *MSD* mtaji ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuacha kutegemea fedha za hospitali na vituo vya afya katika manunuzi ya dawa na vifaa tiba. Hatua hii ni ya kupongeza, hata hivyo Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha *MSD* inatumia mtaji huo ili kujiendesha kibiashara.

(ii) *MSD* kuingia mikataba na makampuni yanayozalisha dawa ili iweze kununua dawa na vifaa tiba kwa bei nafuu kutoka kwa wazalishaji moja kwa moja badala ya makampuni binafsi yaliyopo nchini ambayo inauzia *MSD* kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kusamehe baadhi ya vifungashio vya dawa na *moulds* kwa ajili ya utengenezaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 44.39 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.02 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ya shilingi trilioni 41.48. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 30.31 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 68.2 ya bajeti yote na shilingi trilioni 14.08 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 31.72 ya bajeti yote. Bajeti ya maendeleo inajumuisha shilingi trilioni 10.80 fedha za ndani na shilingi trilioni 3.28 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mikopo na misaada kutoka nje; Serikali inategemea kukopa jumla ya shilingi trilioni 5.47 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.63 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.65 ya mwaka 2022/2023. Vilevile Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 2.10 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara Ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, fedha hizi zimepungua kwa asilimia 30.69 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.03 zilizotarajiwa kukopwa katika mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, hali hii imechangiwa na Serikali kuchukua tahadhari ya mikopo kutoka nje ambayo kwa hali ilivyo hivi sasa upatikanaji wake umekuwa mgumu. Tahadhari hiyo inatokana na masalia ya athari ugonjwa wa UVIKO–19, vita ya Urusi na Ukraine, kufunguka kwa shughuli za kiuchumi pamoja na Sera za Marekani na Nchi za Ulaya za kupunguza ukwasi katika chumi zao na hatimaye kupunguza mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, hatua za kikodi zinazopendekezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Ushuru wa Fododha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Common External Tarrif)*. Mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 yanaongozwa na *Protocol* ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2005. Aidha, mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2001, unataka Bunge la kila nchi mwanachama kuridhia hatua za ushuru wa forodha za Jumuiya zilizopitishwa na Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kanuni za Bunge hazielekezi utaratibu wa mapendekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za mabadiliko ya ushuru wa forodha kuwasilishwa Bungeni kabla ya kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki, Kamati ya Bajeti imeweka utaratibu ambao unawezesha Wizara ya Fedha kuwasilisha mapendekezo ya ushuru wa forodha kwa Kamati kabla ya kuyapeleka katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashiriki. Kamati inampongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuendelea kudumisha na kuenzi utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hatua zinazopendekezwa kuhusu Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki; Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali na kubaini kwamba hatua mpya zilizopendekezwa ni 19 na hatua nyingine 44 ni muendelezo wa hatua zilizochukuliwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na zimegusa masuala mbalimbli kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu malipo ya Ushuru wa Forodha; Kamati ilikutana na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania ili kupokea maoni yao kuhusu ushuru wa forodha. Baada ya Kamati kuchambua maoni ya wadau hao inashauri maeneo mbalimbali kama inavyooneka kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati:-

Kwanza, tatizo la upatikanaji wa fedha za kigeni; katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni nchini. Sababu za kutopatikana kwa fedha za kigeni zimebainishwa vizuri na Serikali hata hivyo sababu za wapi tunapata fedha za kigeni hazijajadiliwa kwa kina. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba fedha za kigeni nchini kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na Sekta kuu tatu; Sekta ya Kilimo, Sekta ya Utalii na Sekta ya Madini. Aidha, kuna sekta nyingine ambazo zinachangia lakini si kwa kiasi kikubwa kama vile Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza mauala yafuatayo ili kusaidia kuongeza mauzo na huduma za sekta hizo nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni.

Pili, kuanzisha utaratibu wa kutumia wabia yaani *Public Private Partnership* kwenye ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuchochea skimu za umwagiliaji. Hivi sasa mabonde yote ya Umwagilia yaliyopo chini ya Tume ya Umwagiliaji yanategemea bajeti ya Serikali. Hatua hii itasaidia kuwa na kilimo cha uhakika kisichotegemea mvua.

Tatu, kuimarisha miundombinu ya utalii katika Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu pamoja na Malikale ili kuwezesha watalii kufika na kuzuru maeneo hayo.

Nne, kufanya mapitio ya kodi, ada na tozo ambazo ni kikwazo katika kuongeza mauzo nje ya bidhaa na huduma ili kuchochea ukuaji na utolewaji wa huduma zitakazoliingizia Taifa fedha za kigeni.

Tano, kuchochea mauzo ya dhahabu na makaa ya mawe nje ya nchi.

Sita, kudhibiti uagizwaji wa bidhaa zisizo za msingi ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba endapo mapemndekezo hayo yatafanyiwa kazi ni wazi kwamba tatizo la upungufu wa fedha za kigeni zitapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mikopo; Kamati inaipongeza Serikali kwa kupata mikopo mbalimbali na imetekeleza miradi mbalimbali kama ilivyo kwenye Taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni utafiti wa vyanzo mbalimbali vya mapato na Sera za Kikodi zinazopendekezwa na Serikali; moja ya changamoto inayokabili utozaji wa kodi pamoja na usimamizi wake nchini ni kutofanyika utafiti wa kutosha kabla ya kuanzisha sera mpya ya kodi au kuanzisha chanzo kipya. Hatua hii imekuwa ikisababisha mabadiliko ya mara kwa mara ya sheria za kodi au marejeo ya viwango vilivyopendekezwa katika muda mfupi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 Muswada wa Sheria ya Fedha uambatishwe na muhtasari wa matokeo ya utafiti wa hatua mbalimbali zinazopendekezwa tofauti na ilivyo sasa ambapo maelezo yanayoambatishwa ni nia na madhumuni ya Muswada tu. Aidha, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili yakufanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato pamoja na sera za kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uwasilishwaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha kila mwaka Bungeni; Muswada wa Sheria ya Fedha ni muswada unaowasilishwa Bungeni kila mwaka. Hata hivyo, uzoefu wa Kamati unaonesha kwamba muswada huo katika kipindi cha miaka saba haujawahi kusomwa kwa mara ya kwanza na ya pili na kupitishwa ndani ya siku 14 kabla haujapitishwa na Bunge. Hatua hii imekuwa inaleta changamoto ya muda kwa Kamati ya Bajeti kuuchambua, kufanya utafiti na kushirikisha wadau kabla ya kuwasilisha Taarifa ya maoni yake Bungeni. Mataifa ya jirani kama Kenya muswada huo huchukua si chini ya mwezi mmoja. Kwa mfano Muswada wa Fedha wa mwaka 2023 wa Kenya ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la Kenya tarehe 28 Aprili, 2023 na hivi sasa unajadiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaleta uwazi katika jamii na kuondoa mtazamo hasi wa jamii kwamba Bunge lao tukufu linapitisha sheria kandamizi za kodi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba muswada unawasilishwa Bungeni mapema zaidi walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, utungaji wa kanuni zinazoenda kutekeleza sheria mbalimbali za kodi; ni utaratibu wa kawaida kwa Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti mbalimbali ya sheria. Aidha, Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza Kifungu cha 38 kimeweka utaratibu wa kuwasilisha kanuni Bungeni kwa ajili ya kuzipitia na kufanya marekebisho pale inapobidi. Kamati ya Bajeti imebaini kwamba kanuni zimekuwa ni kichocheo cha kuanzisha ada, tozo na faini mbalimbali. Aidha, kuna baadhi ya kanuni hutungwa kinyume na malengo yaliyopo kwenye sheria. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kanuni zote zitakazotungwa zenye lengo la kuanzisha, ada, tozo au faini ziidhinishwe kwanza na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kabla ya kutolewa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kutumika kwa sababu ndiye mwenye mamlaka kwenye masuala yote ya fedha.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa ukusanyaji wa mapato ya kodi kwa pato la Taifa; Taifa letu limekuwa na uwiano wa chini kati ya pato la Taifa na mapato ya kodi. Wastani wa pato la Taifa kwa makusanyo ya kodi kwa mwaka 2022 ilikuwa ni asilimia 12.3 na uwiano wa mapato yote ya ndani kwa Pato la Taifa ni asilimai 14.9. Uwiano huu ni chini ya uwiano kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni asilimia 15. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi na kubaini masuala ambayo yanachangia hali hiyo na ni kama yafuatayo:-

(i) Wingi wa mamlaka za udhibiti ambao unasababisha wafanyabiashara wengi kuogopa kurasimisha biashara zao;

(ii) Kutosomana kwa mifumo ya kukusanyia mapato na baadhi ya mapato ya Serikali kukusanywa nje ya mifumo iliyopo;

(iii) Ukubwa wa sekta isiyo rasmi;

(iv) Biashara za magendo katika mipaka ya nchi kavu na bahari;

(v) Mtazamo hasi wa wananchi kuhusu ulipaji wa kodi hasa katika kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi;

(vi) Ukusanyaji hafifu wa kodi za Serikali, mfano kodi ya majengo na kodi ya ardhi; na

(vii) Elimu duni ya ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini endapo changamoto hizi hazitapatiwa ufumbuzi kwa wakati Tanzania itaendelea kuwa chini ya wastani wa uwiano wa kodi na pato la Taifa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kurejesha asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa na Halmashauri kutokana na kodi ya majengo, kodi ya mabango na kodi ya pango la ardhi; Serikali inakusudia kufanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Majengo na Sheria ya Ardhi ili kurejesha utaratibu wa ukusanyaji wa kodi ya majengo na kodi ya pango la ardhi kwa Serikali za Mitaa. Aidha, uamuzi wa kurejesha asilimia 20 ni wa busara ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa vyanzo hivyo vya mapato. Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kujiendesha wenyewe *(automated)* ili pindi makusanyo yanapokusanywa moja kwa moja asilimia 20 irudi kwenye akaunti za Halmashauri husika. Mfumo ukiachwa kama ulivyo hivi sasa zikaingia Mfuko Mkuu wa Serikali inaweza kuwa vigumu kurejesha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (*Export Credit Guarantee Scheme - ECGS)* na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati; Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Mfuko wa Dhamana kwa wakopaji wanaozalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 600 ambapo Benki Kuu ya Tanzania itatoa shilingi bilioni 280 na Benki ya Dunia itatoa mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 150. Hatua hii ina lengo la kuongeza mauzo nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kabla ya kuanza kutumia fedha hizi kuweka wazi masuala yafuatayo:-

Kwanza, vigezo vya wanufaika, nyaraka zitakazotakiwa kuwasilishwa, sekta zinazolengwa au kupewa kipaumbele, kiwango kitakachokuwa kinatolewa kulingana na uwezo na mchakato wa kupokea maombi na kuchagua washindi.

Kamati inaamini bila kuwa na vigezo na utaratibu kuna uwezekano wa fedha hizo kutotumika kwa matumizi yaliyokusudiwa kama ilivyokuwa mwaka 2007 kuhusiana na fedha za *EPA* ambapo shilingi bilioni 133 kutoka Benki Kuu zilitumika kwa matumizi yasiyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa matumizi ya seti ya mitambo 25 kwa ajili ya kuchimba visima na mabwawa; Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kusambaza seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika mikoa 25 na seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa katika kila kanda. Hata hivyo, kila Halmashauri italazimika kuwa na kiasi cha shilingi milioni 15 ili kuweza kutumia mitambo hii. Hatua hii itaziathiri Halmashauri zenye mapato madogo ambazo zitashindwa kutumia fursa hii ipasavyo ilihali Halmashauri zenye mapato mengi zitanufaika. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu ambao utawezesha Halmashauri zenye mapato madogo kunufaika na mitambo hiyo kwa kutoa ruzuku kwa Halmashuri zisizokuwa na mapato makubwa ili nazo zinufaike na mitambo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza vyema Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Vilevile namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na

Mipango na Serikali nzima kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati wakiongozwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Bi. Lilian Masabala, Ndugu Wilfred Akasi na Bi. Trifina Karaguza pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Fadhat Kamote kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2022, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2023/24, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ikisomwa pamoja na kifungu 9(1)(a) na (b) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2022, Mpango wa

Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/24 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuonyesha kwa vitendo nia yake thabiti ya kuwaondolea watanzania umaskini na kuwaletea maendeleo. Uthubutu wake katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii umekuwa msingi imara katika kutekeleza kauli mbiu yake ya "*KAZI IENDELEE*". Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kumsaidia Mhe Rais katika majukumu yake. Vilevile, inatambua juhudi za Makamu wa Rais katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuendeleza kampeni za upandaji miti nchi nzima.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Waziri Mkuu atakuwa na madaraka ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu kwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili (12) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika umethibitisha kwamba Bunge ni mahali pa kutoa hoja zenye mashiko na ushahidi na si mahali pa upotoshaji wa Umma.

**1.1. Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu kumi na mbili (12) Sehemu ya kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya pili ni Tathmini ya Mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla; Sehemu ya tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/23; Sehemu ya nne ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo

wa Taifa kwa mwaka 2023/24; Sehemu ya tano ni Matumizi ya Takwimu na Matokeo ya Sensa ya watu na Makazi; Sehemu ya sita ni Hoja Mahususi; Sehemu ya saba inahusu Tathmini ya Utekelezaji wa Mifuko Maalum iliyozingirwa – *Ringfenced;*

Sehemu ya nane ni Mapitio Ya Utendaji Kazi Utekelezaji Wa Bajeti Wa Baadhi Ya Mashirika, Kampuni, Wakala Na Mamlaka Za Umma; Sehemu ya tisa inahusu Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24; Sehemu ya kumi inahusu Hatua za kikodi zinazopendekezwa na Serikali; Sehemu ya kumi na moja inahusu Maoni na mapendekezo ya Kamati na mwisho ni Hitimisho.


**2.0. TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA KWA MWAKA 2022**

**2.1. Hali ya Uchumi wa Dunia**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2023 (World Economic Outlook Report, April 2023) inaonyesha kuwa uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa **asilimia 3.4** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 6.3** mwaka 2021. Ukuaji huu ni chini ya makadirio ya kiwango cha ukuaji wa **asilimia 4.4** na ulisababishwa na athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine na mabadiliko ya tabianchi yaliyo sababisha ukame kwa baadhi ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) unaonyesha kwamba katika mwaka 2023 ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea kama vile Marekani pamoja na nchi zinazoibukia kiuchumi ikiwemo China, utaporomoka kutoka **asilimia 2.7** ya mwaka 2022 hadi **asilimia 1.3.** Hii ni kutokana na mataifa haya kusitisha na kufunga maeneo ya uzalishaji na vituo vya biashara. Hali hii itapelekea mdororo wa uchumi katika mataifa machanga yanayoibukia kiuchumi. Hivyo, ni muhimu kwa Serikali kuwa na mikakati thabiti ya kupambana na vihatarishi vinavyotokana na mdororo wa uchumi wa dunia.

**Kielelezo Na 1: Athari za UVIKO-19, Vita ya Urusi na Ukraine, na Mabadiliko ya Tabianchi**




***Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

**2.2. Uchumi wa Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2023 (World Economic Outlook Report, April 2023) uchumi wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa **asilimia 3.9** mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 4.8** mwaka 2021. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi kulichangiwa na kuyumba kwa uchumi wa dunia pamoja na nchi washirika wa kibiashara, hali iliyosababisha uwepo wa masharti magumu ya upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na kudorora kwa urari wa biashara. Matukio haya yamesababisha mfumuko mkubwa wa bei kwa bidhaa mbalimbali ikiwemo mafuta, gesi na vyakula.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hiyo pia inaonyesha kwamba nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara zinazozalisha mafuta zitaendelea kunufaika kutokana na kupanda kwa bei za mafuta na gesi ulimwenguni. Kwa mantiki hiyo, nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo hazizalishi mafuta na gesi uchumi wake unatarajiwa kuyumba kutokana na kupanda kwa bei ya nishati hizo katika soko la dunia. Aidha, uchambuzi wa IMF unaonyesha

kwamba nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zitakumbwa na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa Dola za Kimarekani, kupungua kwa mikopo na misaada nafuu pamoja na kupungua kwa kasi ya uwekezaji katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya na miundombinu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika soko la Kimataifa pamoja na kuboresha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa ili kuendelea kupata fedha na bajeti isiathirike, pamoja na kuweka Sera za kikodi na zisizo za kikodi zinazoweza kuvutia wawekezaji.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia Mwaka 2018 - 2022**

| **Kundi/Mwaka** | **Ukuaji Halisi (Asilimia)** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** |
| Dunia | 3.6 | 2.9 | -3.1 | 6.3 | 3.4 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.3 | 1.7 | -4.5 | 5.4 | 2.7 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 4.6 | 3.7 | -2.0 | 6.9 | 4.0 |
| Nchi za Asia Zinazoendelea | 6.4 | 5.3 | -0.8 | 7.5 | 4.4 |
| Nchi za Afrika Zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.3 | 3.1 | -1.7 | 4.8 | 3.9 |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (World Economic Outlook)*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa za hali ya uchumi wa dunia na uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

i. Kwa kuwa mfumuko wa bei duniani Mwaka 2022 uliongezeka na kufikia wastani wa **asilimia 8.7** ikilinganishwa na **asilimia 4.7** mwaka 2021. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia wastani wa **asilimia 14.5** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 11.0** mwaka 2021. Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya jinsi ya kukabiliana na mfumuko

wa bei unaotokana na uagizaji wa bidhaa nchini (*Imported Inflation*) ili kutokuathiri uchumi wa Taifa

ii. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi kweye Sekta ambazo Tanzania ina nguvu ya ushindani (*Competitive Advantage*) ili kuendelea kukuza Uchumi kwa kiwango kinachotarajiwa. Sekta hizo ni Utalii, Kilimo, Mifugo na Madini.

iii. Kwa kuwa Tanzania imefanikiwa kupata masoko ya mazao ya chakula katika nchi mbalimbali Barani Afrika, na kwa kuwa bei ya mazao ya chakula hususan nafaka katika soko la dunia inatarajiwa kupanda katika mwaka 2023 kutokana na kupungua kwa bidhaa hizo katika soko la dunia. Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya nafaka nchini kwani uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba kati ya **tani milioni 9.49** za nafaka zinazozalishwa nchini ni tani 13,062 tu ndio huongezewa thamani.

iv. Kwa kuwa Soko la Bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange-TMX) limefanya mauzo ya bidhaa mbalimbali katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 ambapo **tani milioni 107.06** za bidhaa mbalimbali zenye thamani ya **shilingi bilioni 223.26** zimeuzwa. Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya mazao na bidhaa zitakazokuwa zinauzwa katika soko hilo pamoja na kuongeza idadi ya wanunuzi wanaoshiriki katika kununua bidhaa mbalimbali katika soko hilo. Vilevile, kutoa elimu kwa wakulima juu ya umuhimu wa kuuza bidhaa zao katika soko hilo pamoja na kuangalia namna ya kuunganisha mfumo wa stakabadhi ghalani katika soko la TMX kwani bidhaa zinazouzwa TMX zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya juu kuliko za stakabadhi ghalani. Hatua hizi zitawaongezea wakulima kipato pamoja na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

v. Kamati inashauri ujenzi wa maghala mapya uendane na ukarabati wa maghala yaliyopo, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza ujenzi wa vyumba vya baridi (Cold Rooms) kwa ajili ya kuhifadhai Samaki, mbogamboga, matunda na maua kwa ajili ya kuuza nje ya nchi pamoja na kuongeza leseni za ujenzi wa maghala ya mazao ya kilimo kwa watu binafsi.

vi. Katika mwaka 2022/23, thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua ilikuwa **dola za Marekani milioni 289.6** ikilinganishwa na **dola za Marekani milioni 378.6** mwaka 2021/22, sawa na upungufu wa **asilimia 23.5**. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kufufua mashamba ya maua, mbogamboga na matunda yaliyopo Wilaya ya Arumeru katika Mkoa wa Arusha. Ufufuaji wa mashamba haya utaliingizia Taifa mapato ya kigeni pamoja na kurejesha ajira zaidi ya 2000 zilizopotea.

**2.3. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2022, Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 4.7** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 4.9** mwaka 2021. Katika mwaka 2022, thamani halisi ya Pato la Taifa ilifikia **shilingi trilioni 141.873** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 135.478** mwaka 2021**.** Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika kipindi husika kumechangiwa na athari za UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Changamoto hizi zimepelekea kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa katika soko la dunia, kuathirika kwa mnyororo wa ugavi (supply chain disruptions) pamoja na kupanda kwa gharama za bidhaa za msingi kama vile mafuta na ngano.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Benki kuu ya Tanzania inaonyesha kwamba katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/23 uchumi wa Tanzania ulikua kwa wastani wa **asilimia 5.2** ikilinganishwa na **asilimia 4.9** katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Ukuaji huu wa uchumi unaashiria kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa ajira na mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa shughuli za kiuchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa na kubaini kwamba Sekta ya Kilimo pamoja na kuwa imechangia **asilimia 26.2** katika Pato la Taifa, ukuaji wa Sekta hii sio wa kuridhisha kwani Sekta hii imekua kwa **asilimia 3** ukilinganisha na ukuaji uliotarajiwa wa **asilimia 5**. Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba Sekta ya Kilimo inajikita zaidi katika uzalishaji wa mazao ya chakula yanayohitajika nchini pamoja na mazao ya biashara yanayohitajika katika soko la


dunia. Hatua hii itaongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi pamoja na kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Aidha, Kamati inampongeza Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ongezeko la bajeti ya Sekta ya Kilimo hadi kufikia **Shilingi bilioni 970.8** katika mwaka wa fedha 2023/24. Kamati inaamini kwamba ongezeko hili linaenda kufanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Kilimo.

**2.4. Mfumuko wa Bei**

**Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo katika mwaka 2022 mfumuko wa bei ulifikia wastani wa **asilimia 4.3**, ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.7** mwaka 2021. Mwenendo huu uko ndani ya lengo la muda wa kati la **asilimia 5.0** na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kiwango ambacho hakizidi **asilimia 8.0** na wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya **asilimia 3.0** hadi **7.0**. Ongezeko hili la mfumuko wa bei lilitokana na vita kati ya Urusi na Ukraine pamoja na athari za ugonjwa wa UVIKO -19 hali iliyosababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa za walaji katika soko la dunia. Hali hii itasababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia mfano, Mafuta ya petroli, ngano na mafuta ya kula.

**Mheshimiwa Spika,** kupanda kwa bei za baadhi ya bidhaa na huduma muhimu ikiwemo chakula na nishati kulisababisha athari za mfumuko wa bei kwa matabaka ya kipato cha chini, kati na juu kuongezeka hadi **asilimia 4.7, asilimia 5.8** na **asilimia 3.8** mtawalia mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 2.4, asilimia 2.4** na **asilimia 3.0,** mtawalia mwaka 2021. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuchochea uzalishaji wa ngano pamoja na mafuta ya kula nchini katika kukabiliana na mfumuko wa bei.

**Kielelezo Namba .2. Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Aprili, 2022 hadi Aprili, 2023 (2020 = 100)**




**Chanzo:** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu 2023*

**2.5. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji fedha**

**Mheshimiwa Spika**, Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni imeendelea kuwa tulivu. Katika mwaka, 2022, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,314.5** ikilinganishwa na **shilingi 2,309.2** katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na kushuka kwa **asilimia 0.2** kwa shilingi. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo katika uzalishaji wa bidhaa na huduma zinazoweza kuuzika katika masoko ya kimataifa hususan bidhaa za kilimo, gesi na dhahabu pamoja na kuchochea shughuli za utalii nchini.


**2.6. Akiba ya Fedha za Kigeni**

**Mheshimiwa Spika**, akiba ya fedha za kigeni ilipungua kufikia **Dola za Marekani milioni 5,177.2** mwezi Disemba 2022 sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa **miezi 4.7** kutoka **Dola za Marekani milioni 6,386.0** mwezi Disemba 2021 sawa na **miezi 6.6** ya uagizaji. Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni nchini kumesababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo mfumuko wa bei katika soko la dunia, kulipa madeni ya nje pamoja na kugharamia miradi ya maendeleo ya kimkakati. Hali hii

imesababisha nakisi ya **dola za Marekani milioni 4,414.2** za urari wa malipo yote ya nje katika kipindi cha Julai, 2022 ikilinganishwa na nakisi ya **Dola za Marekani milioni 2,516.1** kwa kipindi kama hicho mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na tatizo la uhaba wa Dola za Marekani linaloikumba dunia kwa sasa, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuanzisha mchakato wa kununua na kutunza dhahabu kama akiba ya fedha za kigeni. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupata fedha za kigeni kutoka kwa mabenki ya ndani na nje kwa njia ya *currency swap*, kudhibiti soko la fedha za kigeni lisilo rasmi (parallel foreign exchange market) pamoja na kuweka mikakati ya maboresho kwenye soko la fedha za kigeni. Lengo la hatua hizo ni kuwianisha thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni (exchange rate) kwenye soko la jumla la fedha za kigeni kuwa sawia na ile iliyopo kwenye soko la rejareja.

**Kielelezo Na 3. Mwenendo wa Akiba ya Fedha za Kigeni**




***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

## 2.7. Biashara ya Nje

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi kufikia mwezi Januari, 2023 urari wa malipo kwa Sekta ya nje ulikuwa na nakisi ya **Dola za Marekani milioni 5,261.3** ikilinganishwa na nakisi ya **Dola za Marekani Milioni 2,659.3** katika


kipindi kama hicho kwa mwaka 2022. Aidha, thamani ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje mwaka 2022 ilikuwa **Dola za Marekani milioni 654.9** ikilinganishwa na **Dola za Marekani milioni 813.5** mwaka 2021, sawa na upungufu wa **asilimia 19.5**. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kujielekeza zaidi katika kuchochea uzalishaji wa mazao yanayoongoza kuuzwa katika soko la nje kama vile Korosho ambayo mauzo yake yameongezeka kutoka **Dola za Marekani milioni 159** mwaka 2021 hadi **milioni 226.9** mwaka 2022, Katani kutoka **Dola za Marekani milioni 127.5** mwaka 2021 hadi **Dola za Marekani milioni 178.5** pamoja na Pamba kutoka **Dola za Marekani milioni 81.3** mwaka 2021 hadi **Dola za Marekani milioni 103.4** mwaka 2022 ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kupunguza nakisi ya urari wa malipo ya jumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa bidhaa zisizo za asili Kamati inaishauri Serikali ijielekeze kwenye mauzo ya bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) ambazo mauzo yake yaliongezeka kutoka dola za Marekani **milioni 90.2** mwaka 2021 hadi **Dola za Marekani milioni 131.2** mwaka 2022 pamoja na bidhaa za Viwanda ambazo mauzo yake yaliongezeka kutoka **Dola za Marekani bilioni 1.20** mwaka 2021 hadi **Dola za Marekani bilioni 1.42** mwaka 2022. Hatua hizi zote kwa ujumla zitasaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza nakisi.

**2.8. Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi mwezi Aprili 2023, deni la Serikali lilikuwa ni **Shilingi trilioni 79.1** ukilinganisha na Deni, la **Shilingi trilioni 69.26** katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la **asilimia 13.9** (**Shilingi trilioni 9.84).** Ongezeko la deni limetokana na sababu mbalimbali zikiwemo : Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, kutolewa kwa hatifungani maalumu yenye thamani ya **shilingi trilioni 2.18** kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999 na malimbikizo ya riba ya deni la nje.

**Kielelezo Na.4: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2014 - Machi 2023 (Shilingi Bilioni)**




| | Machi-2014 | Machi-2016 | Machi-2017 | Machi-2018 | Machi-2019 | Machi-2020 | Machi-2021 | Machi-2022 | Machi-2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Ndani | 6,464. | 10,002 | 12,073 | 14,158 | 13,133 | 14,730 | 16,116 | 21,778 | 26,851 |
| Deni la Nje | 18,236 | 28,068 | 30,809 | 35,729 | 37,639 | 40,245 | 43,736 | 47,483 | 50,158 |
| Deni la Serikali | 29,537 | 38,071 | 42,883 | 49,728 | 50,772 | 54,976 | 59,852 | 69,261 | 77,010 |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba deni letu ni himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali masuala yafuatayo:

i. Serikali iendelee kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni. Hii ni kwa sababu deni la Taifa hulipwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima (*first charge*) katika matumizi ya Serikali;

ii. Kwa kuwa Serikali ilitoa hatifungani maalumu yenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.18** kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio ya viwango vya Pensheni ya Wastaafu kabla ya Miaka ya 90 ili viendane na hali halisi ya sasa;

iii. Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati (Semi concessional loans) ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara;

iv. Mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwe katika miradi ambayo itakamilika na kuanza kuzalisha mapato katika kipindi cha muda mfupi; na

v. Kuboresha mikakati ya kukusanya mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.


**2.9. Mwenendo wa Viwango vya Riba na Huduma za Kibenki**

**Mheshimiwa Spika,** viwango vya riba za mikopo ya mabenki vilipungua kwa kasi ndogo, hadi kufikia **asilimia 15.91** katika kipindi cha mwezi Aprili 2023 kutoka wastani wa **asilimia 16.31** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii imetokana na jitihada za Serikali kupitia Benki kuu kuongeza ukwasi kwenye mabenki ili kushusha viwango vya riba. Aidha, kwa upande wa riba za amana zilipungua hadi **asilimia 6.79** mwaka 2023 kutoka **asilimia 6.81** mwaka 2022. Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuongeza ukwasi katika mabenki ili kushusha viwango vya riba za mikopo. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutumia nyenzo mbalimbali za Sera ya fedha ili riba za mikopo ziwiane na kiwango cha mfumuko wa bei wa **asilimia 4.3**. Aidha, kuwe na utaratibu maalum utakaowezesha watumishi wa umma kupata mikopo yenye riba nafuu.

**2.10. Tathmini ya Hali ya Umaskini Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** viashiria vya kupima hali ya umaskini nchini hupatikana kwa kutumia Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey - HBS), utafiti huo hufanyika kila baada ya miaka mitano. Matokeo ya Utafiti huo ya mwaka 2017/18 yanaonyesha kuwa kaya zenye wanakaya wachache wana kiwango kidogo cha umaskini kuliko kaya zenye wanakaya wengi. Aidha, kiwango cha umaskini wa mahitaji ya chakula na ya msingi ni kikubwa kwa kaya zinazoongozwa na wakuu wa kaya wenye elimu ndogo. Kamati inatambua kuwa maendeleo ni pamoja na kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula. Hivyo, Serikali iendelee kusimamia vema Sera yake ya Elimu bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia. Vilevile, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Serikali iwekeze zaidi katika sekta ambazo zinahusisha wananchi wengi kama vile kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwakwamua kutoka kwenye umaskini.

**Kielelezo Na. 5: Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya, HBS 2017/18**




***Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

## 3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23 ni ya pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26, ambapo Serikali ilipanga kukusanya na kutumia **Shilingi trilioni 41.48** kutoka vyanzo vya nje na ndani**.** Kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa **shilingi trilioni 27.01**, misaada na mikopo ya masharti nafuu yalikuwa **shilingi trilioni 4.65**, mikopo ya ndani ilikuwa **Shilingi trilioni 5.78** na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara **Shilingi trilioni 3.03**. Hadi kufika Aprili, 2023 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi trilioni 32.43** kutoka vyanzo vyote ikiwa ni sawa na **asilimia 78.18** ya bajeti nzima. Uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato katika kila chanzo ni kama inavyoonekana hapo chini.

### 3.1.1. Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** hadi Aprili, 2023 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi trilioni 18.81** sawa na **asilimia 79.53** dhidi ya lengo la mwaka mzima la kukusanya **Shilingi trilioni 23.06.** Ufanisi huu umetokana na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali katika kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari, matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ulipaji kodi, usimamizi wa

ukusanyaji wa kodi pamoja na kushughulikia mashauri ya kodi ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa na ukusanyaji wa ufanisi kwa kipindi cha miaka 3 mfululizo ambapo mapato yameongezeka kutoka **Shilingi trilioni 17.62** mwaka 2019/20 hadi kufikia **Shilingi trilioni 20.93** mwaka 2021/22**.** Kamati inaipongeza Serikali, hata hivyo Mamlaka hii bado inahitaji kuwezeshwa kwa kupatiwa rasilimali watu pamoja na rasilimali fedha ili iweze kuhuisha mifumo na kukusanya mapato kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kufanya marejesho ya kodi (Tax Refunds) kwa wafanyabiashara jambo ambalo limekuwa ni kilio cha muda mrefu. Ulipaji wa marejesho umeongezeka kutoka **shilingi bilioni 246.5** mwaka wa fedha 2019/20 hadi kufikia **shilingi bilioni 836.98** mwezi Machi, 2023**.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2023 Mapato yasiyo ya Kodi yalifikia **shilingi trilioni 2.07**, sawa na **asilimia 61.79** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 3.35** kwa mwaka. Kwa mwenendo huu ni wazi kuwa lengo la kukusanya kiasi kilichotarajiwa halitofikiwa. Kamati ilibaini kuwa kutokufikiwa kwa lengo kumesababishwa na baadhi ya Wizara na Idara za Serikali kutotumia mifumo ya kielektroniki kukusanyia mapato. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Umma zinatumia mifumo iliyowekwa ili kupunguza tatizo la upotevu wa mapato.

**3.1.2. Mapato ya Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2023 Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia **shilingi bilioni 788.8** sawa na **asilimia 78.12** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 1.01**. Aidha, Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Halmashauri zenye uwezo mkubwa wa kukusanya mapato lakini huwekewa ukomo na Wizara ya Fedha na Mipango ulio chini ya uwezo wa Halmashauri husika kukusanya. Vilevile, Kamati imebaini bado kuna changamoto ya ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo. Hivyo, Kamati inaamini mfumo wa TAUSI ambao unasaidia kutambua vyanzo vya mapato vya Halmashauri husika

na hivyo kusaidia kukadiria uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato yake.

### 3.1.3. Misaada na Mikopo ya Masharti Nafuu kutoka Nje

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilitarajia kupata **shilingi trilioni 4.65** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Serikali ilikuwa imepokea **shilingi trilioni 4.61** sawa na **asilimia 99.14**. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 1.50** ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti; **shilingi bilioni 85.4** ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta; na **shilingi trilioni 2.22** ni misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo. Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano na Washirika wa Maendeleo (Development Cooperation Framework-DCF) pamoja na kuimarisha ushirikiano na uhusiano wa kimataifa. Ni kutokana na jitahada zake ndio maana tumeweza kufikia ufanisi wa **asilimia 99.14.**

### 3.1.4. Mikopo ya ndani

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilikusudia kukopa katika soko la ndani **shilingi trilioni 5.78.** Hadi kufikia mwezi Aprili 2023 mikopo ya ndani ilifikia **shilingi trilioni 4.68** sawa na **asilimia 81.97** ya lengo la mwaka. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba ukopaji wake katika soko la ndani hauathiri upatikanaji wa mikopo kwa Sekta binafsi. Aidha, Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma ili washiriki katika kununua dhamana za Serikali kwani katika katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na muitikio mdogo.

### 3.1.5. Mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilikusudia kukopa **Shilingi trilioni 3.03** kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Serikali ilifanikiwa kukopa **Shilingi trilioni 1.47** sawa na **asilimia 48.51** ya lengo la mwaka. Sababu za kutofikiwa kwa lengo kulitokana na vita ya Urusi na Ukraine iliyosababisha kuongezeka kwa gharama za mikopo mipya na hivyo kuathiri upatikanaji wake. Mwenendo huu umeathiri mipango ya Serikali kutokana na kutopatikana kwa fedha hizo. Vilevile, hali hii itaendelea kuwepo kutokana na

sababu nyingine ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kigeni unaochangiwa na Sera ya Marekani ya kukabiliana na mfumuko wa bei. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kukabiliana na adha ya upatikanaji wa mikopo ya nje. Pia Serikali ihakikishe kuwa mikopo yote inayopatikana inasimamiwa vyema na kutekeleza shughuli iliyokusudiwa na si vinginevyo.

**3.2. Mwenendo wa Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23 Serikali ilikusudia kutumia **Shilingi trilioni 41.48,** kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni **Shilingi trilioni 26.47** na **Shilingi trilioni 15.01** ni matumizi ya maendeleo ikiwa ni **asilimia 36.02** ya bajeti nzima. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya **Shilingi trilioni 32.43** sawa na **asilimia 78.18** ya lengo la mwaka. Fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa **Shilingi trilioni 20.94** sawa na **asilimia 79.1** na **Shilingi trilioni 11.49** ni matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 76.55**. Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji huu wa bajeti, ni wazi kwamba hadi kufika tarehe 30 Juni, 2023 bajeti ya Serikali itakuwa imetekelezwa kwa zaidi ya **asilimia 90**.

**4.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2022/23 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ulitengewa jumla ya **shilingi trilioni 15.01**, sawa na **asilimia 36.18** ya Bajeti ya Serikali ambapo **shilingi trilioni 12.31**, sawa na **asilimia 82.0** ni fedha za ndani na **shilingi trilioni 2.7**, sawa na **asilimia 18** ni fedha za nje. Mpango huu ni wa pili katika Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya "***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***".

**4.1. Tathmini ya Utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi trilioni 11.49** ambayo ni sawa na **asilimia 76.5** ya Bajeti iliyokuwa imetengwa ya **Shilingi trilioni 15.01** kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kamati inampongeza Mhe. Dkt Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nia yake ya dhati ya kuliletea Taifa maendeleo. Muhtasari wa utekelezaji wa miradi katika Sekta mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

**4.1.1. Sekta ya Afya**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Afya na kuongeza bajeti yake kutoka **shilingi trilioni 1.11** mwaka 2022/23 hadi **shilingi trilioni 1.24** mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **asilimia 11.**
Mafanikio mengine ya Serikali katika Sekta hii ni pamoja na**:-**

i. Kutoa ajira mpya ili kupunguza changamoto ya Watumishi katika Sekta hii, ambapo jumla ya ajira mpya **8,992** zimetolewa katika kipindi cha Julai hadi Aprili 2023;

ii. Kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya afya kwa kujenga Hospitali tano (5) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu;

iii. Kununua na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vya afya 150, zahanati 300, na hospitali za Halmashauri vyote pamoja na kuipatia mtaji MSD ili ifanye kazi kama bohari ya dawa na sio kitengo cha manunuzi ya dawa serikalini;

iv. Kulipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuuwezesha kutoa huduma za afya nchini;

v. Kujenga hospitali mpya na kukarabati hospitali kongwe 19 za Halmashauri, ukamilishaji wa zahanati 300 katika Halmashauri 184; na vi. Kutoa jumla ya **shilingi bilioni 463** sekta ya afya ili kukabiliana na athari za kiuchumi na Kijamii zinazotokana na UVIKO -19.

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji huo umebadili kabisa taswira ya sekta ya afya kwenye teknolojia na miundombinu ambapo rufaa za wagonjwa kwenda nje ya nchi zimepungua kwa **asilimia 97**. Hakika hizi ni jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada hizi bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa vifaa

tiba kwenye hospitali mpya, upungufu wa Watumishi **106,445** kati ya watumishi **216,061** wanaohitajika, sawa na **asilimia 50.4**, ucheleweshaji wa manunuzi ya dawa kutokana na utaratibu wa manunuzi ya dawa kuwa sawa na ununuzi wa bidhaa nyingine za Serikali, baadhi ya maeneo kutokuwa na vituo vya afya na zahanati. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiwezesha Sekta hii kifedha na rasilimali watu ili iweze kutatua changamoto zinazoikabili.

**4.1.2. Sekta ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sekta ya Elimu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikisha masuala yafuatayo:-

i. Kutoa ajira **21,000** za Walimu ili kuondoa changamoto ya uhaba wa walimu wa shule za msingi na sekondari;

ii. Kutoa mkopo kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kuchaguliwa kujiunga na vyuo vya Ufundi vya DIT, MUST na Arusha Technical College (ATC);

iii. Kurekebisha kifungu cha 15 cha Sheria ya kuendeleza Ufundi Stadi Sura 82 kwa kupeleka theluji moja ya mapato VETA; na

iv. Kuondoa ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa mikopo ya vyuo vya kati (VETA) ili kuondoa malamiko yaliyojitokeza katika utoaji wa mikopo ya vyuo vikuu.

**4.1.3. Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

**4.1.3.1. Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo ni moja ya Sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi ambapo inakadiriwa kuwa kati ya **asilimia 60** hadi **70** ya Watanzania wamejiajiri katika Sekta hii. Aidha, mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa kwa mwaka 2022 ulikuwa **asilimia 26.2.** Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika sekta hii. Hata hivyo, sekta hii bado ina kabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Matumizi ya mbegu zisizo na ubora na ambazo hazijafanyiwa majaribio na hivyo kusababisha tija ndogo pamoja na hasara kwa wakulima;

ii. Mchakato wa manunuzi wa mbolea kuchukua muda mrefu, na hivyo kusababisha mbolea kupatikana muda ambao msimu wa kilimo umeshaanza. Hali hii inasababisha kuwa na mavuno duni kutokana na kukosekana kwa mbolea za kupandia na kukuzia kwa wakati;

iii. Ardhi ya kilimo kuendelea kupungua kutokana na kuvamiwa kwa ajili ya makazi;

iv. Uchimbaji wa mabwawa kufanywa na Sekta zaidi ya moja ambazo ni Sekta ya Mifugo, Uvuvi, Kilimo na Maji na hivyo kusababisha mtawanyo wa fedha usio na tija;

v. Upotevu wa mazao baada ya kuvunwa (*post harvest loss*) kutokana na miundombinu ya kuhifadhia mazao; vi. Ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo na biashara; na

vi. Mabadiliko ya tabianchi yanayopelekea ukame na hivyo kusababisha uhaba wa chakula.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali:-

i. Kuendelea kuwekeza kwenye vyanzo vya uhakika vya umwagiliaji ambavyo vitatatua changamoto ya kilimo cha kutegema mvua;

ii. Kuendelea kutenga fedha za kutosha kwenye Taasisi zinazofanya utafiti kama TARI na ASA ili kupata mbegu bora;

iii. Kuhuisha miradi inayofanana inayotekelezwa na Wizara zaidi ya moja mfano uchimbaji wa mabwawa na visima na usambazaji wa maji; na

iv. Kuangalia upya utaratibu wa uagizaji wa mbolea ili mbolea ipatikae kwa wakati kuendana na msimu wa kilimo.

#### 4.1.3.2. Sekta ya Mifugo na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2022 imechangia **asilimia 7** ya Pato la Taifa. Mchango mkubwa unatokana na uzalishaji wa nyama ya ng"ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Katika mwaka 2022 idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia **milioni 173.9** ikilinganishwa na mifugo **milioni 165.9** mwaka 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 4.8.** Uzalishaji wa nyama kwa mwaka 2022 ulikuwa **tani 769,966** ikilinganishwa na **tani 738,166** mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi katika mwaka 2022 imechangia **asilimia 1.8** ya Pato la Taifa. Katika Mwaka 2022 **tani 471,512** za samaki zenye thamani ya **shilingi trilioni 3.16** zilivunwa ikilinganishwa na **tani 477,018** zenye thamani ya **shilingi trilioni 2.78** mwaka 2021. Changamoto zilizopo katika Sekta hizi ni pamoja na:-

i. Kukosekana kwa malisho ya mifugo na hivyo kusababisha wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine ili kutafuta malisho;

ii. Kutokuwa na mbegu na mifugo bora;

iii. Ukosefu wa ithibati katika machinjio na hivyo kuuza nyama inayozalishwa nchini nje ya nchi ;

iv. Biashara ya utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani;

v. Kukosekana kwa chakula cha samaki;

vi. Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kuvuna rasilimali zilizopo bahari kuu;

vii. Kuendelea kuagiza samaki kutoka nje ambapo mwaka 2022 samaki wenye thamani ya **shilingi milioni 268** waliagizwa kutoka nje;

viii. Uvuvi haramu unaopelekea Serikali kukosa mapato stahiki na kuharibu ikolojia ya viumbe hai wanaoishi kwenye majini; na

ix. Upungufu wa Maafisa ugani.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza tija katika Sekta hizi Kamati inapendekeza masuala yafuatayo yafanyiwe kazi:-

(iii) Kuongeza idadi ya Maafisa Ugani na kuwajengea uwezo ili kuongeza utolewaji wa huduma za ugani;

(iv) Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mifugo kama vile Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Bodi ya maziwa na Bodi ya nyama. Kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi pamoja na kurahisisha utaratibu wa utolewaji wa vibali na usajili;

(v) Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi iendelee na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ili kupunguza migogoro;

(vi) Kutenga bajeti ya kutosha kwa vituo vya Taifa na kikanda vya uhimilishaji wa mifugo, ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mitamba;

(vii) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya samaki na nyama ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara; na

(viii) Serikali iweke mkakati wa kudhibiti uharibifu wa mazalia ya samaki pamoja na uvuvi haramu.

**Mheshimiwa Spika,** endapo Serikali itafanyia kazi ushauri wa Kamati ni wazi kwamba Sekta hizi zitakuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa pamoja na kupata manufaa yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu.

**4.1.3.3. Sekta ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa katika usambazaji wa maji mijini na vijijini. Kwa mwaka 2022/23, Sekta hii ilitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 709.4**. Fedha hizo zimefanikisha kukamilika kwa miradi 80 ya usambazaji maji mijini na miradi 1,373 vijijini. Hatua hii imewezesha upatikanaji wa maji kuongezeka kutoka **asilimia 70.1** kwa vijijini na **asilimia 84**

mijini mwaka 2020 hadi **asilimia 77.0** kwa vijijini na **asilimia 88** mijini mwaka 2022. Pamoja na juhudi hizi ni vyema Serikali ikaongeza usimamizi katika miradi yake inayoitekeleza ili ilete tija inayokusudiwa. Serikali kuharakisha mchakato wa manunuzi wa miradi ili ikamilike kwa wakati pamoja na kudhibiti upotevu na wizi wa maji ambao unasababisha hasara kwa Serikali.

**4.1.4. Sekta ya Miundombinu ya Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ikiwemo barabara za kufungua fursa za kiuchumi na kuunganisha Tanzania na nchi jirani, madaraja na vivuko. Hadi Aprili 2023, jumla ya **kilometa 1,151.37** zimejengwa kwa kiwango cha lami na **kilometa 1,483.74** zinaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami na **kilometa 1,124.3** za barabara za Mikoa zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 350** kwa kiwango cha lami, kukarabati **kilometa 25** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa **madaraja 13,** kufanya maandalizi mbalimbali ya ujenzi wa **madaraja 11** na kufanya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **daraja 1** katika barabara kuu na baadhi ya barabara za Mikoa. Kati ya **kilometa 350** zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami **kilometa 282** ni za Miradi inayoendelea na **kilometa 68** ni za Miradi mipya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi juu ya ujenzi wa barabara nchini na kubaini masuala yafuatayo:-

i. Ujenzi wa baadhi ya barabara chini ya kiwango, na hivyo kusababisha barabara hizo kutodumu kwa muda mrefu;

ii. Kuchelewa kufanya ukarabati na marekebisho na hivyo kusababisha kugharimu fedha nyingi zaidi ukilinganisha na endapo marekebisho hayo yangefanyika kwa wakati;

iii. Uchelewaji wa mchakato wa manunuzi unaosababisha miradi kuchukua muda mrefu na kuongeza gharama za utekelezaji wake; na

iv. Kutokulipa kwa wakati hati za madai za wakandarasi na hivyo kusababisha malimbikizo ya riba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatatua changamoto hizi ikiwemo kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya marekebisho ya barabara ili kuhakikisha kunakuwa na barabara zenye ubora na ambazo zitadumu kwa muda mrefu. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutumia mfumo wa ujenzi wa EPC + F ili kuendeleza kasi ya ujenzi wa barabara.

**4.1.5. Sekta ya Viwanda na Biashara**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2023/24 Sekta hii imetengewa jumla ya **shilingi bilioni 117.82**, hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 18.9** kutoka **shilingi bilioni 99.11** zilizotengwa mwaka 2022/23. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Sekta hii ni pamoja na idadi ya watu walioajiriwa kwenye Sekta ya Viwanda imeongezeka kutoka **345,615** mwaka 2021 hadi **354,477** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 2.56.** Kutoa fedha kwa ajili ya ulipaji wa fidia katika mradi wa Liganga na Mchuchuma ili taratibu za kuendeleza mradi huo zifuate pamoja na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji nchini – *BluePrint* kwa kufuta na kupunguza tozo na ada 39 mwaka 2022 ikilinganishwa na tozo na ada 14 zilizofutwa ama kupunguzwa mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kutotabirika kwa Sera za Kodi na hivyo kutovutia uwekezaji;

ii. Uwepo wa biashara za magendo katika mipaka na hivyo kuleta ushindani usio sawa kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani;

iii. Uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni zilizopitwa na wakati;

iv. Wingi wa Mamlaka za udhibiti; na

v. Ugumu katika ulipaji wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji nchini - *BluePrint*. Lengo ni kutanua wigo wa ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini na kuchochea Dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na Ushindani. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) ambalo jukumu lake la msingi ni kuendeleza ukuaji wa viwanda nchini kwa kufanya uwekezaji kwenye maeneo ya kimkakati yenye kuchochea uchumi na maendeleo ya viwanda nchini. Kwa sasa Shirika linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti ukilinganisha na mahitaji ya Shirika hilo.

### 4.1.6. Sekta ya Utalii

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake kubwa katika kuitangaza nchi yetu kupitia Filamu ya Royal Tour. Jitihada hizi za Mhe. Rais zimeongeza idadi ya watalii wa nje kutoka watalii **922,692** mwaka 2021 na kufikia idadi ya Watalii **1,454,920** mwaka 2022, sawa na ongezeko la **asilimia 57.7.** Vilevile, watalii wa ndani walikuwa **2,363,260** ikilinganishwa na watalii wa ndani **788,933** waliotembelea vivutio vya utalii nchini mwaka 2021, sawa na ongezeko la **asilimia 199.55**. Aidha, mapato yatokanayo na Utalii yameongezeka kutoka **Dola za Marekani bilioni 1.31** mwaka 2021 hadi **Dola za Marekani bilioni 2.53 m**waka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 93.**

**Jedwali Na.2 Idadi ya Watalii Waliotembelea Katika Hifadhi za Taifa na Mapato ya Utalii Mwaka 2018 - 2022**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | Jumla | Mapato (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | | |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486.8 |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539.5 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614.7 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028.6 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079.5 |

***Chanzo: Wizara ya Maliasiri na Utalii***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Sekta ya Utalii inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

i. Upungufu wa bajeti kwa Mamlaka mbalimbali zinazosimamia maeneo ya Utalii mfano TANAPA imeongezewa hifadhi sita na TAWA imeongezewa idadi ya mapori hata hivyo bajeti za Mamlaka hizo haziendani na ongezeko la majukumu;

ii. Upungufu wa malazi ya watalii ukilinganisha na mahitaji;

iii. Migogoro ya ardhi kati ya wananchi na maeneo ya Hifadhi;

iv. Kuongezeka kwa maafa yanayotokana na muingiliano baina ya wananchi na wanyamapori;

v. Miundombinu duni ya usafiri na usafirishaji wa Watalii kwenye maeneo ya hifadhi; na

vi. Fidia ndogo zinazolipwa kwa wananchi wanapodhurika na wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Ukanda wa Afrika Mashariki nchi yetu inaongoza kwa kuwa na vivutio vingi, hata hivyo idadi ya Watalii wanaotembelea Taifa letu ni wachache ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya na Rwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kikodi ilizochukua katika mwaka wa fedha 2023/24 ili kutanzua changamoto zinazoikabili Sekta hii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi ili kuvutia wawekezaji, kufanya mapitio ya viwango vya kodi, ada na tozo ili kuhakikisha kwamba haviwi vikwazo katika ukuaji wa Sekta ya Utalii, kuongeza bajeti kwa ajili ya kutangaza vivutio vya Utalii na kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege ( air strips) ili kuchochea ukuaji wa Sekta. Aidha, Serikali ishirikiane na Sekta Binafsi katika ujenzi wa Hoteli za nyota mbalimbali ili kutatua upungufu wa vitanda.

**4.1.7. Sekta ya Ardhi na Mazingira**

**4.1.7.1. Sekta ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ardhi ni Sekta ya msingi katika maendeleo ya Sekta zote za uchumi. Kamati inaipongeza Serikali

inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023 ili kuwapunguzia wananchi gharama, pamoja na kushusha kodi ya ongezeko la mtaji kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 3.**

**Mheshimiwa Spika**, mbali na jitihada zilizofashwa na Serikali bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Kasi ndogo ya upangaji wa matumizi ya ardhi. Hadi mwaka 2022 ni takribani **asilimia 25** tu ya ardhi ya Tanzania ndio imepimwa na kupangiwa matumizi;

ii. Ukusanyaji wa kodi ya pango ya ardhi usioridhisha;

iii. Migogoro ya wananchi juu ya uporwaji wa ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa ni kwa sababu ya upimaji na upangaji hafifu; na

iv. Kasi ndogo ya upimaji wa ardhi ya vijiji ambapo hadi mwaka 2022 vijiji vilivyopimwa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ni **2,673** kati ya vijiji **12,345** vilivyopo nchini sawa na **asilimia 21.6**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi ya vijiji. Kwa kuwa Ardhi ni maliasili isiyoongezeka, ni muhimu kuwa na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunapanga matumizi bora ya ardhi kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Kwa upande wa kodi ya pango ya ardhi, kamati inaishauri Serikali kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa kodi ili kukusanya kodi hiyo kwa urahisi.

**4.1.7.2. Sekta ya Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya sababu iliyochangia kushuka kwa uchumi wa Dunia Tanzania ni mabadiliko ya tabianchi. Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Nchi yetu kutengewa jumla ya **Dola za Marekani milioni 33.59** kwa kipindi cha miaka

minne (2022/23 - 2025/26) kwa ajili ya miradi ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kutoka Mfuko wa *Global Environmental Facility*. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini Sekta ya Mazingira inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Matumizi ya nishati zinazoongeza hewa ya ukaa na sio nishati jadidifu;

(ii) Ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza nishati ya kuni na mkaa na shughuli nyingine za binadamu;

(iii) Matumizi ya bidhaa mbalimbali zenye madhara katika mazingira kama plastiki ngumu;

(iv) Shughuli za binadamu ikiwemo kilimo na uvuvi; na

(v) Utupaji wa taka hovyo ambazo zina madhara kwenye mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaushauri Serikali kuhakikisha Sheria ya Mazingira Sura ya 191 inasimamiwa kikamilifu. Aidha, kufanya marekebisho ya Sheria ya Mazingira sura ya 191 iliyoanzisha Mfuko wa Mazingira ili uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ushuru wa bidhaa uliowekwa kwenye Saruji wa **shilingi 20** ambao unategemea kuongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 147,549.6** mapato yazingirwe (*ringfenced*) na kupelekwa kwenye mfuko wa Mazingira.

**5.0. MATUMIZI YA TAKWIMU ZA MATOKEO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI**

**Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kwamba katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilitenga kiasi cha **shilingi bilioni 400.928** kwa ajili ya zoezi la Sensa ya watu na makazi. Kwa mujibu wa Matokeo ya Sensa Tanzania idadi ya watu **61,741,120.** Idadi hii imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 3.2** ikilinganishwa na **asilimia 2.7** mwaka 2012. Aidha, Tanzania Bara ilikuwa na watu **59,851,347** sawa na **asilimia 96.9** ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu **1,889,773** sawa na **asilimia asilimia 3.1**.

### 5.1. Matumizi ya Takwimu ya Sensa katika Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 inaonyesha kwamba zaidi ya **asilimia 50** ya watanzania wote wapo kati ya umri wa miaka 15 hadi 60 ambao ni umri wa kufanya kazi. Mkoa wenye asilimia kubwa ya watu wenye umri huu ni Dar es Salaam (**asilimia 66.1**) ukifuatiwa na Kusini Unguja (**asilimia 59.7**). Aidha, Mkoa wenye asilimia ndogo wa kundi la watu wa umri huu ni Simiyu (**asilimia 45.6)**. Aidha, mwaka 2022, Kitengo cha Huduma za Ajira kilisajili watafutakazi **10,540** ikilinganishwa na watafutakazi **8,849** mwaka 2021, sawa na ongezeko la **asilimia 19.1.** Vilevile**,** idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ilikuwa **9,207,431**, sawa na **asilimia 15.4** ya watu wote Tanzania Bara. Kiwango cha wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi kimeongezeka kutoka **asilimia 5.58** Mwaka 2012 hadi **asilimia 5.7** kwa Mwaka 2022. Mkoa wenye asilimia kubwa ya wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi ni Kilimanjaro (**asilimia 10.4**) ukifuatiwa na Mtwara (**asilimia 9.1**). Aidha, Mkoa wa Katavi una asilimia ndogo ya kundi hilo (**asilimia 3.6**).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia matumizi ya takwimu za kidemografia zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika zoezi la Sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2022 katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo. Kamati inaamini kwamba endapo Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo vitafanyika kwa kufuata takwimu za Sensa ya watu na makazi, hususan kwa kuwaweka watu katika makundi mbalimbali kama vile makundi ya nguvu kazi na makundi tegemezi Taifa litakuwa na Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Dira ya Maendeleo ambayo italeta matokeo chanya katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na muda mrefu.


### 5.2. Mgawanyo wa Fedha za Maendeleo ili Kuchochea Ukuaji wa Uchumi kwa Mikoa Mbalimbali

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Sensa yanaonesha kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 5,383,728 sawa na asilimia 8.7 ya watu wote Tanzania Bara ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 3,699,872 sawa na asilimia 6.0. Vilevile, Mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi

ndogo ya watu wapatao **889,946** sawa na **asilimia 1.4** ya watu wote Tanzania Bara. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara kwa mwaka 2022 ulikuwa wastani wa **watu 68** kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa **watu 65** mwaka 2021. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa **watu 3,865** kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mwanza uliokuwa na wastani wa **watu 391** kwa kila kilometa ya mraba.

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi kwamba idadi kubwa ya watu na msongamano mkubwa wa watu katika mikoa iliyotajwa inasababishwa na kupatikana kwa huduma za kijamii na miundombinu bora pamoja na fursa za kiuchumi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia sera za kibajeti ili kuchochea maendeleo katika mikoa yote nchini. Hatua hii itapunguza watu kuhama kutoka mikoa mingine na kuelekea katika mikoa hiyo.

**Kielelezo Namba 6: Idadi ya Watu kwa Mkoa (Katika Milioni)**




**Chanzo:** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023*

**5.3. Utozaji wa Kodi ya Majengo kwa Maendeleo ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Idadi ya majengo nchini kulingana na Sensa ya Majengo iliyofanyika sambamba na Sensa ya Watu ni **14,348,372**. Kati ya majengo hayo, majengo **68,724** ni ya Ghorofa, majengo **13,540,363** ni ya kawaida (yasiyo ya ghorofa) na majengo **739,285** yapo katika hatua ya uendelezaji. Kwa ujumla, majengo yenye anwani za makazi ni **10,751,123** sawa na **asilimia 74.9**; wakati majengo **3,597,249** sawa na **asilimia 25.9** hayana

anwani za makazi. Tanzania Bara, **asilimia 74.8** ya majengo yote yana anwani za makazi.

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kwamba kwa mujibu wa mabadiliko ya kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Ukadiriaji), yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha namba 3 ya mwaka 2021 kila jengo la kawaida lililopo ndani ya kiwanja litalipiwa **Shilingi 12,000** na **Shilingi 60,000** kwa kila sakafu ya ghorofa. Kwa Halmashauri za Wilaya na miji midogo, nyumba za ghorofa zinatozwa **Shilingi 60,000**. kwa utaratibu huu mpya, kila mnunuzi wa umeme atakatwa **Shilingi 1,000** kwa mwezi kwa nyumba ya kawaida na **Shilingi 5,000** kwa kila sakafu ya ghorofa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia takwimu za majengo zilizopatikana kupitia sensa ili kutoza kodi ya majengo.

## 6.0. HOJA MAHUSUSI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 kanuni ndogo za 4, 5 na 6 na Kanuni ya 124 kanuni ndogo ya 1, 2 na 3 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023; Kamati ya Bajeti ilipokea jumla ya Hoja mahususi 22 kwa mujibu wa kanuni ya 117 na Hoja mahususi 5 kwa mujibu wa kanuni ya 124. Taarifa hii inatoa muhtasari wa mashauriano baina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Uongozi na Serikali.

### 6.1. Hoja zitokanazo na Majadiliano ya Kamati kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2023/24

#### 6.1.1. Hoja Zilizotokana na Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** hoja 10 zilizohusu utolewaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2022/23 zilipokelewa kutoka kwenye Kamati za Kisekta. Baada ya mashauriano baina ya Kamati ya Uongozi na Serikali kati ya hoja 10 zilizopokelewa, Kamati ilikubaliana na Serikali kwa hoja 5, na hoja 5 zilizosalia Serikali iliomba muda zaidi ili kuzifanyia kazi.

Hoja hizo ni:-

i. Utolewaji wa Barua ya Muamana (*Letter of Credit*) kwa Kampuni ya Mbolea ya Taifa (Tanzania Fertiliser Company - TFC) ili iweze kuagiza mbolea kwa wakati kuendana na msimu wa Kilimo;

ii. Kupitia upya Muundo wa Kitengo cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu (Financial Inteligence Unit - FIU) pamoja kufanya mabadiliko ya Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu ili kuendana na Miundo ya Kimataifa;

iii. Kuongeza fedha za dharura kwa Wakala wa Barabara Vijijini TARURA ili aweze kufanya ukarabati wa barabara zilizoharibika kutokana na mvua; na

iv. Kupitia upya Mgawanyo wa Mkopo wa **Dola za Marekani Milioni 150** ili kuongeza fedha kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuweza kupima vijiji vingi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali iliomba muda wa ziada ili kuzifanyia kazi hoja hizi, Kamati ya Bajeti itafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha Serikali inatimiza ahadi zake kwa Kamati ya Uongozi.

**6.1.2. Hoja za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea jumla ya hoja 12 zilizohitaji nyongeza ya fedha ya **Shilingi bilioni 97.7**. Baada ya mashauriano baina ya Kamati ya Uongozi na Serikali , Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali katika hoja 9 na hoja 3 zilihitaji ufuatiliaji zaidi.

Hoja hizo zilihusu:-

i. Kuongeza Fedha kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA);

ii. Mahitaji ya Fedha za Mishahara kwa Watumishi wa Hospitali ya CCBRT; na

iii. Fedha za dharura kwa ajili ya ukarabati wa barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu haya na kutoa ushauri kwa Serikali na Bunge kadri itakavyokuwa inawezekana.

**6.2. Hoja Zinazotokana na Majadiliano ya Bunge kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,** Hoja zilizopokelewa kutokana na majadiliano Bungeni zilikuwa Hoja 5. Hoja hizo zilihusu masuala yafuatayo:-

i. Uagizaji wa Mafuta ghafi ya mchikichi kutoka nje (Crude Palm Oil) pamoja na uzalishaji wa Mafuta ya kula ndani ya Nchi;

ii. Kuongeza fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ili kununua Helikopta kwa ajili ya kufukuza wanyama pori wakali na waharibifu;

iii. Kufanya Mapitio ya Mkopo wa Mradi wa Uboreshaji wa Milki ya Ardhi (LTP) wa **Dola za Marekani milioni 150** ili kupata fedha zaidi kwa ajili ya upimaji wa Ardhi na Mipaka ya Vijiji;

iv. Utozaji wa Ushuru wa Forodha kwa Bidhaa ya Kitenge pamoja na thamani ya bidhaa hiyo inapofika Bandari ya Dar es salaam; na

v. Upungufu wa Fedha za Kigeni nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na majibu ya Serikali na utekelezaji wa baadhi ya hoja hizo umeonekana kupitia hatua za kodi zilichokukuliwa na Serikali kupitia Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kabla ya kuanza utaratibu wa kutoa vibali vya kuagiza mafuta nje ya nchi (*import quota permit*) kujiridhisha na Takwimu za uzalishaji wa mafuta ndani ya nchi. Kutokufanya hivyo kunaweza kusababisha taharuki katika upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.

## 7.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MIFUKO MAALUM ILIYOZINGIRWA (RINGFENCED FUNDS)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilifanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Mifuko maalum na kubaini yafuatayo:-

### 7.1. Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Barabara ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tozo ya Barabara na Mafuta Sura 220 ili kuhakikisha uwepo endelevu wa fedha za kugharamia matengenezo ya barabara. Chanzo kikuu cha Mfuko huu ni tozo ya mafuta ya dizeli, petroli na ya taa zinazochangia jumla ya **Shilingi 363** sawa na **asilimia 98** ya fedha zote za mfuko. Vyanzo vingine ni pamoja na ushuru wa magari ya kigeni na tozo ya uzidishaji wa uzito. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 856.79.** Hadi kufikia Machi, 2023 Mfuko ulikuwa umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 653.79** sawa na **asilimia 76.31** ya bajeti. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutumia mfumo wa ujenzi wa barabara wa EPC + F ambapo katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya barabara saba zenye urefu wa Kilomita 2,035 zitajengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba fedha za Mfuko hazikidhi mahitaji ya kugharamia matengenezo ya barabara kikamilifu. Uwezo wa Mfuko kwa miaka mitano iliyopita umekuwa chini ya wastani wa **asilimia 50** ya mahitaji halisi ya fedha za kugharamia matengenezo. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa urefu wa mtandao wa barabara usioendana na ongezeko la bajeti kwa ajili ya ukarabati. Hivyo, kumekuwa na barabara zilizoharibika kwa kiwango kikubwa na kuhitaji matengenezo makubwa. Kutokuzitengeneza barabara hizo kwa wakati kutaathiri biashara ya usafiri na usafirishaji pamoja na matumizi ya bandari zetu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali iangalie mkakati mbadala wa ugharamiaji endelevu wa barabara zetu kama vile kutumia hatifungani za miundombinu pamoja na kushirikisha Sekta Binafsi kwa mfumo wa ubia.

### 7.2. Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Agency - REA)

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko wa REA uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 508.81**. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi bilioni 463.1** kinatokana na tozo kwenye Mafuta

na Umeme na fedha kutoka kwenye mkopo wa Shirika la Fedha Duniani (IMF- ECF) pamoja na **Shilingi bilioni 45.71** zinazotokana na michango ya Wabia wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 12 Aprili 2023, REA ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 475.39** kati ya matarajio ya **Shilingi bilioni 424.01** sawa na **asilimia 93.43**.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto iliyokuwa inawakabili Wakala wa Nishati Vijijini ni mikataba isiyoruhusu mabadiliko ya bei na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Kufuatia ushauri wa Kamati, Serikali ilifanya marejeo ya mikataba 39 kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na gharama zilizotokana na mabadiliko ya mikataba zilifidiwa na fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Programu ya Upanuzi wa Huduma ya Nishati Vijijini na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi .

### 7.3. Mfuko wa Maendeleo ya Reli (Railway Development Levy - RDL)

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Reli ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017 kwa lengo la kuendeleza na kukarabati miundombinu ya Reli nchini pamoja na kugharamia mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR. Chanzo cha mfuko huu ni tozo ya **asilimia 1.5** ya thamani ya bidhaa zinazoingizwa nchini (*imports*) kwa matumizi ya ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miaka miwili (2021/22 hadi Machi, 2023) akaunti ya mfuko ilikuwa na **Shilingi trilioni 1.04.** Aidha, katika kipindi hicho Shirika lilipata idhini ya kutumia **Shilingi trilioni 1.01.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 388.48** zilitumika katika mwaka 2021/2022 na **Shilingi bilioni 621.87** zimetumika katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Kamati, inaipongeza Serikali kwa kutumia fedha hizi kujenga reli ya kisasa ya SGR pamoja na kukarabati miundombinu ya reli ya kati ili iendelee kutoa huduma.

## 8.0. MAPITIO YA UTENDAJI KAZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI WA BAADHI YA MASHIRIKA, KAMPUNI, WAKALA NA MAMLAKA ZA UMMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9 (f) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 kinaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kukutana na Mashirika ya Umma ili kuangalia mizania yao ya fedha pamoja

na kuangalia endapo mashirika hayo yanafuata misingi ya fedha za umma na ya Sheria nyingine za nchi. Ili kutekeleza takwa hilo la kisheria Kamati ilifanya Tathimini ya utendaji kazi wa Mashirika, Kampuni, Wakala na Mamlaka hizo. Masuala yafuatayo yalibainika:-

**8.1. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (Tanzanian Petroleum Development Corporation - TPDC)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania - TPDC, ili kutathmini utendaji kazi wa Shirika katika kuongeza matumizi ya gesi asilia na Maendeleo ya Utaftaji wa Mafuta nchini. Aidha, Kamati ilibaini kwamba kati ya makampuni 22 yaliyopatiwa idhini na Serikali ya kuwekeza kwenye vituo vya gesi, makampuni 20 yameonyesha nia ya kuwekeza kwenye vituo vya kujazia gesi katika jiji la Dar es Salama na makampuni 2 yalionyesha nia ya kuwekeza nje ya Dar es Salaam. Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha makampuni kuwekeza nje ya Mkoa wa Dar es Salam ili kupanua wigo wa matumizi ya gesi asilia kwenye mikoa mingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua nia ya Serikali ya kujenga vituo vikuu viwili (mother CNG station) kwa ajili ya kujazia gesi kwenye magari. Vituo hivyo vinatarajiwa kujengwa katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kamati inashauri kwamba vituo hivyo vijengwe maeneo tofauti na maeneo yaliyo pendekezwa ili kundoa msongamano wa magari katika maeneo tajwa. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga moja ya vituo vya usambazaji katika maeneo yanayo milikiwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) ili kusaidia matumizi ya gesi asilia kwa magari ya Serikali.

**8.2. Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procureent Agency – PBPA)**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja ndio mfumo rasmi na pekee unaotumiwa na Serikali katika kuagiza bidhaa ya mafuta ya petroli, ni vyema basi mfumo huu ukatambuliwa kisheria. Kifungu cha 168(1) cha Sheria ya Petroli Sura 392 kimetumia maneno "*efficient procurement*" ambayo hayajatafsiriwa kwenye Sheria. Aidha, kifungu cha 168(2) kinampa Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni za mfumo huo

kama Sheria inavyoelekeza. Kamati inaishauri Serikali ili kuondoa mwanya wa matumizi mabaya ya maneno "*efficient procurement*" kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Petroli ili kutoa tafsiri ya maneno "*efficient procurement*" kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023.

**8.3. Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana (Capital Market and Security Authority - CMSA).**

**Mheshimiwa Spika,** CMSA imeendelea kusimamia masoko ya mitaji na kwa ujumla mwenendo wa masoko ya mitaji nchini ni wa kuridhisha kwani masoko yameendelea kuwa thabiti na himilivu. Hata hivyo, Kamati ilibaini ushiriki mdogo wa mifuko ya hifadhi katika masoko ya mitaji. Kumekuwa na upungufu wa ushiriki wa wanunuzi wakuu ambao ni mifuko ya hifadhi ya jamii uliotokana na maboresho yaliyofanywa katika sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuunganisha mifuko na kuundwa kwa *Public Sector Social Security Fund* - PSSSF. Ushiriki wa PSSSF haujawa mkamilifu kama ilivyokuwa hapo awali na hivyo kupunguza ukwasi kwenye soko la hisa. Takwimu zinaonyesha kuwa mifuko hii haijashiriki kununua hisa kwa takribani miezi 39. Kamati inaishauri PSSSF kuongeza ushiriki kwenye masoko ya mitaji ili kuchangamsha Soko la hisa nchini. Vilevile, Kamati inashauri PSSSF kuangalia mikakati yake ya uwekezaji ili kuhakikisha kuwa inafanya uwekezaji ulio na tija.

**8.4. Bohari ya Dawa – Medical Stores Department (MSD)**

**Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa – MSD inakabiliwa na changamoto ya mtaji wa jumla ya **shilingi bilioni 592.9** kwa ajili ya kununua na kuhifadhi dawa kwenye maghala pamoja na ujenzi wa maghala ili vituo vya afya viweze kuhudumiwa pale vinapohitaji dawa na vifaa tiba. Athari ya ukosefu wa mtaji ina sababisha ucheleweshaji wa dawa na vifaa tiba kwenye hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa MSD hulazimika kusubiria fedha kutoka kwa hospitali na vituo vya afya ndipo mchakato wa ununuzi wa dawa uanze.

**Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Fedha na Mipango kupitia Hotuba ya Bajeti ya Serikali Kuu ameahidi katika mwaka wa fedha 2023/24 kuipatia MSD mtaji ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuacha kutegemea fedha za hospitali na vituo vya afya katika manunuzi ya dawa na vifaa tiba. Hatua hii ni ya

kupongeza, hata hivyo Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha MSD inatumia mtaji huo ili kujiendesha kibiashara; na

(ii) MSD kuingia mikataba na makampuni yanayozalisha dawa ili iweze kununua dawa na vifaa tiba kwa bei nafuu kutoka kwa wazalishaji moja kwa moja badala ya makampuni binafsi yaliyopo nchini ambayo inauzia MSD kwa bei ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kusamehe baadhi ya vifungashio vya dawa na *moulds* kwa ajili ya utengenezaji wa dawa nchini.

**8.5. Shirika la Taifa la Maendeleo (National Development Corporation - NDC)**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Taifa la Maendeleo lilianzishwa kwa lengo la kuondoa ombwe la ugharamiajia wa miradi mikubwa ya kimkakati "Financing Gap" kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili kupata fedha kwa ajili ya miradi hiyo ya kimkakati. Hata hivyo, uhalisia umekuwa tofauti na matarajio na madhumuni ya Shirika hili. Kamati ilibaini masuala yafuatayo:-

i. Miradi mingi ni ya Muda mrefu na utekelezaji wake umeathiriwa na upatikanaji wa Bajeti ya maandalizi ya awali, vibali pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi na leseni kutoka katika Taasisi nyingine za Serikali;

ii. Uwepo wa miradi ya muda mrefu ambayo imepitwa na teknolojia na hivyo kuwa vigumu kufufuliwa kama ilivyo kwa kiwanda cha Matairi cha General Tyre cha Arusha;

iii. Miradi ya NDC kuwa chini ya Sekta mbalimbali hivyo kuleta ugumu katika usimamizi pamoja na utekelezaji. Mfano Miradi ya Magadi Soda katika ziwa Engaruka na Mchumuma na Linganga vibali na leseni ziko chini ya Wizara ya Madini, Mradi wa Kilimo cha Mchikichi uko chini ya Wizara ya Kilimo; na

iv. Taasisi nyingine za Serikali kama Tume ya Madini pamoja na Wizara ya Madini kutoza Shirika la NDC ada za leseni pamoja na vibali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ili kuweza kutatua changamoto ya upatikanaji wa mitaji ihusishe sekta binafsi ambao ndo wadau wakubwa na kuangalia uwezekano wa kuingia mikataba na wawekezaji ya ulipaji fidia na ujenzi wa miundombinu ili miradi itekelezwe kwa wakati.

**9.0. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) inayotoa mwelekeo halisi wa mwenendo wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2023/24. Bajeti ya mwaka 2023/24 imebeba dhima ya „***kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kuhimili na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha sekta ya uzalishaji ili kuboresha hali ya maisha***".

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 44.39** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 7.02** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/23 ya **shilingi trilioni 41.48**. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 30.31** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni **asilimia 68.2** ya bajeti yote na **shilingi trilioni 14.08** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 31.72** ya bajeti yote. Bajeti ya maendeleo inajumuisha **shilingi trilioni 10.80** fedha za ndani na **shilingi trilioni 3.28** fedha za nje.

**9.1. Mapato ya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kukusanya kiasi cha **shilingi trilioni 31.39**. Kati ya fedha hizo, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 26.73** sawa na ongezeko la **asilimia 13.02** ukilinganisha na ya mwaka 2022/23 ya **Shilingi trilioni 23.65.** Mapato yasiyo ya kodi anatarajiwa kuwa **Shilingi trilioni 4.66** sawa na ongezeko la **asilimia 39.10** ukilinganisha na lengo la mwaka 2022/23 la **Shilingi trilioni 3.35.** Aidha, mapato ya Halmshauri yaliongezeka na kufikia **Shilingi trilioni 1.14** ukilinganisha na **Shilingi trilioni 1.01** ya mwaka

2022/23 sawa na ongezeko la **asilimia 13.** Kwa ujumla mapato ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 16.22** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 27.01** ya mwaka 2022/23. Ukuaji wa mapato ya ndani ni zaidi ya mara tatu ya ukuaji wa Pato la Taifa la **asilimia 5.2** na ni takribani mara 4 ya mfumuko wa bei**.** Hivyo, ni wazi kwamba ili kuweza kufikia lengo hilo lazima kupanua wigo wa kodi pamoja na kuimarisha usimamizi wake. Kinyume na hivyo itakuwa vigumu kwa Serikali kufikia lengo hilo.

**9.2. Mikopo na Misaada Kutoka Nje**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inategemea kupokea jumla ya **Shilingi trilioni 5.47** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni ongezeko la **asilimia 17.63** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 4.65** ya mwaka 2022/23. Vilevile, Serikali inatarajia kukopa **shilingi trilioni 2.10** kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara Ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, fedha hizi zimepungua kwa **asilimia 30.69** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 3.03** zilizotarajiwa kukopwa katika mwaka 2022/23**.**

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imechangiwa na Serikali kuchukua tahadhari ya mikopo kutoka nje ambayo kwa hali ilivyo hivi sasa upatikanaji wake umekuwa mgumu. Tahadhari hiyo inatokana na masalia ya athari ugonjwa wa UVIKO – 19, vita ya Urusi na Ukraine, kufunguka kwa shughuli za kiuchumi pamoja na Sera za Marekani na Nchi za Ulaya za kupunguza ukwasi katika chumi zao na hatimaye kupunguza mfumuko wa bei.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mikopo ya ndani, Serikali imepanga kukopa katika soko la ndani kiasi cha **shilingi trilioni 5.44** ikiwa ni pungufu ya **asilimia 5.88** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 5.78** ya mwaka 2022/23. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 3.52** ni kwa ajili ya kudumisha deni (Rollover) na **shilingi trilioni 1.92** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**9.3. Sera za Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 44.39** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 30.31** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Shilingi trilioni 14.08** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Jedwali Namba 3: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti ya Serikali kati ya** Mwaka 2022/23 na 2023/24

| NA. | | 2022/23 | 2023/24 | TOFAUTI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | **MAPATO** | **B1** | **B2** | **B2-B1** | **(B2-B1)/B1*100** |
| 1. | Mapato ya Ndani | 27,005,582 | 30,237,128 | 3,231,546 | 11.97 |
| **NA.** | | **2022/23** | **2023/24** | **TOFAUTI** | **ASILIMIA** |
| | Mapato ya Kodi (TRA) | 23,652,758 | 26,725,409 | 3,072,651 | 12.99 |
| | Mapato yasiyo ya Kodi (TRA) | 3,352,824 | 3,511,719 | 158,895 | 4.74 |
| 2. | Mapato ya Halmashauri | 1,012,286 | 1,143,883 | 131,597 | 13.00 |
| 3. | Mikopo/Misaada kutoka Nje | 4,648,561 | 5,466,215 | 817,654 | 17.59 |
| | Mikopo ya Masharti Nafuu - GBS | 1,949,480 | 2,184,134 | 234,654 | 12.04 |
| | Misaada na Mikopo ya Miradi | 2,576,958 | 3,151,958 | 575,000 | 22.31 |
| | Misaada na Mikopo ya Kisekta | 122,123 | 130,123 | 8,000 | 6.55 |
| 4. | Mikopo ya Ndani na Nje | 8,814,152 | 7,540,840 | -1,273,312 | -14.45 |
| | Mikopo ya Nje | 3,034,004 | 2,100,464 | -933,540 | -30.77 |
| | Mikopo ya Ndani | 2,480,148 | 1,898,316 | -581,832 | -23.46 |
| | Mikopo ya Ndani - Rollover | 3,300,000 | 3,542,061 | 242,061 | 7.34 |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE** | **41,480,580** | **44,388,077** | **2,907,497** | **7.01** |
| | **MATUMIZI** | **B1** | **B2** | **B2-B1** | **(B2-B1)/B1*100** |
| 5. | Matumizi ya Kawaida | 26,475,748 | 30,310,847 | 3,835,099 | 14.49 |
| | Mfuko Mkuu wa Serikali | 11,308,365 | 12,771,533 | 1,463,168 | 12.94 |
| | Mishahara | 9,830,753 | 10,882,126 | 1,051,373 | 10.69 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 5,336,630 | 5,518,819 | 182,189 | 3.41 |
| 6. | Matumizi ya Maendeleo | 15,004,833 | 14,077,220 | -927,613 | -6.18 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Fedha za Ndani | 12,305,752 | 10,795,139 | -1,510,613 | -12.28 |
| | Fedha za Nje | 2,699,081 | 3,282,081 | 583,000 | 21.60 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | **41,480,580** | **44,388,067** | **2,907,487** | **7.01** |
| | **NAKISI YA BAJETI (% OF GDP)** | **3.0%** | **2.7%** | | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonyesha kuwa mapato yetu ya ndani ya **Shilingi trilioni 31.39** yanaweza kuhudumia kwa **asilimia 100** matumizi yote ya kawaida ya **Shilingi trilioni 30.31** ukiacha miradi ya maendeleo ambayo ni matumizi ya msingi. Hatua hii ni muhimu katika kupunguza utegemezi wa kibajeti, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mapato ya ndani ili kuweza kukidhi na kuhudumia mahitaji ya miradi ya maendeleo bila kusahau ushirikishwaji wa sekta binafsi.

## 10.0. HATUA ZA KIKODI ZINAZOPENDEKEZWA NA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### 10.1. Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Common External Tarrif -CET)

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 (The East Africa Customs Management Act 2004) yanaongozwa na Protokali ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki (The East Africa Customs Union Protocol) ya mwaka 2005. Aidha, mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2001, unataka Bunge la kila Nchi mwanachama kuridhia hatua za ushuru wa forodha za Jumuiya zilizopitishwa na Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Kanuni za Bunge hazielekezi utaratibu wa mapendekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za mabadiliko ya ushuru wa forodha kuwasilishwa Bungeni kabla ya kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki, Kamati ya Bajeti imeweka utaratibu ambao unawezesha Wizara ya Fedha kuwasilisha mapendekezo ya Ushuru wa Forodha kwa Kamati kabla ya kuyapeleka katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashiriki. Kamati

inampongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuendelea kudumisha na kuenzi utaratibu huo.

**10.1.1. Uchambuzi wa Hatua zilizopendekezwa kuhusu Ushuru wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali na kubaini kwamba, hatua mpya zilizopendekezwa ni 19 na hatua nyingine 44 ni muendelezo wa hatua zilizochukuliwa katika mwaka wa fedha 2022/23 na zinalenga masuala yafuatayo:-

i. Kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio sawa wa bidhaa kutoka nje ya Jumuiya pamoja na kuchochea uzalishaji wa viwanda vya ndani kwa kushusha gharama za malighafi zinazotumika katika uzalishaji;

ii. Kulinda na kuongeza ajira katika Jumuiya;

iii. Kuchochea uchakataji wa mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani ndani ya Jumuiya;

iv. Kushusha ushuru wa forodha kwa bidhaa muhimu zinazohitajika nchini;

v. Kuongeza Mapato ya Serikali;

vi. Kuchochea uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya kimkakati; na

vii. Kuimarisha ushirikianao wa kiuchumi kati ya nchi wanachama kwa kununua na kuuza bidhaa zinazopatikana ndani ya Jumuiya.

**10.1.2. Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mabadiliko ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania *(Confederation of Tanzania Industries)* ili kupokea maoni yao kuhusu Ushuru wa Forodha. Baada ya Kamati kuchambua maoni ya wadau hao, ina ushauri ufuatao:-

**10.1.2.1. Kuweka Mikataba Maalumu na wazalishaji wa Ndani wanaolindwa ili kukidhi mahitaji ya soko.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya wazalishaji wa ndani wamelindwa dhidi ya ushindani wa bidhaa wanazozalisha kutoka nje. Wazalishaji hao hulindwa kwa kutoza ushuru wa juu (*Import duty*) kwa bidhaa zinazoingizwa katika Jumuiya zinazofanana na zile wanazozalisha. Hata hivyo, baadhi yao wamekuwa hawazalishi kukidhi mahitaji ya soko. Mfano Tanzania kuna viwanda viwili vya uzalishaji wa mapipa vyenye uwezo wa kuzalisha **mapipa 120,000** kwa mwaka hata hivyo wanazalisha **mapipa 48,000** tu na hivyo kuleta upungufu wa **mapipa 72,000**. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha wazalishaji wote wanaolindwa wanakidhi soko la ndani na endapo itaonekana hawafanyi hivyo basi ushindani uruhusiwe ili wananchi wapate bidhaa kwa bei nafuu.

**10.1.2.2. Ubora wa Bidhaa na Malighafi zinazozalishwa nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba baadhi ya viwanda vilivyolindwa havizalishi bidhaa zenye ubora unaotakiwa. Mfano viwanda vya chumvi nchini vinazalisha chumvi zilizosafishwa kwa asilimia **asilimia 83** wakati chumvi inayotakiwa katika uzalishaji wa bidhaa za usafi (Detergent) ni **asilimia 85**. Pamoja na kwamba chumvi kutoka nje inatozwa ushuru wa **asilimia 25** ili kulinda viwanda vya ndani, ni lazima viwanda hivi vizalishe chumvi yenye ubora unaohitajika. Kutokufanya hivyo ni dhahiri kwamba tutaumiza viwanda vya ndani vinavyotumia chumvi kama malighafi kwa faida ya wazalishaji wa chumvi ambao hawataki kuongeza ubora.

**10.1.2.3. Ushirikishwaji wa Wamiliki wa Viwanda nchini kwa Mapendekezo yanayoletwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji, Viwanda na Biashara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kila Waziri huwasilisha mapendekezo ya nchi yake ili yaridhiwe na Baraza. Kamati imebaini kwamba baadhi ya mapendekezo ya nchi wanachama yanaathiri viwanda vya ndani lakini hupitishwa kwa sababu wamiliki wa viwanda hawashirikishwi ili kutoa maoni yao. Kamati inaishauri Serikali kutafuta utaratibu mzuri wa kuishirikisha Sekta Binafsi katika

mapendekezo yanayotolewa na nchi wanachama ili kupata maoni yao. Hatua hii itasaidia kupunguza madhara katika uzalishaji kwa viwanda vya ndani.

**10.2. Mabadiliko ya Kodi mbalimbali za Ndani kwa Mwaka wa Fedha 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria mbalimbali za kodi, ada na tozo zinazopendekezwa na Serikali pamoja na usimamizi wake na kubaini zinagusa maeneo yafuatayo:-

i. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (Blue Print);

ii. Kuchochea Sekta za Uzalishaji za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Viwanda;

iii. Kuchochea Sekta za Huduma kama Sekta ya Utalii; na

iv. Kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nimpongeze Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa moyo wake wa uthubutu wa kufanya mabadiliko katika Sheria za kodi ili kuchochea uchumi na kuondoa kero kwa wafanyabiashara. Baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameonyesha uthubutu ni yafuatayo:-

i. Kuongeza kima cha usajili kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka **Shilingi milioni 100** hadi **Shilingi milioni 200**. Ombi hili limekuwa la muda mrefu kwa wafanyabiashara nchini;

ii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake vinavyouzwa nchini. Hatua hizi zitaongeza idadi ya ndege za kukodi ili kuchochea biashara ya utalii;

iii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye malighafi za kutengeneza vifungashio vya madawa na moulds zinazotumika kutengeneza madawa ya binadamu. Hatua, hii itasaidia kuchochea uzalishaji wa madawa ndani ya nchi;

iv. Kurekebisha kifungu cha 56 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 ili miamala ya utoaji wa hisa mpya na uhamishaji wa miliki ya kampuni unaofanyika ndani ya nchi isitozwe Kodi ya Mapato. Kifungu hiki kimekuwa ni kikwazo kwa wawekezaji wengi nchini;

v. Kuanzisha utaratibu wa Kalenda ya kodi kwa kutobadili viwango vya ushuru wa bidhaa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2023/24;

vi. Kupunguza ada ya Mabango kutoka **shilingi 10,000** hadi **shilingi 7,000** kwa mita na ya video kutoka **shilingi 13,000** hadi **shilingi 10,000**;

vii. Kuhamisha ukusanyaji wa Kodi ya Mabango pamoja na Kodi ya Majengo kutoka Mamlaka ya Mapato kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti itafanya Uchambuzi wa kina wa hatua zote za Kodi zilizopendekezwa na itawasilisha Taarifa yake Bungeni kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023.

## 11.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 11.1. Tatizo la Upatikanaji wa Fedha za Kigeni Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za Kigeni nchini. Sababu za kutopatikana kwa fedha za Kigeni zimebainishwa vizuri na Serikali hata hivyo sababu za wapi tunapata fedha za kigeni hazijajadiliwa kwa kina. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba fedha za kigeni nchini kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na Sekta kuu tatu; Sekta ya Kilimo, Sekta ya Utalii na Sekta ya Madini. Aidha, kuna sekta nyingine ambazo zinachangia lakini si kwa kiasi kikubwa kama vile Sekta ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza masuala yafuatayo ili kusaidia kuongeza mauzo na huduma za Sekta hizo nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni nchini:-

(i) Kuanzisha utaratibu wa kutumia wabia yaani Public Private Partnership kwenye ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuchochea skimu za umwagiliaji. Hivi sasa Mabonde yote ya Umwagilia yaliyopo chini ya Tume ya Umwagiliaji yanategemea Bajeti ya Serikali. Hatua hii itasaidia kuwa na kilimo cha uhakika kisichotegemea mvua;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya Utalii katika Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu pamoja na Malikale ili kuwezesha watalii kufika na kuzuru maeneo hayo;

(iii) Kufanya mapitio ya Kodi, ada na tozo ambazo ni kikwazo katika kuongeza mauzo nje ya bidhaa na huduma ili kuchochea ukuaji na utolewaji wa huduma zitakazoliingizia Taifa fedha za Kigeni;

(iv) Kuchochea mauzo ya dhahabu na makaa ya mawe nje ya nchi; na

(v) Kudhibiti uagizwaji wa bidhaa zisizo za msingi ili kupunguza matumizi ya fedha za Kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini mapendekezo haya endapo yatafanyiwa kazi ni wazi kwamba tatizo la upungufu wa fedha za kigeni nchini litapungua kwa kiasi kikubwa.

### 11.2. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Fedha za Mikopo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti katika kipindi cha Miaka mitatu imepata fursa ya kupitia na kuchambua Taarifa za Mikopo Mitatu. Mikopo hiyo ni:-

i. Mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kupitia Dirisha la *Rapid Credit Facility* - RCF kwa lengo la kukabiliana na kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii zilizoathiriwa na ugonjwa UVIKO - 19 wa jumla ya **Shilingi trilioni 1.29;**

ii. Mkopo kutoka Dirisha la *Extended Credit Facility* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wa miaka mitatu wenye jumla ya **Shilingi trilioni 2.4**;

iii. Mkopo wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki ya Ardhi (LTP) kutoka Benki ya Dunia wa **Dola za Marekan milioni 150** sawa na **Shilingi Bilioni 350**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba mkopo ambao matumizi yake kwa takribani **asilimia 99** ulitumika kwa shughuli zilizokusudiwa ni Mkopo wa RCF au maarufu kama fedha za UVIKO. Aidha, kiasi cha fedha za mikopo mingine miwili kama ilivyoanishwa hapo juu kimeelekezwa katika shughuli ambazo hazina manufaa ya muda mrefu. Fedha hizo zimeelekezwa katika mafunzo, ununuzi wa vifaa vya ofisi, utekelezaji wa shughuli zisizo na tija na kutokuwa na mpango wa uendelevu wa miradi pindi mkopo utakapokoma.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na changamoto hii Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:-

i. Kuhakikisha matumizi yote ya mikopo yanaelekezwa kwenye miradi yenye kuleta tija na ama kuongeza mapato ya Serikali au kuweka amali za muda mrefu;

ii. Kuhakikisha kwamba fedha za mikopo hazitumiki kugharamia matumizi ya kawaida;

iii. Kuweka utaratibu wa kukagua shughuli zote za Wizara, Idara, Mamlaka na Wakala wa Serikali zinazoenda kutekelezwa ili kujiridhisha endapo zina malengo sawia na mkopo; na

iv. Kuhakikisha wakati wote utolewaji wa fedha unaenda kutekeleza shughuli zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwamba hatua hizi zitaondoa changamoto ya matumizi mabaya ya mikopo.

**11.3. Utafiti wa Vyanzo mbalimbali vya mapato na Sera za Kodi zinazopendekezwa na Serikali.**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayokabili utozaji wa kodi pamoja na usimamizi wake nchini ni kutofanyika utafiti wa kutosha kabla ya kuanzisha Sera mpya ya kodi au kuanzisha chanzo kipya. Hatua hii imekuwa ikisababisha mabadiliko ya mara kwa mara ya Sheria za kodi au marejeo ya viwango vilivyopendekezwa katika muda mfupi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanzia mwaka wa Fedha 2024/25 Muswada wa Sheria ya Fedha uambatishwe na muhtasari wa matokeo ya utafiti wa hatua mbalimbali zinazopendekezwa tofauti na ilivyo sasa ambapo maelezo yanayoambatishwa ni nia na madhumuni ya Muswada tu. Aidha, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili yakufanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato pamoja na Sera za kodi.

**11.4. Utaratibu wa Uwasilishaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha Kila Mwaka Bungeni.**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha ni Muswada unaowasilishwa Bungeni kila mwaka. Hata hivyo, uzoefu wa Kamati unaonyesha kwamba Muswada huo katika kipindi cha miaka 7 haujawahi kusomwa kwa mara ya kwanza na ya pili na kupitishwa ndani ya siku 14 kabla haujapitishwa na Bunge. Hatua hii imekuwa inaleta changamoto ya muda kwa Kamati ya Bajeti kuuchambua, kufanya utafiti na kushirikisha wadau kabla ya kuwasilisha Taarifa ya maoni yake Bungeni. Mataifa ya jirani kama Kenya Muswada huo huchukua si chini ya mwezi mmoja. Mfano Muswada wa Fedha wa mwaka 2023 wa Kenya ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la Kenya Tarehe 28 Aprili, 2023 na hivi sasa ndio unajadiliwa na Serikali. Hatua, hii inaleta uwazi katika jamii na kuondoa mtazamo hasi wa jamii kudhani kwamba Bunge lao Tukufu linapitisha Sheria kandamizi za Kodi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba muswada unawasilishwa Bungeni mapema zaidi walau mwezi mmoja kabla haujapitishwa na Bunge.

**11.5. Utungaji wa Kanuni zinazoenda kutekeleza Sheria Mbalimbali za Kodi.**

**Mheshimiwa Spika,** ni utaratibu wa kawaida kwa Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti

mbalimbali ya Sheria. Aidha, Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 kifungu cha 38 kimeweka utaratibu wa kuwasilisha kanuni Bungeni kwa ajili ya kuzipitia na kufanya marekebisho pale inapobidi. Kamati ya Bajeti imebaini kwamba Kanuni zimekuwa ni kichocheo cha kuanzisha ada, tozo na faini mbalimbali. Aidha,kuna baadhi ya Kanuni hutungwa kinyume na malengo yaliyopo kwenye Sheria. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kanuni zote zitakazotungwa zenye lengo la kuanzisha, ada, tozo au faini ziidhinishwe kwanza na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kabla ya kutolewa kwenye gazeti la Serikali na kuanza kutumika kwa sababu ndiye mwenye mamlaka kwenye masuala yote ya fedha.

**11.6. Uwiano wa Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa.**
**Mheshimiwa Spika,** Taifa letu limekuwa na uwiano wa chini kati ya Pato la Taifa na Mapato ya Kodi. Wastani wa Pato la Taifa kwa Makusanyo ya Kodi kwa mwaka 2022 ilikuwa ni **asilimia 12.3** na uwiano wa mapato yote ya ndani kwa pato la Taifa ni **asilimai 14.9**. Uwiano huu ni chini ya uwiano kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni **asilimia 15**. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi na kubaini masuala ambayo yanachangia hali hiyo ni yafuatayo:-

i. Wingi wa mamlaka za udhibiti ambao unasababisha wafanyabiashara wengi kuogopa kurasimisha biashara zao;

ii. Kutosomana kwa mifumo ya kukusanyia mapato na baadhi ya mapato ya Serikali kukusanywa nje ya mifumo iliyopo;

iii. Ukubwa wa sekta isiyo rasmi;

iv. Biashara za Magendo katika mipaka ya nchi kavu na bahari;

v. Mtazamo hasi wa wananchi kuhusu ulipaji wa kodi hasa katika kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi;

vi. Ukusanyaji hafifu wa Kodi za Serikali mfano kodi ya majengo na Kodi ya Ardhi; na

vii. Elimu duni ya ulipaji wa kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini endapo changamoto hizi hazitapatiwa ufumbuzi kwa wakati Tanzania itaendelea kuwa chini ya wastani wa uwiano wa Kodi na Pato la Taifa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

**11.7. Mfumo wa Kurejesha Asilimia 20 ya Mapato yanayokusanywa na Halmashauri Kutokana na Kodi ya Majengo, Kodi ya Mabango na Kodi ya Pango la Ardhi.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Majengo na Sheria ya Ardhi ili kurejesha utaratibu wa ukusanyaji wa Kodi ya majengo na kodi ya Pango la ardhi kwa Serikali za Mitaa. Aidha, uamuzi wa kurejesha **asilimia 20** ni wa busara ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa vyanzo hivyo vya mapato. Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kujiendesha wenyewe *(automated)* ili pindi makusanyo yanapokusanywa moja kwa moja **asilimia 20** irudi kwenye akaunti za Halmashauri husika. Mfumo ukiachwa kama ulivyo hivi sasa zikaingia Mfuko Mkuu wa Serikali inaweza kuwa vigumu kurejesha fedha hizo.

**11.8. Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji Wanaozalisha Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (Export Credit Guarantee Scheme - ECGS) na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme - SMECGS).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Mfuko wa Dhamana kwa wakopaji wanaozalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi**.** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 zimetengwa jumla ya **shilingi bilioni 600** ambapo Benki Kuu ya Tanzania itatoa **Shilingi bilioni 280** na Benki ya Dunia itatoa mkopo nafuu wa **Dola za Marekani milioni 150**. Hatua hii ina lengo la kuongeza mauzo nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kabla ya kuanza kutumia fedha hizi kuweka wazi masuala yafuatayo: vigezo vya

wanufaika, nyaraka zitakazotakiwa kuwasilishwa, Sekta zinazolengwa au kupewa kipaumbele, kiwango kitakachokuwa kinatolewa kulingana na uwezo na mchakato wa kupokea maombi na kuchagua washindi. Kamati inaamini bila kuwa na vigezo na utaratibu kuna uwezekano wa fedha hizo kutotumika kwa matumizi yaliyokusudiwa kama ilivyokuwa Mwaka 2007 kuhusiana na *External Payment Arrears Account* maarufu kama EPA ambapo **Shilingi bilioni 133** kutoka Benki Kuu zilitumika kwa matumizi yasiyokusudiwa.

**11.9. Utaratibu wa Matumizi ya Seti ya Mitambo 25 kwa ajili ya kuchimba visima na mabwawa**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kusambaza seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika Mikoa 25 na seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa katika kila kanda. Hata hivyo, kila Halmashauri italazimika kuwa na kiasi cha **Shilingi milioni 15** ili kuweza kutumia mitambo hii. Hatua hii itaziathiri Halmashauri zenye mapato madogo ambazo zitashindwa kutumia fursa hii ipasavyo ilihali Halmashauri zenye mapato mengi zitanufaika. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu ambao utawezesha Halmashauri zenye mapato madogo kunufaika na mitambo hiyo kwa kutoa ruzuku kwa Halmashuri zisizokuwa na mapato makubwa ili nazo zinufaike na Mitambo hiyo.

**12.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mhe. Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wote. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali nzima kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kipindi chote.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati wakiongozwa na Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Bi. Lilian Masabala, Ndg. Wilfred Akasi na Bi. Trifina Karaguza pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Fadhat Kamote kwa kuipatia Kamati

ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
19 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa mawasilisho hayo ya maoni ya Kamati kwa niaba ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina ya Wabunge ambao wameomba kuanza kuchangia bajeti kuu ya Serikali, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, ajiandae.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwako kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Bajeti Kuu ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema sisi Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako tukufu, lakini kubwa nikupongeze na kukushukuru wewe kwa umahiri wako, uhodari wako, uzoefu wako, kwa kweli unaliongoza Bunge vizuri, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge na tujipongeze Waheshimiwa Wabunge wote tulivyo mpata Mheshimiwa Spika huyu, ahsanteni tujipongeze Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Spika kaka yetu Azzan Zungu kwa kazi nzuri anayofanya ya kukusaidia wewe. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza

kuchangia kwa namna hii toka nizaliwe naomba nianze mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nikipongeze sana chama chetu Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri kinachofanya kutengeneza Ilani inayotekelezeka kwa mpango wa bajeti tunayokwenda kupitisha leo na kipekee nimpongeze sana Mwenyekiti wa chama chetu Ndugu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukiongoza vizuri Chama cha Mapinduzi. Lakini kipekee nimpongeze kaka yetu *Comrade* Abdulrahman Kinana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi anavyomsaidia Mheshimiwa Mwenyekiti wa chama chetu na nimpongeze *Comrade* Daniel Chongolo, Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo anasimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia kwa bajeti kuu ya Serikali kama ambavyo nimeomba, lakini kubwa naomba nianze kwa kweli kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuandaa bajeti kubwa na nono ambayo haijawahi kutokea kwa takribani miaka yote toka nchi yetu imeumbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kujadili na kupitisha bajeti hii kubwa ya shilingi trilioni 44.14; ni bajeti kubwa sana inayokwenda kujibu na kutatua kero za Watanzania wanyonge. Hongera sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa kutuleta bajeti hiyo kubwa. Lakini Waheshimiwa Wabunge mnakwenda kuvunja rekodi kuwa Wabunge wa kwanza kupitisha bajeti kubwa ya namna hii, hongereni sana kwa kupitisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na bajeti; kwa takribani miaka minne iliyopita bajeti ambayo tumeipitisha katika Bunge hili ukiangalia na ukilinganisha na bajeti ya leo ni kubwa, hii bajeti inakwenda kuisha maradufu kuliko za miaka iliyopita. Mwaka 2019/2020 tulipitisha katika Bunge hili hili takribani shilingi trilioni 29.5 na tukapeleka fedha za maendeleo shilingi trilioni 9.3, mwaka uliofuata mwaka 2020/2021 tukapitisha bajeti katika Bunge hili hili shilingi trilioni 34.8 na tukapeleka kwenye fedha za maendeleo shilingi trilioni 13.3, mwaka 2021/2022 tukapeleka bajeti shilingi trilioni 36.84 na tukapeleka kwenye miradi ya maendeleo shilingi

trilioni 13.87. mwaka jana kwa maana mpango unaomalizika tulipitisha trilioni kama mnavyofahamu shilingi trilioni 41.48 na zilizokwenda kwenye miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 15.00.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu bajeti hii ikipita ni shilingi trilioni kubwa zaidi ya shilingi trilioni 2.8 zaidi ya bajeti iliyopita ambayo ni takribani asilimia 7.0 ya bajeti zilizopita. Tujipongeze sana Wabunge, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze sasa kwenye miradi ya kimkakati, tumeona kwenye bajeti nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mwigulu Madelu Nchemba hongera sana kwa kazi kubwa. Wewe na timu yako Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mwigulu kwa sababu alivyoisoma bajeti ya juzi imetatua na inakwenda kujibu kero za Watanzania wanyonge. Hongera sana kaka yangu Mwigulu Mungu akutangulie, tuna matumaini makubwa bajeti ikitekelezeka maana yake utafanya kazi ya kukumbukwa kwa dunia nzima, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze sasa kwa miradi michache ya kipaumbele. Tumeona Mradi wa *SGR,* tumeanza kuutekeleza takribani miaka minne iliyopita, lakini kasi tunayokwenda nayo hatuna budi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha kudhihirisha kwamba utekelezaji wa mradi huo utakamilika kama ulivyotarajiwa na tunaona miradi mikubwa kama ambavyo ameweka dhamira yake wazi kwamba kazi inaendelea tunamhakikishia sisi Waheshimiwa Wabunge na mimi ninasema kwa niaba yangu na wananzengo ambao wanatusikiliza, Mheshimiwa Rais kazi anayoifanya ni ya uzalendo sana. *(Makofi)*

Ndugu zandu Waheshimiwa Wabunge hii treni ya *SGR,* ya mwendo kasi ikitekelezwa kama ambavyo tumepanga nimeona kwenye bajeti ilivyosomwa katika nchi za Afrika Mashariki itakuwa ndio treni ya kwanza kutembea kuliko nchi nyingine ambazo zinatuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni treni ambayo tumeona bajeti yake ni kubwa, lakini utekelezaji wake unakwenda vizuri. Nimesikiliza vizuri sana bajeti ya Mheshimiwa Mwigulu na Waziri wa Ujenzi kwamba tumeshakamilisha kipande cha kilometa 300 kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na tunakwenda kukamilisha umbali wa kilometa 822 kutoka Morogoro kwenda Makutopora na kutoka Makutopora kwenda mpaka Tabora takribani kilometa 371 zinakwenda kutekelezweka na itakamilika si muda mrefu, lakini kutoka Isaka kwenda Mwanza kilometa 341 inakwenda kukamilika na kutoka Isaka kwenda Tabora 342 zinakwenda kukamilika, kutoka Tabora mpaka Kigoma kilometa 506 zinakwenda kukamilika. *(Makofi)*

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu wenzetu majirani wetu wanajiandaa pia kujenga *SGR,* lakini nataka niwape taarifa kwamba Rwanda hawajaanza kutumia, Burundi hawajaanza kutumia, Kenya hawajaanza kuitumia, sisi chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakwenda kuwa watu wa kwenza kutumia treni ya mwendokasi ya *SGR* ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Lakini hiyo haitoshi na nikapenda niwaambie Watanzania treni hii nadhani tumeshapata taarifa kwamba ina uwezo wa kukimbia umbali wa kilometa 160 kwa saa. Sasa hesabu kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ambapo ni kilometa 1,112 itakwenda masaa mangapi? Kwa hiyo, ni masaa machache sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Watanzania tujiandae kuitumia ili iweze kulrta tija kwenye shughuli zetu za uchumi. Lakini nitoe rai tu kwa wasimamizi kwamba isimamie kwa haraka, ikamilike haraka ili Watanzania waanze kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *SGR* napenda nizungumze eneo hili kwa upana kidogo, itakuwa inatumia umeme na ni mara ya kwanza sisi hapa Bara la Afrika ukiondoa Ethiopia ambao walianza kuitumia kwa umbali wa kilometa 752. Ukiondoa Ethiopia, Morocco, Afrika ya Kusini na Nigeria nchi inayofuata kwa nchi za Afrika ni Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amedhihirisha kwa nchi za Afrika Mashariki kuwa Rais wa kwanza kuanza

kulitembeza na kulikimbiza li-*SGR* tukiwa sisi Watanzania. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumze mabehewa yatakayoanza kufanya kazi kwa nilivyosoma katika Taarifa za Serikali. Kutakuwa na mabehewa takribani 400 ya abiria lakini mabehewa 59 yataanza kuingia na mabehewa 14 yameshaanza kuingia. Mheshimiwa Waziri wa ujenzi na wewe hongera sana Kaka Mbarawa kwa kusimamia kwa ubora kabisa kazi hiyo. Lakini hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Rais ameifanya na sisi watendaji tumuunge mkono kwa kuharakisha utekelezaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabehewa haya yatakuwa na uwezo wa kutunza umeme kwa masaa manne bila kukatika hata kama umeme utakatika sehemu zingine. Kwa hiyo, ni jambo la kheri ni uhakika kwamba yatafanya kazi lakini mabehewa ya mizigo yatakuwa takribani 1,430. Sasa elewa ni mizigo mingapi ya Watanzania itabebwa katika mabehewa yale kwa muda mfupi. Kwa hiyo, ni kazi nzuri naomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais na Serikali tukamilishe mradi huu na mradi huu ndugu zangu Wakenya wanatengemea kuanza kuujenga mwakani na Burundi na Uganda na sehemu nyingine mwaka 2025. Kwa hiyo, miaka mitatu hii tutakuwa tunaongoza katika ulingo wa kuhudumia hapa Afrika Mashariki, Tanzania tukiongoza kukimbiza na kutembeza li-treni la mwendo kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere; naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais nimeona fedha zilizotolewa kwenda kukamilisha mradi ule kwa mwaka jana takribani shilingi bilioni 869 ambazo tuna matarajio kwa muda uliopangwa mradi huu unakwenda kukamilika. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira hiyo ya kutoa fedha na wewe Mheshimiwa Mwigulu Nchemba usingekuwa unatoa fedha mradi usingefika kiwango hicho, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati Kaka yangu January Makamba kwa kusimamia vizuri pamoja na timu yake pamoja na *TANESCO* wanafanya kazi nzuri

ni matumaini yetu kwamba mradi ule unakwenda kufufua uchumi kwa kiwango cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnaonisikiliza, Mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mradi mkubwa sana. Kama tulivyo kwenye *SGR* kwa nchi za Afrika Mashariki ndio bwawa kubwa peke yake hakuna bawawa lingine linalozalisha umeme wa namna hii na kwa nchi za *SADC* ni bwawa la tatu kwa ukubwa ikiongozwa na Bwawa la Mambilla lililoko Nigeria na Caculo Cabaça la Angola na linafuata la Tanzania. Kwa Afrika nzima ni bwawa la nne ukiondoa la Ethiopia ambalo ni Renaissance, la megawati 6,450 na duniani kote ni bwawa la 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuelewane, sasa elewa dunia kuna nchi ngapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa Afrika anaongoza kwa kuwa na bwawa kubwa kwa nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais hongera sana kwa kazi hiyo tunakwenda kufufua uchumi tunakwenda kumaliza changamoto za kinishati tukikamilisha bwawa hili pamoja na miradi mingine itakapo kamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeze Serikali na Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge, na ninyi Waheshimiwa Wabunge mnakwenda kuingia kwenye rekodi ya Bunge *Hansard* zitaandika kwamba militekeleza miradi hii mikubwa kwa niaba ya Watanzania. Mjipongeze sana kwa kazi nzuri tunayoifanya. Bwawa la Mwalimu Nyerere likikamilika litatuongezea umeme, kwa sasa nimeona kwenye taarifa kwamba tuna takribani megawati 1,872 kwa uwezo wa juu, ingawaje mahitaji yetu nilivyoona kwenye taarifa ni megawati 1,432.05 lakini tukikamilisha tutakuwa na takribani megawati 4,193 ukijumlisha na miradi mingine. Maana yake nini? Mwaka 2025/2026 miaka inayokuja michache mahitaji yetu ya umeme yaweza kufikia megawati 2070 kwa sasa mahitaji yetu ni megawati 1,432.05. Kwa hiyo, tutaweza kujitosheleza kuwa na umeme nchini, lakini na kuwasambazia majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge leo hii Kenya ana jumla ya megawati 2,722 anahitaji umeme takribani megawati 500; kwa hiyo, tunaweza kumuuzia. Rwanda ana megawati 230, Burundi ana megawati 86, Zambia ana megawati 1,472; sisi tunakwenda kuwa na megawati 4,198 mnasubiri nini kupiga makofi kwa Mheshimiwa Rais wetu, ni kazi kubwa ameifanya. Lakini ni ninye Waheshimiwa Wabunge na Serikali na wananzengo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sekunde 30 malizia sentensi yako.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee dakika mbili. Mradi huu unakwenda kujibu kero za Watanzania, mahala ambapo kuna changamoto za umeme. Tumeelewa bado kuna vitongoji takribani 36,101 lakini mradi unakwenda kukamilisha vitongoji vya Wabunge takribani vyote, hata kwako pale Igomba, Itonya na Itua ambako kuna kero wanakwenda kupelekewa umeme. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba Watanzania wengi watapata umeme, hata Gezaulole kwa Mheshimiwa kule Kigamboni watapata umeme, mpaka kule Itonya na maeneo mengine ambayo nimesema mpaka Katubuka watapata umeme. Kwa hiyo, ni matumaini hata kule Chato kwenye Majangala watapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mkubwa sana ni mategemeo yetu kwamba utakwenda kujibu kero za Watanzania.

Naomba niombe kidogo kwa sababu hela hizi ni nyingi zinakwenda kwa wananchi takribani kujibu kero za Watanzania wanyonge na wakulima wanyonge. Ninajua mradi huu utakwenda kwa Watanzania milioni 61; utakwenda kwa ng'ombe tulionazo milioni 6.6; kwa mbuzi milioni 21.6; kwa kondoo milioni 92.7; pamoja na nguruwe milioni 3.7; na mifugo mingine, lakini tutatatua kero za wakulima wetu kwa ajili ya kuwapelekea kilimo cha umwagiliaji. Naona Mheshimiwa Bashe umefanya kazi kubwa

sana, peleka miradi ya umwagiliaji kule Chato, maeneo ya Makurugusi, Ilyamchele, Nganza, Rubambangwe, Nyambogo, Katende, Mongela pamoja na maeneo mengine ambayo hayajapata mradi wa umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimiwa Mbarawa tumepitishia bajeti kubwa sana; kuna barabara ya kero kubwa ya muda mrefu kule Jimbo langu la Chato na wanachato wananisikia, kutoka Nyamirembe - Gatini mpaka Katoke yenye umbali wa kilometa 51.0 inayojengwa kwa kiwango cha lami. Naomba uanze kutekeleza miradi hiyo kwa sababu Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 2.3 na tayari umezipokea. Tangaza *tender,* peleka ma-*bulldozer* wananchi wa Ichwankima wanaopitiwa na barabara hiyo, wananchi wa Busarara, wananchi wa Nyambiti, wananchi wa Kalwelezo, wananchi wa Kazunguti, wananchi wa Kasenka mpaka Katoke mradi uweze kukamilika kwa kiwano cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba kipekee, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, tumtakie kila la kheri sisi pamoja na Watanzania wote Kwenda kutekeleza mradi huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge huyu amepewa upendeleo kwa sababu hajawahi kuchangia, kwa hiyo, wewe mwingine utakatwa. *(Kicheko/Makofi)*

Usije ukasema sasa Mheshimiwa mbona anapendelea, aah aah! Huyu hajawahi kuchangia, kwa hiyo wengine fuata muda uliopangiwa tafadhali. Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu mimi kwanza naunga mkono bajeti, kwa sababu kuna miradi mikubwa ya Musoma Vijijini ambayo inaanza mwezi wa nane, barabara na kilimo cha umwagiliaji na miradi mingi, kwa hiyo, Musoma Vijijini tuunge bajeti hii mkono, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mimi utakuwa una takwimu, mjitayarishe kwa takwimu. Ni kwamba ninachangia namna ambavyo uchumi wetu unaweza kukua kwa haraka. Sasa hivi tuko kwenye kati ya 4% na 5%; tulikuwa tuko kwenye 7% tukashuka kwa sababu nyingi zilizoelezwa na kuondoa umaskini hii ni wachumi wa dunia magwiji wote wanasema uchumi ni lazima ukue zaidi ya 8%. Kwa hiyo, kati ya 8% mpaka 10%, ndio mchango wangu mimi; mipango na ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipanga kwenye maendeleo ya miaka mitano ikifika mwaka 2025 tuwe na *GDP per capita* ya dola 3,000 na kufika huko kwa mahesabu yote wanaojua uchumi, wanaojua mambo ya umeme unahitaji umeme wa megawati 10,000; kwa hiyo, umeme haujatosha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hali ilivyo ni kwamba *GDP per capita* yetu mwaka jana ilikuwa dola 1,253; jirani yetu alikuwa *GDP per capita* dola 2,278; nimechukua Algeria ambayo ina gesi ina *GDP per capita* dola 4,315; Seychelles naichukua kwa sababu ina elimu bora sana Afrika halafu ndio yenye uchumi bora, ina *GDP per capita* zaidi ya dola 19,000. Nini tufanye uchumi wetu ukue kwa 8% mpaka 10%?

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa ni umeme, alipoishia Dkt. Kalemani, lakini tunahitaji umeme wa uhakika, tunahitaji umeme mwingi na umeme wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa vipimo vya umeme duniani na hivi ndio vipimo vya kiuchumi, sio kusema unaweza ukafikisha umeme kwenye kijiji, kwenye kitongoji hata ukafikisha vitongoji vyote suala linakuja ni wangapi kwenye hicho kitongoji wanatumia huo umeme. Hicho ndio kipimo cha kiuchumi *(electricity consumption*

*power per capita)*. Vilevile ukifikisha hapo unaweza ukasema wangapi wamepata fursa kwenye hicho kijiji kupata umeme *(access to electricity)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba ripoti zetu zinavyotoka Serikalini lazima zitaje hizo takwimu, ukisema tu vijiji na vitongoji hujajibu hoja ya kiuchumi. Sasa angalia mambo ya umaskini na utumiaji wa uchumi. Nimewatajia Seychelles *GDP per capita* yao zaidi ya dola 19,000; *power per capita* ni *units* 4,514 tunaiita sisi *unit,* lakini ni *kilowatt hour.* Unakuja Algeria yenye gesi, umeme wanaotumia *power per capita* ni *units* 1,600; unachukua Kenya ambayo inatuzidi *GDP per capita*, *power per capita* yao ni *unit* 170 na Tanzania ni 103, hizi ni kidogo ni chache kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Tanzania tufanyeje? Cha kwanza tuongeze umeme na vyanzo vya umeme viwe vingi, siyo kimoja. Tatizo letu ukisema vyanzo vingi wengine wanasema unachukia bwawa, ni watu wasiokuwa na uelewa. Tunataka vyanzo vingi na umeme wetu utokane na *natural gas,* utokane na maji, utokane na makaa ya mawe. Halafu unaenda kwenye *renewables* yaani *geothermal, solar, wind, biomass, biogas, tides and waves.* Hapo lengo letu ni kufikisha umeme wa megawati 10,000. Hapo ndio tutaanza kusema sasa uchumi unaanza kukwamuka.

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme nayo napendekeza ipunguzwe, sasa hivi umeme majumbani ni *US cents 9.7* kwa *unit,* viwandani ni *unit 10* ndio zinatumika *US cents 10* kwa *unit.* Kenya wako juu, lakini hii siyo sababu ya kufanya sisi tusipunguze umeme kwa sababu eti nchi za Afrika Mashariki umeme bei iko juu. Kwa hiyo, bei ikiwa chini watumiaji watakuwa wengi. Sasa ili uchumi ukue kwa kasi tunahitaji umeme mwingi na tufikishe zaidi ya megawati 10,000.

Mheshimiwa Spika, kingine cha pili ambacho kitafanya uchumi ukue kwa kasi na umaskini uzidi kutokomea, tuna mambo ya kilimo sawa, mambo ya madini sawa, mambo ya utalii sawa. Kuna kimoja ambacho lazima bajeti inayokuja iwekee mkazo ni uchumi wa gesi. Uchumi wa gesi ni hivi, natoa Algeria ndio ina-*export LNG* ya kwanza Afrika nzima, ina-*export* tani 29.3 kwa

mwaka. *GDP* yake niliyowatajia zaidi ya dola 3,000. Qatar ndio ina-*export LNG* ya kwanza duniani ni tani 80,000,000. *GDP per capita* ya Qatar ni zaidi ya dola 84,000.

Mheshimiwa Spika, sasa Tanzania tufanyeje? Lazima tuongeze mambo ya gesi. Sasa hivi tunazo hizo trilioni 57.5 ni nyingi, lakini hatujafanya kazi zaidi. Algeria wanazo *159 TCF,* Mozambique majirani zetu wanazo 100 mpaka *200 TCF*. Kwa hiyo, Tanzania tufanye nini? Lazima tutafute mafuta na gesi kwa bidii zaidi na ndiyo maana mimi mpaka leo hii naamini kabisa kwamba *TPDC* haifai kufanya kazi ya kuuza mafuta ambayo inaweza kufanywa na kila mtu. Lakini kila mtu hawezi kutafuta mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, Mozambique wanaanza ku–*export LNG* kwa gesi inayotoka *Ruvuma Basin*. Sasa sisi tuko na wao kwenye *Ruvuma Basin*. Tunapaswa kuiuliza *TPDC* huko tuna gesi kiasi gani? Tuna mafuta kiasi gani? Maana yake wenzetu kwenye hiyo *basin* wameshapata *over hundred trillion cubic feet of natural of gas*. Sisi huku chini hatujafanya *explorations. TPDC* iende huko, iache kuuza mafuta. Hatujatafuta mafuta kwenye Ziwa Tanganyika, kwenye Ziwa Nyasa, kwenye Ziwa Rukwa na muhimu zaidi tena wewe Spika ni mwanasheria, huko tunakoenda kuna hizi *resources* zitakuwa kwenye mipaka ya nchi mbili, kwa hiyo, *TPDC* ina kazi mafuta na gesi yakipataikana Ziwa Tanganyika, sisi na Congo na Zambia mambo yatakuwaje? Tukienda *Ruvuma Basin* tukapata gesi na Mozambique wana gesi hiyo *shared resource* itakuwaje?

Kwa hiyo, tuweke mkazo kwenye utafutaji wa gesi na mafuta na wataalamu wapo tumewasomesha ambao mimi nawafahamu tumewasomesha Norway tulipeleka *Masters* 40, hatujui wanafanya kazi gani? China tulipeleka *Masters Ph.D* 100, vijana wengi wamesoma kwenye *oil and gas* hawana kazi.

Sasa *natural gas;* uchumi wa gesi kwa Tanzania matumizi ya kufanya uchumi ukue cha kwanza kabisa tuzalishe umeme yaani *kilowatt hour* moja hiyo *unit* moja inahitaji *cubic feet 7.36* kuzalisha *unit* moja ya umeme na sisi tuna *materials* na uzuri wa umeme na gesi hauna ukame, hauko *capital intensive*. Kwa hiyo, umeme

mwingi tungeutoa siyo kwamba tunasimamisha maji, lakini tungewekeza sana kwenye gesi tupate umeme mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha pili, uchumi wetu kukua kutokana na *natural gas.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia Profesa.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Spika, ni mambo ya mbolea na mambo ya viwandani.

Sasa nimalizie hiyo dakika moja kwa biashara ya *LNG*. Biashara ya *LNG* itatusaidia kwa sababu duniani sasa hivi kufika mwaka 2030 biashara hiyo itakuwa na ukubwa wa dola bilioni 210; Tanzania lazima ipate pale. Msumbiji wana *LNG plants* mbili, ya kwanza inaitwa *Floating LNG* ambayo gesi wameenda kuichukua huko huko baharini na wameanza kusafirisha tani 13,000,000 kwa mwaka za *LNG* na nyingine wanayoitengeneza wataanza na tani 12,800,000 lakini wataenda mpaka milioni 43,200,000. Kwa hiyo Tanzania kama tunataka uchumi wetu ukue kwa haraka ni lazima tuwekeze kwenye umeme, tuzalishe uwe mwingi, halafu lazima twende kwenye uchumi wa gesi na huu uchumi una vitu vingi sana na ushauri mwingine ni kwamba kwa sababu kuna viwanda vingi kama hivi nimewaambia umeme, mbolea na viwandani kabla haujampatia mshindani wako gesi yako, nadhani ni busara umpatie bidhaa zinazotokana na gesi kuliko kumpatia gesi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniventure Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza niweze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaendela kuifanya kwa ajili ya Watanzania, lakini pia nimpongeze Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu na taasisi ya *TRA* ambayo inakusanya mapato kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii kwa kweli imetoa mwelekeo kwa wananchi maskini, hasa kwenye vyuo ambavyo ni vyuo vya ufundi kuwa na ada bure. Hili tunakwenda kuongeza wataalam ambao walikuwa wanabaki, wanapochaguliwa na Serikali kwenda kwenye vyuo hivyo wanakosa ada. Kwa hiyo, hapo tumekwenda kumgausa mwananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye vyuo vya kati vya sayansi afya na mambo mengine, kutoa mkopo ambao W abunge hawa mmeridhia miaka yote ili hawa wanafunzi waweze kupata mikopo na wao waweze kusoma kwa sababu wengi walikuwa wanabaki. Napongeza sana na ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Rais kwa kukubaliana na jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nilimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alisema tozo siyo za Rais, tozo siyo za Waziri Mwigulu na mimi nakubaliana na yeye, tozo ni za Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Kama kuna tozo vikwazo ni nafasi yetu sisi Bunge kuziondoa tozo hizo vikwazo, kuliko kumuachia mzigo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kushauri hapa ili angalau tuone ni namna gani hawa wafanyabiashara wanaweza kukwepa kodi kwa sababu ya tozo vikwazo na naomba nianzie na *service levy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa *service levy* uliwekwa kwa ajili ya viwanda wanapozalisha wanatozwa *service levy* kwa ajili ya Halmashauri zetu. Lakini msingi wake ulitokana na kwamba ili hii *service levy* itozwe ni kwamba Halmashauri zetu baada ya kuangalia mauzo ambayo yanauzwa kwenye Wilaya zetu, yanapeleka moja kwa moja viwandani, viwanda vinalipa. Naomba nitoe mfano, pale Ilemela Kiwanda cha Bia *service levy*

Halmashauri ya Ilemela inatoza moja kwa moja pale, lakini hata yule *agent* ambaye kiwanda kinamuuzia kwenda pale pale mita 100, na yeye akiuza Halmashauri inamtoza kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bidhaa hizi zote ukiangalia kwa mfano tu nataka nitoe mfano, *bundle* moja ya bati mfanyabiashara ananunua shilingi 370,000 ukimtioza 0.3% sawa sawa na shilingi 1,100 lakini huyu anapata shilingi 1,400. Je, atakuwa tayari kutoa risiti? Ndio maana sasa unakuta wafanyabiashara hawatoi risiti kwa sababu wakitoa risiti, *service levy* inakwenda kuwa nyingi kuliko faida ambayo anapata mfanyabiashara. Kwa hiyo, hapa tunakwenda moja kwa moja kupunguza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *service levy* mwanzo msingi wake ilikuwa ni *income,* lakini leo wanatoza kwa *revenue*. *Income* maana yake ni kwamba umeshatoa matumizi yote na gharama zote, kinachobaki ndicho kinachopaswa kutozwa, lakini wao sivyo, kwa hiyo, ndiyo maana sasa tunakwenda wafanyabiashara wanakwepa kutoa risiti kwa sababu ya vikwazo hivyo na hilo wanajifanya sasa wafanyabiashara kuandamana kwenye mambo haya. Sasa lawama zinamrudia Mheshimiwa Rais, zinamrudia Waziri wa Fedha lawama, kumbe vikwazo hivi inapaswa tukae chini tuangalie je, tutoze kwa *revenue?* Je, tutoze kwa *income* au tupunguze badala ya 0.3% tuwe na 0.03% hapo ndipo sasa risiti zote zitatolewa, nilitaka kushauri hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi 100 ambayo imeongezwa kwenye mafuta kwanza niwatoe hofu Watanzania na niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, nataka tu kutoa mfano, lori likipakia lita 1,000 kule Dar es Salaam kubeba mzigo kwenda Mwanza inayoongezeka ni shilingi 100,000 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hiyo unaweza ukasema kwamba inaweza kupunguza gharama za uendeshaji au kuongeza gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba kwa sababu soko la dunia la mafuta hatuna uwezo nalo, kuna kushuka na kuna kupanda kodi hii inakwenda kutusaidia kwenye miradi ya kimkakati hasa kwenye kilimo

ambapo kwa kweli Watanzania wengi wapo kwa sababu tunaweza kutengeneza hofu, lakini tukashindwa kutengeneza huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naendelea kusema kule Magu mahindi yanakauka kwa sababu ya kukosa maji. Kwa hiyo, hii shilingi 100 pamoja na kwenda kwenye miradi ya kimkakati hasa reli ya *Standard Gauge* lakini pia lazima iende kwenye kilimo kwa ajili ya umwagiliaji ili wananchi wetu waweze kupata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika kidogo na ninashangaa sana sijui wataalam hawa Waziri wa Fedha wanakushauri vizuri? Leo Serikali imetoa ruzuku ya mbolea, Serikali imetoa ruzuku ya mbegu, watu wamelima vya kutosha, alizeti Mwanza, Simiyu, Tabora, Singida, Mbeya na Iringa na maeneo mengine Babati imelimwa ya kutosha; pamba ipo ya kutosha, mikoa 17 inayolima pamba. Kwa hiyo, tuna uhakika wa kuwa na mafuta mengi ya kutosha kwenye nchi hii, kwa hiyo, unapokwenda kutoa kodi kwa mafuta yanayotoka nje unaweka 25% badala ya 35% unakwenda kuwafanya wakulima wa nchi hii kwa masikini, siyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili siyo sawa, halafu unakwenda kuongeza 18% *VAT* kwenye mafuta yanayozalishwa nchini unatoa ya nje, kwa kweli hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha hawakukushauri vizuri. *(Makofi)*

Naomba nishauri Serikali, hatuwezi kuongeza ajira ya wakulima wetu, hatuwezi kuongeza ajira kujenga viwanda kama kodi za mafuta yanayotoka nje tunazipunguza. Napendekeza 35% ya mafuta yanayotoka nje iwekwe ili kuhakikisha kwamba wakulima wetu wa alizeti wanapata bei nzuri, wakulima wetu wa pamba wanapata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tukatajirisha nje, tukawaweka wananchi wetu kuwa maskini, hili haliwezekani. Nishauri sana, naunga mkono lakini kwenye hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha nitashika shilingi. Kama 35% haitawekwa, kama *VAT* haitaondolewa kwenye mafuta ya ndani, hili nitashika shilingi kwa sababu tunakwenda kuwatia umaskini wananchi na hivi viwanda

vinamilikiwa 80% na Watanzania. Leo ukiruhusu hiyo 25% maana yake viwanda vyetu vinakwenda kufa. Hili siyo sawa, niombe sana kwa kweli Waziri wa Fedha unafanya kazi vizuri, lakini katika hili niombe kwa kweli lazima tulinde wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuja kwenye ngano; ngano tunalima, kule Njombe wanalima, kule Katavi wanalima, kule Arusha, Babati wanalima, lakini mapendekezo ya wataalam wako Mheshimiwa Waziri yanasema unaondoa 35% unaweka 10%. Sasa hawa Watanzania wanalima ngano ya nini? Kwa sababu ukipunguza tu kodi ya ngano nje maana yake kwamba unamfanya mkulima wa Tanzania asiendelee kulima. Sasa hapa tunakuza uchumi? Hapa tunakuza uchumi au tunakuza mapato? Haiwezekani, lazima tuwe tayari, tumetoa mbegu za ngano, tumetoa ruzuku kila mahali, kwa hiyo lazima tulinde wakulima wetu na tulinde biashara ya Tanzania na niombe sana hapa, kama tuna mazao ambayo ni ya kimkakati ambayo yanaweza kwenda kuinua uchumi na kupunguza fedha za kigeni kwenda nje lazima tuyalinde kwa wivu, tusiyaachie hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili Bunge ndilo ambalo linaweza kutengeneza mwelekeo wa uchumi kwa nchi hii. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri mimi nataka uwe na uwezo wa kukusanya fedha ili heshima ya nchi iwepo ni mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapokwenda kupunguza kodi, tunapunguza mapato. Ili heshima ya familia iwepo ni mapato kwenye familia. Familia ukikosa baba wa familia hela hauna heshima. Kwa hiyo, tunapokwenda kupunguza mapato kwa sababu ya vitu kutoka nje tunakwenda kupunguza heshima ya nchi. Lazima tujitegemee, tutaendelea kukulaumu, tutaendelea kumlaumu Mheshimiwa Rais, lakini lazima tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest* mimi ni Mwenyekiti wa Wachambuaji wa Pamba Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019 Serikali ilisema wanunuzi wa pamba wanunue pamba kwa bei yoyote itafidia. Bunge lako limeshatoa azimio na hawa wafanyabiashara 100% ni Watanzania. Leo benki *interest* zinaendelea kuwa *cruel.* Niombe kwa sababu ni Azimio la Bunge na fedha tunaamini zipo, Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuweza kulipa ili kuwawezesha hawa wafanyabiashara na kuwezesha viwanda viweze kuendelea. Hatuwezi kulipa madeni ya nje tushindwe kulipa madeni ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza atafutatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia bajeti ya Serikali. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyosimamia vizuri uchumi wa Tanzania katika hiki kipindi kigumu ambacho dunia na nchi zote sasa hivi zinapambana na hali mbaya ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nchi yetu ukilinganisha yale malengo ambayo tulijiwekea wenyewe lakini ni malengo ya *millennium (MDGs)* tumefanya vizuri sana. Hongera sana Mheshimiwa Rais, lakini hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu wewe ndiyo uko mstari wa mbele kuhakikisha ya kwamba haya yanayotokea yanatokea kwa manufaa ya Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukuaji wa pato la Taifa nchi yetu ilikua kwa 4.7% ukilinganisha na nchi za Jangwa la Sahara 3.9%. Kwa hiyo, Tanzania imefanya vizuri kuliko nchi zingine ambazo zilikuwa na wastani wa 3.9%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile *exchange rate* ya kwetu kwa muda mrefu imekuwa himilivu ukilinganisha na wenzetu na kwa nini inabidi Mheshimiwa Waziri wa Fedha aiangalie sana hii *exchange rate* isije ikatuyumbisha kwa sababu ukiliangalia nakisi yetu ya bajeti nyingi ni fedha za kigeni. Kwa hiyo, tukiyumba kwenye fedha ya kubadilishia ya shilingi yetu ina maana uchumi wetu utayumba na hii hata *inflation* tunayoisema sasa hivi ya 3.4% hatutaimudu tena.

Kwa hiyo, tunakushukuru sana kwa hatua tuliyofikia mpaka leo ya kwamba tumeendelea kufanya vizuri, lakini hata ukija kwenye fedha za kigeni bado nchi yetu imefanya vizuri zaidi pamoja na kuongezeka kwa nakisi ya malipo, bado nchi yetu inaonesha kuwa tunaweza kuagiza bidhaa nje kwa miezi zaidi ya minne ukilinganisha na miezi sita ambayo ilikuwepo mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kujirekebisha katika hali hii nilikuwa napendekeza Serikali iangalie vigezo ambavyo vinatufanya sisi tuwe washindani ukilinganisha na nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ndiyo inayotuletea fedha za kigeni. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Benki Kuu itaanza kununua dhahabu kama sehemu ya kuwekeza fedha za kigeni na hii ni hatua muhimu, kwa sababu Benki Kuu itanunua dhahabu kwa kutumia shilingi, lakini dhahabu itakayonunuliwa ni sawa na fedha za kigeni. Ombi langu ni kwamba Serikali iangalie jinsi ya kuwalipa hawa hasa wachimbaji wadogo bei ambayo ni nzuri ukilinganisha na wanunuzi wengine. Kwa hiyo, kila wakati Serikali iwe *flexible* kuwa itakachowalipa hawa wachimbaji wadogo wadogo bei yao iwe nzuri zaidi ili tuweze kukusanya dhahabu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake kwa sababu katika hii dunia ya ushindani bila ubunifu unaweza kwenda na maji. Juzi mimi nilikuwa shuhuda wa Serikali ilikuwa inasaini mikataba ya ujenzi wa barabara kwa njia ya *EPC+F (Engineering, Procurement* na *Construction + Finance);* huu ni ubunifu mkubwa mno. Sijawahi kuona ujenzi wa barabara kilometa zaidi ya 2,000 na mkataba wa

shilingi trilioni 3.7 ambayo ni mbadala wa tulivyozoea ku-*finance* ujenzi wa miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikiri kabisa inawezekana tulichelewa kufanya mifumo ya aina hii ya utekelezaji wa miradi yetu na nina imani kwa sababu mikataba imeshasainiwa, imani ya kwangu ni kwamba hizi kilometa zaidi ya 2,000 zitakamilika ndani ya muda mfupi. Serikali hapo haitaingiza tena mfukoni kwake kwa ajili ya kulipa ujenzi wa hizo barabara mpaka mradi utakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengi wanaweza kuwa wanajiuliza itakuwaje wakishamaliza? Kinachotakiwa hapa ni jinsi ya kufanya *management* ya ukwasi wa Serikali yetu. Kwa hiyo, *planning* ni muhimu kuhakikisha kuwa itakapoiva hii mikataba tuweze kuwalipa ili tuendelee hata katika miradi mingine. Ninashukuru vilevile katika hizi barabara, imo barabara ya *TANZAM* kuanzia Igawa mpaka Tunduma ambayo itakuwa ya njia nne na hii siyo barabara kwa ajili ya Tanzania peke yake, ni barabara pamoja na majirani zetu wa nchi za *SADC* ikiwemo *DRC Congo,* Zambia, Malawi, Zimbabwe lakini mpaka Afrika Kusini na hii ndiyo inabeba uchumi wa Tanzania kwa *Dar es Salaam Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hii *EPC+ Finance,* lakini Serikali imeonesha kuwa sasa hivi miradi mingi tutakwenda kwa mfumo wa *PPP*. Kwa muda mrefu Mradi wa *PPP* ilitakiwa uanze lakini ilichelewa kutokana na sheria yetu ilikuwa siyo rafiki kwa wawekezaji. Bunge lako mwezi huu limeshapitisha marekebisho ya hiyo sheria na kutokana na hayo marekebisho, itaanza na ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro ambayo itakuwa ni *express highway* lakini baadae itakuja Morogoro mpaka Dodoma na itakuja na *ring road* au barabara ya mzunguko hapa Dodoma na nina imani vilevile itaenda kwenye ujenzi wa reli ya Kusini Mtwara – Mbamba Bay, lakini na barabara ya Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mfumo wa *PPP* ndiyo mifumo inayotakiwa sasa hivi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu kwa sababu *risk* yote ya miradi unaihamishia kwa sekta binafsi ikiwemo na *EPC* ni kwamba *risk* zote unakuwa

umezihamishia kwa watu binafsi, kwa hiyo, Serikali kinachotakiwa ni kuisimamia na kuhakikisha kuwa kile tulichokubaliana kinaenda sawia, lakini vilevile na ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kutokana na maboresho ya bandari ambayo yanafanyika sasa hivi, nina imani kuwa fedha za kigeni zitakuja za kutosha kwa ajili ya kuhimili madeni haya yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninachoomba Serikali pamoja na hayo maboresho kutakuwa na ongezeko la mizigo, tuhakikishe tunakamilisha *SGR* kwa muda mfupi, lakini tukamilishe vilevile reli ya *TAZARA* ni muhimu kwa ajili ya biashara ya bandari yetu kwa sababu hiyo mizigo asilimia 70 yote haitakuwa bora yaanze kupita tena kwenye *expressway,* tupitishe kwenye reli ambayo itatufanya gharama za usafirishaji za kwetu ziwe za chini ukilinganisha na nchi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupambana na hali hii ya uchumi, naiomba Serikali iangalie zaidi na iweke kipaumbele cha kwanza kuhakikisha inaboresha biashara ya madini. Madini ndiyo yanayotuletea fedha zetu za kigeni kwa sasa hivi. Nimeona juzi nampongeza tena Mheshimiwa Rais ameidhinisha kulipa fidia ya wananchi wa Liganga walipwe zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kufufua ule mradi mkubwa. Ule mradi utailetea Tanzania *FDI* zaidi ya shilingi bilioni tatu ambayo ni fedha nyingi sana. Ajira zaidi ya 30,000 lakini utakapochimba chuma na haya makaa ya mawe naomba haya yachakatwe hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naiomba Wizara ya Madini Serikali iharakishe vilevile machimbo ya madini ya *niobium* kule Mbeya kwa sababu yale ndiyo utakuwa mgodi wa kwanza Afrika na mgodi wa tatu duniani na madini ya *niobium* ni kwa ajili ya kutengeneza kifaa kinaitwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia Mheshimiwa.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, madini ya *niobium* ni kwa ajili ya kutengeneza chuma kinaitwa *ferroniobium* ambacho kinahitajika sana kwenye ujenzi wa madaraja pamoja na reli zetu, lakini vilevile naiomba Serikali tunaporekebisha hiyo miundombinu vilevile na barabara ambazo zinalisha hizi barabara kuu kama barabara ya Mbalizi – Shigamba nayo ipewe kipaumbele, barabara ya Isyonje – Kikondwe ipewe kipaumbele, barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Makongorosi ipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao hawakupata nafasi ya kuingia wakati tukitangaza wageni wengine.

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na hawa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Busokelo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 75 wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 153 na walimu 12 wa Shule ya Msingi *Bridge* kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 110 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Kampasi ya Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Charles John Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kujadili au kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024; lakini na Mpango wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa mwaka 2023/2024 dhima yake ni kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha sekta za kiuzalishaji ili kuboresha maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini na mpishi mwenyewe Waziri wa Fedha. Hii kauli ya kuboresha maisha nimeipenda sana. Kama unaita majina, Mheshimiwa Mwigulu kama uliita jina wewe hili unajua kuita majina, tunataka kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa kama tulivyoisikia na katika maandishi, utekelezaji wake ni mzuri na ni wa kiwango cha juu, ni kutokana na taarifa lakini ni kutokana na kule tunakoishi nchi nzima, uraiani kwetu, mikoani kwetu, utendaji unaonekana.

Mheshimiwa Spika, ziko dalili wazi; miradi ya umeme vijijini inaendelea, ujenzi wa mashule ikiwemo vyuo vya *VETA,* ninapozungumza *VETA* Kijiji cha Bushagara, *VETA* inajengwa inaendelea, lakini jitihada za Serikali za kuweka pesa katika mabenki *TIB* ili kuwaongezea watu ukwasi na kuweza kukopa. Lakini jitihada za Serikali katika miradi ya maji, tulikuwa na miradi ya maji 586, kipindi tulichomaliza, nimeiona kwa macho yangu katika Jimbo langu, nimeiona popote napopita Tanzania katika kamati ulizotutuma, lakini mpango wa Serikali wa kutengeneza miradi 1,293 mimi inanituma bila wasiwasi kuunga mkono bajeti hii ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuisahau *TARURA* niipongeze Serikali kwa mpango wake wa kutenga pesa zaidi kwa idara hii ya

*TARURA,* ili tuweze kutengeneza barabara ziweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, linazungumzwa suala la uchumi wa dunia, wanazungumza uchumi wa dunia na kiashiria rahisi cha uchumi wa dunia ni takwimu. Mimi ningependa niwaeleze Watanzania na Wabunge wenzangu viashiria rahisi vya kujua uchumi wa dunia ni mzuri, lakini sisi kiongozi wetu na wasaidizi wake akiwemo Waziri wa Fedha, tumeweza kuudhibiti uchumi. Wakati kuna nchi sio za kutafuta, ndege zilishindwa kuruka, magari yalishindwa kutembea kwa kukosa mafuta, tatizo hili hapa kwetu halikutokea. Wakati kuna nchi watu walilala njaa, Serikali kabisa viongozi wakuu walihangaika wakitafuta chakula sisi hapa hatukukosa chakula. Yupo rafiki yangu aliwahi kuniuliza unamfahamu Waziri wa Kilimo, nikasema yule ni mtumishi mwenzangu akasema kamshukuru. Nilikuwa na shida na njaa kwetu nikamwambia akaandika karatasi *NRFA* wakapeleka chakula, sisi hatukulalamika na chakula. Kwa hiyo, Serikali imeudhibiti uchumi huu wa dunia kwa tafsiri ya kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtanzania yeyote ajipime kwa hilo ulikuwa kwenye kituo cha mafuta ukakosa mafuta, haikutokea, lakini kuna nchi zimekosa mafuta, zimekosa chakula. Watu wamekuwa na *black out,* umeme umeshindwa kuwaka wakataka *black out,* lakini Tanzania hatukuweza kuingia katika hilo. Baya zaidi kuna nchi katika bajeti zao walisimamisha bajeti za maendeleo, yaani Serikali imetengeneza bajeti mwaka jana kwamba maendeleo yasitekelezwe, lakini Tanzania hakuna mradi uliosimama. Kama anavyosema Mheshimiwa Rais hakuna kilichosimama na kweli hakuna kilichosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze Serikali na Mheshimiwa Waziri umeweka msingi wa bajeti ambao ni kazi kubwa na kazi lazima ifanyike. Msingi mmoja wa bajeti unasema kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, ili bajeti yetu iweze kufanikiwa ni lazima kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi. Mimi nina ushauri wa mambo mawili. Tunapoizungumzia sekta binafsi tusiangalie wakubwa tu, hata hawa wadogo wanaolima kilo mbili za

maharage, wanaolima mahindi na wao twende nao. Sekta binafsi ni mzalishaji yoyote, tusikimbilie wale wakubwa. Suala la pili ninaloomba unapozungumza sekta binafsi kuna sekta binafsi ya Tanzania na sekta binafsi ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, nimshauri Mheshimiwa Waziri lazima sekta binafsi ya Kitanzania tuifikirie. Tungependa watoto wetu tuwaweke katika shughuli kusudi wasije kuwa watazamaji kwenye mchezo ambao waliuanzisha wao. Niipongeze Serikali hasa Mheshimiwa Waziri, umezungumzia juu ya mamlaka za udhibiti, ukazungumzia na *TRA*, lazima kama tunaitegemea sekta bonafsi basi mamlaka za udhibiti zifanye mazingira ya kufanya shughuli yawe mazuri, wasiwe kikwazo. Siwezi kuongezea zaidi namna ya kutekeleza hii, ni kutembea na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, lakini ni kutembea na maneno yako ambayo uliyatoa kwa maneno yanayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Tume ya Mipango, tuliomba Tume ya Mipango, Wabunge tumezungumza Tume ya Mipango, hatimaye Tume ya Mipango iko kazini.

Ombi la kwanza Serikali, mamlaka Tume ya Mipango muwape majukumu lakini muwape mamlaka na wawajibike kwayo *(authority, responsibility and accountability)*. Tungependa Tume ya Mipango ituongoze, tunatengeneza dira lakini dira bila Tume ya Mipango haiwezi kufika mahali popote. Unaweza ukawa na mali nyingi, ukakusanya rasilimali nyingi ukazitumia, lakini ukazitumia bila mpango. Sipendi kuzungumza mengi zaidi tuna imani na Tume ya Mipango, lakini Tume ya Mipango iwe wazi ili kusudi watu waweze kutoa mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie dhima ya mwaka wa fedha ujao inayosisitiza kuimarisha sekta za uzalishaji ili kuboresha maisha. Hili neno kuboresha maisha kuna ndugu yangu mmoja anaishi Songwe huko analipenda na mimi nimelipenda zaidi naona Mheshimiwa Waziri ameiga kwako, tuboreshe maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu urari wa biashara ya bidhaa na huduma, katika urali wa biashara wa

bidhaa na huduma mwaka huu tunaomaliza tumepata hasi bilioni 3.87, bidhaa na huduma, lakini urari wa biashara na bidhaa tumepata nakisi ya bilioni 6.066, urari wa biashara ya huduma tumepata chanya bilioni 2.199 maana yake nini, tumeokolewa na utalii na sekta za huduma.

Kwa hiyo, kwa kuanzia lazima tuwekeze nguvu nyingi kwenye utalii, lakini hizi sekta za kiuzalishaji tulizozungumza lazima tuwekeze katika sekta za uzalishaji kusudi tuuze zaidi. Maana yake nini? Tuingie kwenye *import substitution come export promotion,* tuingize pesa zaidi kwa kutoka nje ndio tuweze kuhimili kutekeleza bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naona umeniwashia taa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Daktari Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumza zaidi kwenye kilimo; tunafahamu sote kwamba tulikuwa na *slogan* kama Taifa kwamba kilimo ni uti wa mgongo na bado hata kama hatutaji lakini kiekweli kilimo ndio kinashiikilia maisha ya Watanzania nusu walioko hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu kilimo cha kizamani cha kutegemea mvua au kutumia akili za babu zetu kimepitwa na wakati. Tunahitaji kuwa na kilimo cha kitafiti. Kule Mbeya tuna Chuo cha Kilimo Uyole takribani zaidi ya miaka minne, mitano walikuwa hawajapata fedha kwa ajili ya utafiti na sisi tunaamini katika utafiti.

Mheshimiwa Waziri ni lazima tuwekeze katika elimu kwa watafiti wetu ambao wamekwishakusoma ili kuweza kuwasaidia wakulima wetu. Ninaomba sana sana Wizara yako Mheshimiwa

Waziri imeweze kutoa fedha kwa wakati hasa pale Uyole, lakini tukienda *SUA* wanahitaji kupata fedha tuweze kufahamu namna gani kama udongo unafaa, tunafahamu tunahitaji mitamba mizuri, tunahitaji wawe na fedha ili wafanye utafiti. Mheshimiwa Waziri kwa hilo naomba uwekeze sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia utafiti huo huo leo hii tuna kilimo cha parachichi. Kilimo hiki kimeleta watu wengi sana toka nje ya nchi sitataja kwa ajili ya mambo ya kidiplomasia, lakini mwisho wa siku kwenye mashamba, vijijini unakutana na wateja ambao wanakuja kununua parachichi hizi. Hicho ni kitu kizuri mimi sikatai, lakini mwisho wa siku tunapata kiasi gani fedha za kigeni kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inasimamia hawa wateja wanaokuja, wanatenda haki kwa wakulima wetu? Tumekuwa na tabia mbaya sana ambayo inafanywa na wanunuzi hawa, wananunua parachichi halafu wanaziita *reject,* ni nani anasimamia kama kweli hizi ni *reject?* Kwa sababu babu anayelima parachichi kijijini kule Rungwe na sehemu zingine za Njombe hawezi kujua kama hii ni *reject* au siyo *reject,* kwa sababu yeye kama mnunuzi anaamua kusema hii ni *reject* na utakuta hiyo *reject* ni kubwa kuliko yale mazuri na anaondoka na ile *reject* Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana sana usimamizi kwa wakulima wa parachichi, tunaona kuna madalali wengi sana hapo katikati, tunaomba msimamie kama Serikali. Mwisho wa siku kazi hii ni ngumu ambayo mwananchi wa kawaida amejiwekeza, amelima, ametaka kupata faida na familia yake anakuja dalali anakubaliana na mnunuzi kihuni na mwisho wa siku watu wetu hawapati haki anayostahili kuipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tunajua kabisa tunasema parachichi ni dhahabu ya kijani, tunafahamu kabisa kule kwetu tulipotoka, tumetoka katika mia zote parachichi kumi kwa shilingi 1,000 sasa hivi angalau zimeongezeka bei, lakini bado Wizara ya Fedha mtusaidie…

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, hawa watu wanapokwenda kuagiza parachichi…

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia ulipaswa uendelee kuongea nilitaka umalize sentensi yako. Maadam umekaa ngoja upokee basi taarifa manake unao huo utayari, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi naomba kumpa taarifa mzungumzaji dada yangu Sophia kwamba kwa muktadha huo kama Taifa maana na mimi natoka tunakolima parachichi, tunahitaji kuwa na kitu kama bodi kwa ajili ya ku-*regulate* zao hili la parachichi. Bodi ya Parachichi kama ambavyo tuna bodi katika mazao mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda unapokea taarifa hiyo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa hii kwa mikono miwili na naiongezea Mheshimiwa Waziri uichukue hiyo taarifa ya Mheshimiwa Chumi na kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa kwamba parachichi tumesema ni dhahabu ya kijani, inawapatia wananchi wetu fedha, lakini kumekuwa kuna tozo nyingi ambazo hazina maana kwa mkulima wa kawaida. Ni lazima Halmashauri zetu ijapokuwa sisi Wabunge ni Madiwani katika Halmashauri zetu, lakini tuwe tuna *uniform* moja ya utozaji wa parachichi. Ukienda Njombe wana aina yao ya utozaji, ukienda Rungwe hivyo hivyo. Tunataka sasa na ndio maana ya bodi sasa ikiwepo inaweza ikatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii wale wanaobeba zile parachichi wenye magari yale ya *cooling system* yale wanasimamishwa kila mahali, kila wakati na tozo nyingi sana. Mwisho wa siku

tutakimbiwa na hawa wanunuzi na wakulima wetu watalima tutarudi kule kwenye mia zote tunakuwa hatujafanya sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, sana, sana, Mheshimiwa Waziri ninarudia tena kusisitiza suala la *reject* ninaomba Halmashauri uziambie zisimamie watu wetu waweze kupata haki yao, mambo ya *reject* iwe kweli, mtu wa Serikali pale halmashauri amtetee mkulima ili kujua kama kweli kaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuja kwenye suala la chai, ninafahamu Mheshimiwa Bashe ulikuwa na kikao kwa ajili ya kuhakikisha tunakuwa na mnada kwa ajili ya chai. Pia tunahitaji maabara, lakini mwisho wa siku tunataka tufenye zao la chai liwe la thamani zaidi. Chai inanyweka nchini, chai inanyweka dunia nzima. Leo hii kuna nchi za Ulaya zinanunua sana chai, tunaomba tuwekeze zaidi. Wenzetu wa nchi za jirani, mkulima wa chai ni tajiri lakini leo mkulima wa chai kwenye mikoa yetu hata kumiliki baiskeli ni kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi kama Taifa tunahitaji tuwatetee watu wetu, ninafahamu juhudi za Waziri wa Kilimo anazozifanya kwa zao la chai, lakini bado tunahitaji kuongeza nguvu, tunahitaji kuwa na mnada wa chai ambao mlituahidi kama utakuwepo labda unaweza ukatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kuzungumzia suala la kahawa. Tunafahamu kahawa baada ya petroli duniani kunyweka, kahawa inatumia sana sana sana na wananchi dunia nzima. Tunaomba kahawa ruzuku iwepo kwa wakulima wa kahawa pia tozo ndogo ndogo kwa wanao-*export* kahawa zipungue ili tuwe sawa na wenzetu wa nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, tunapoingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tunahitaji kuwa na uwiano sawa hata tunapoingia kwenye mambo ya ushindani tusiwe tunakabwa sana sisi kwa kodi nyingi kuliko wenzetu ambao wako mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la vanilla Mheshimiwa Waziri; vanilla ni zao zuri lakini limeleta utapeli mwingi sana katika Taifa hili. Sote

tunafahamu na tunalalamika katika Bunge hili. Wanakuja kuelezea vanilla inauzwa milioni moja, mkulima analima vanilla halafu mwisho wa siku inauzwa shilingi 25,000 hadi 30,000. Naomba msimamie hawa watu wanaojiita wao ndio viongozi wa vanilla wanaposema uongo Serikali iweze kupambana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara za vijijini. Leo hii *TARURA* tunaomba muiongezee fedha na hasa maeneo ya milimani yenye Nyanda za Juu Kusini kule kwetu Mbeya kwa mfano, fedha huwezi kumpa sawa na mtu ambaye anatoka sehemu ambayo hakuna milima. Tunafahamu maeneo ya kwetu Mheshimiwa Waziri yana mvua za mwaka mzima *almost,* barabara zinaharibika zaidi na kwetu ndio tunalima zaidi na tunalisha Taifa hili. Tunaomba *TARURA* walioko Nyanda za Juu Kusini kote waongezewe fedha kwa kuwa barabara zao zina changamoto nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka kwenye barabara niende kwenye *TAZARA*. Mheshimiwa Waziri *TAZARA* ni reli ambayo inasaidia sana hasa watu wa Nyanda za Juu Kusini. Tunafahamu mazao yetu hata bila ya kupitia kwenye malori wakati mwingine tunatumia treni ya *TAZARA,* lakini bado Sheria ya *TAZARA* inatubana. Tunafahamu kwamba ilianzishwa kwa Zambia na Tanzania, lakini tunaona wenzetu kidogo kama wanaenda wanasuasua. Tunaomba muweze kuibadilisha *TAZARA* ikibidi ipate wawekezaji kwa kupitia Tanzania na nchi yetu iweze kunufaika kwa sababu bado sisi tunauhitaji sana na reli hii. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri tuisimamie kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie fedha za mikopo ya wanawake. Ninafahamu nia njema ya Serikali ya kusema sasa fedha zipite kwenye mabenki, lakini bado ninalo swali. Kule kwetu vijijini maana watu wengi wanaamini benki inakuwa na utaratibu wake, ili upate mkopo benki lazima uwe na *document,* uwe umesoma na ujaziwe na vitu viko kisomi. Je, mtaweka utaratibu wa kibenki kwa maana ya kupitisha fedha lakini mfumo ule ule wa upatikanaji wa vikundi au mtafanyaje?

Mheshimiwa Spika, si tu hivyo bado tunaomba mfanye haraka kwa sababu mnavyochelewa kuleta majibu haraka kuna wanawake walikuwa wameshakopa ambao tayari wana mikopo hiyo pia wanaendeleza biashara kwa sasa wamesimama hawafanyi kitu chochote. Tunaomba Serikali ije kwa haraka sana iweze kuwarudishia hizo fedha kama mfumo wa benki, lakini uwe kwa haraka na waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nitaunga hoja nikiona kama umekuja na majibu haya ambayo mimi nimeyasema, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kura ya muhimu hiyo ya ndiyo inasubiria. Kura ya ndiyo umeahidiwa hiyo. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii na mimi nianze kwa kutoa pongezi na shukrani nyingi kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na viongozi wake kwenye Wizara hii tusimsahau Gavana wa Benki Kuu kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na kutuonesha kwamba inawezekana mahali popote kufikia au kuendeleza uchumi wa jumla ambao ni tulivu ukiwa na *inflation* iliyo ndogo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema machache kuhusu hii bajeti ambayo nasema ni bajeti nzuri kulinganisha na bajeti nyingine ambazo nimesoma, niseme kidogo kuhusu mambo ya jimboni kwa sababu wananchi wa Vunjo wamesema hawajanisikia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza niseme kwamba nashukuru kwamba Serikali imeweza kuendelea kuipa *TARURA* fedha ya kutosha kiasi na kwa hivyo *TARURA* inakuwa imeendeleza kujenga na kukarabati barabara kule vijijini kwetu.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru kipekee kwamba *TARURA* wamesikia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba waweze kujenga barabara ya Himo sokoni kwenda Makuyuni na Rotima kwa kiwango cha lami, na wameanza kuijenga lakini nawakumbusha kwamba Mheshimiwa aliagiza ipate kilometa 7.4 wasije wakaishia mita 800 ambazo naona wanakazana nazo sasa hivi, naamini watafikisha kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tumeweza kuwasilisha kupitia Bodi ya Barabara ya Kilimanjaro, Mwenyekiti wetu amewasilisha maombi kwa Wizara ya Ujenzi waweze kupandisha hadhi barabara tatu; barabara ya kwanza ni ile ya Pofo - Kilema - Mandaka ambayo tayari wanaanza kuiweka lami, lakini kuna Uchira – Kisomachi – Kolarie; na Chekereni - Kahe hadi *TPC* hizo ni barabara ambazo tumeziombea sasa zipandishwe hadhi ziwe ni barabara za kimkoa, kwa hiyo, ziweze kuhudumiwa na *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba sasa kwa sababu kwenye ile bajeti ya Wizara hii zaidi ya shilingi trilioni 3.7 wanaweza pia na sisi tukapata kidogo wakapokea barabara mojawapo na sisi tukapata kidogo. Hatukupata fedha yoyote au mradi wowote kwenye Wizara hii katika bajeti inayokuja.

Kwa upande wa vituo vya afya, tulishukuru pia kwamba Serikali imeweza kutupa Kituo cha *Marangu Head Quarter* ambacho tulipewa shilingi milioni 500 na kama kinakamilika isipokuwa kuna jengo la *maternity* na *theater* ambalo halitaweza kukamilika kwa fedha hizi. Tunaomba TAMISEMI waweze kuona namna gani wataongeza fedha hiyo, siyo nyingi sana itahitajika shilingi milioni 50 tu kuweza kukamilisha hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia kwamba Serikali iweze kutuletea vifaa tiba ili waweze kuanza kazi kwenye kituo hiki ambacho kiko karibu sana na wananchi wengi. Pia tunaomba kituo kile cha Koresa ambacho tumeahidiwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliyekuwepo basi nacho kianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa maji nilizungumza hapa kwamba Mheshimiwa Waziri atakuja, Naibu Waziri atakuja kule ili tuweze kuhakikisha kwamba ile miradi ambayo ipo kwenye Kata zile za Mwika Kusini na Kaskazini, Mamba Kusini na Kaskazini, Marangu Mashariki na Magharibi na Kilema kwamba kazi yenyewe ziwe zinakamilisha kwa sababu ilikuwa iwe mwaka mmoja, lakini sasa imechukua miaka mitatu bado hatujamaliza.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa elimu; tuna shule tatu tu ambazo zimepewa kidato cha tano na sita. Sasa hiyo ni changamoto kwa sababu tuna shule za sekondari ya kawaida ni 32 na ushee, kwa hiyo, tunaomba kwamba sasa na hasa tukizingatia hii mitaala mpya inayoingia na mfumo mpya wa elimu tunaokuja ku–*adopt* basi waanze kupandisha hadhi baadhi ya shule hizi za kawaida hususani shule kwa mfano ile shule ya Mboni, kuna shule ya Kokirie, kuna shule kule Marangu na kadhalika. Tunaomba kwamba sasa tuanze mchakato wa kuainisha ili zianze kupandishwa hadhi kupata kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba nije sasa kwenye upande wa bajeti hii ambayo nimesema ni bajeti ambayo kwa ujumla inavutia kwa sababu gani? Kuna wakati nilisimama hapa mwaka 2022 ile bajeti tulivyokuwa tunapitisha, kwa hivyo, ile bajeti ilikuwa *contractionary* kwamba isiwe bajeti ya kuchochea uchumi, kwa sababu wakati ule kusema ukweli kuwa na nakisi ya bajeti ambayo ina asilimia tatu ya pato la Taifa, ilikuwa hairuhusu ina maana Serikali haikuona kwamba kuna uwezekano wa kukopa zaidi na kwenye soko la ndani wakati ule ambapo hata sekta binafsi ilikuwa haikopi, haihitaji kukopa kwa sababu mazingira yalikuwa hayaruhusu sana kufanya biashara yenye tija.

Kwa hiyo, wakati ule ilikuwa ni wakati ambao ilikuwa inatarajia kwamba Serikali itakuwa na nakisi kubwa zaidi iweze kukopa zaidi na iweze kuchochea uchumi wakati ule *private sector* ikiwa inaogopa *risks* zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini na pia kwa wakati ule naona huko kulikuwa hali hata riba zilikuwa ziko juu, lakini siyo Serikali

hazikuweza kufanya chochote kwa upande ule. Lakini nilisema kwamba ni *contraction* lakini mwaka huu tunaona pia kwamba ni *contraction* kwa sababu nakisi kwa uwezo wa pato la Taifa iko 2.7 lakini wakati ule ni wakati wake kabisa na mimi napongeza hayo maamuzi kwamba tujaribu kupunguza matumizi na ukopaji kwa sababu hatuna uwezo sasa hivi kuna *cons trait* mbili, *cons trait* ya kwanza sasa hivi ndiyo kubwa zaidi ni hii nakisi kwenye malipo ya nje pamoja na upungufu wa dola. Sasa hiyo ndiyo inatubana kwa sababu unaweza ukawa na miradi mikubwa, lakini mwisho wa ukomo wako utaishia kwenye kuomba fedha za kigeni unazo, na kama huna utalazimika kuishia hapo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba hapa wamesema pia wanakopa, wamepunguza maoteo ya kukopa nje kwa masharti ya biashara. Lakini utaona kwamba mimi naamini kwamba tunapoendelea kutekeleza hii bajeti utakuta kwamba tutalazimika kukopa zaidi kwa sababu tukiongeza miradi hii ambayo tunayo hatutaweza kutokulazimika kukopa zaidi nje ili tuweze kupata dola ambazo zitatusaidia kuendeleza hii miradi ambayo yenye uwezo ambayo tunaenda nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi napongeza pia kwamba Serikali pamoja na Benki Kuu wameweza kushikilia kweli sera zao za kifedha na kibajeti na kuhakikisha kwamba uchumi wetu umebakia tulivu, *inflations* ni 4.3 katika mazingira ambayo ni magumu sana. Japokuwa bado naamini kwamba bado riba haziendani na hii *inflation* ndogo ya kiasi hiki ambayo imekaa kwa muda mrefu. Mimi naamini bado riba tuna kazi ya kufanya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia hii ukamilishaji wa tathimini na ukopeshakaji wa nchi yetu; *fitch ratings* wakatupa *B2 plus* na ile watakupa *B+* ambayo ni nzuri *(rate* nzuri sana) kwa nchi ambayo inaendelea kama ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia kwamba hiyo nisiseme, lakini nisemi hivi kuna jambo moja ambalo ninataka nishauri ili kuongeza mapato yetu na kupunguza ruzuku tunazotoa kutokana na mapato madogo, mimi nafikiri kwamba kwamba kwa upande kwa mfano wa mafuta, mafuta yanashuka bei *petrol* na *diesel*

zinashuka bei, mimi nafikiri kwamba tungekuwa na *threshold* tukisema ikizidi 3,000 tutatoa ruzuku, ikishuka chini ya 3,000 tunapata .... tunaingiza kwenye mfuko wa ku–*standardize* bei za mafuta siyo Serikali iingie tena kwenye bajeti yake kutoa ruzuku tutengeneze huo mfuko kutokana na hii *fluctuation's* ikishuka, ikizidi 3,000 tuwape ruzuku, ikishuka tuendelee kuchukua kwa muda kiasi halafu tuone inaendelea kushuka basi tunaji–*adjust* na sisi chini hivyo hivyo, hiyo ndiyo njia pekee ya kuweza kuwa na ruzuku ya mafuta ambayo itasaidia uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba kuna tatizo la takwimu hizi za ukuaji wa uchumi ni ukuaji wetu wa uchumi. Ukiangalia *figure* tulizonazo kwenye bajeti, kitabu cha bajeti uchumi wetu *GDP* ilikuwa kutoka trilioni 169.8 mwaka 2021/2022 ikafika trilioni 188.6 mwaka 2022/2023. Kwa hiyo, ina maana kuna ukweli wa asilimia 11 kwa bei ya miaka husika. Sasa kama ni bei ya miaka husika kama *inflation* ni *four percent* ina maana tofauti ya bei za soko ya mwaka husika na *constant price* inakuwa sana sana ni hiyo ya *inflation* ile unatoa.

Kwa hiyo, inatakiwa iwe kwamba kama ni *11.1 percent* ukitoa hapo *4.3 percent* unabakiwa na *almost 7 percent* ya *real growth* hasa inawezekana kwamba kuna mahali ambapo tuna-*miss* kidogo huo ukuaji na ukiangalia kwa dola, dola ni fedha ambayo haina *inflation, inflation* yake ndogo sana ile sasa hivi ni kubwa, lakini imekuwa pia kuchukua kwa dola tulizonazo, dola zilikuwa ni bilioni 77.6 iliyo pato letu hasa ikapanda mpaka bilioni 85.3 ambayo ni ukuaji wa *eleven; ten percent* kwa maana ya miaka hiyo miwili.

Mheshimiwa Spika, kwa nini iwe kwamba tunapokuja kwenye shilingi ni *4.3 percent* au and *around five percent*? Sasa *five percent* utakuta ni chini sana kutokana na kwamba nchi nyingine *average* ya *East Africa* ni *6.3 percent*.

Kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba tuangalie hizi takwimu zetu na kuna mahali kumejificha kitu hakijulikani na kwa nini nakubali kwamba inawezekana hivyo? Hakuna ambacho tulikuwa tunafanya miaka ile ya nyuma kabla ya mwaka 2019 na ambacho hatufanyi sasa hivi tunafanya tena zaidi, kwa nini sasa

uchumi utasema bado unakuwa kwa asilimia tano? Mimi nafikiri tuangalie kuna kitu ambacho hakiendi sawa sawa na ningemuomba hapa Waziri wa Fedha kupitia Ofisi ya Takwimu aweze kuangalia na kuona atafanya namna gani.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hiyo nilijaribu kwenye swali moja nilitaka kuuliza asubuhi wakati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sekunde 30, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia namuombea kwa Mwenyezi Mungu ambariki na sisi sote pia atubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kazi kubwa unayoifanya ya kusimamia Bunge hili vizuri na kwa kweli sheria uliyoisoma tunaiona matokeo yake. Nasema hayo kwa sababu wakati ule wa Azimio la Bandari kama hapo angekaa mtu ambaye haelewi elewi sheria yawezekana lile azimio lingerudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kuwaomba ndugu zangu wa kule Nyasa maana yake na wenyewe wamekuwa wanasema mama vipi huko, mama vipi huko? Hasa kuna dada mmoja anaitwa Angella Mayi kimsingi Bunge lipo imara na linafanya kazi zake kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi na tunashauriwa kupitia Mtume Paulo kwamba tusiwakwaze wenzetu wanapojaribu kufanya mambo mazuri, ni wajibu wetu

kusaidia na kushauri kwa upole ili jambo liweze kutekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo anaingoza Serikali vizuri humu Bungeni, lakini pamoja na Wabunge wote kama hasa wa CCM kama Mwenyekiti wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nyasa, Tarafa ya Mpepo tunalima kahawa, safari hii malipo ya Stakabadhi Ghalani yale malipo ya awali yamechelewa sana kiasi kwamba yanaweza kuleta athari. Kwa hiyo, niwaombe wanaohusika washughulikie mapema ili kunusuru hali hayo, lakini pia hata kama kutakuwa na haja ya kufanya mabadiliko namna ya mfumo wa kuuza kahawa basi ni vyema wananchi wenyewe washirikishwe kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa waliyofanya, lakini pia hata elimu waliyotupa katika kipindi cha wiki hizi zilizopita imetusaidia sana kufahamu mambo mengi ambayo yanayohusika katika Wizara hii na kwa namna ya pekee nakupongeza kwa ajili ya suala la ulililoliandika katika ukurasa wa kumi kifungu namba 16 kinachohusu watu wenye ulemavu kwa kutenga shilingi bilioni moja itakayoweza kuwasaidia katika kupata vifaa saidizi pamoja na mambo mengine ya mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu wana changamoto nyingi sana, ni mtu mpaka uishi nao ndiyo utazijua. Mtu mwenye ulemavu ni gharama yaani hata kumuhudumia ni gharama. Sasa hivi kuna mwanafunzi kwa mfano yupo pale Chuo cha *IAA*, Arusha anachangamoto kubwa kwa sababu ni mlemavu anayesota kwa matako, anatakiwa atembee karibu mita 500 kwenda darasani, wenzake wambebe na wenyewe hawapendwi kubebwa, wanapenda kujitegemea, wanapenda utu wao, wanashida.

Ushauri wangu ni kwamba pamoja na fungu hili uone ni namna gani linaweza kutumika katika kusaidia hasa vile vyuo ambavyo havijaweka sera rasmi ya kusaidia watu wenye ulemavu, kupata vifaa saidizi na kwa hii na kukabidhisha huyu binti Sayuni yuko pale Arusha, naomba umsaidie apate angalau kibajaji hata kama kitakuwa ni cha shule aweze kukitumia atakapomaliza watatumia wenzake, inakuwa ni changamoto kubwa sana, naongea kwa uchungu mkubwa kama mzazi na kwa uzoefu mkubwa wa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba Serikali inasikiliza, siku zote watu tunafikiria tunasema Wabunge wanaongea tu, wanaongea tu, Serikali ina masikio, masikio ninayoyaona hapa sasa ni jinsi ambavyo Wabunge kwa muda mrefu walikuwa wanazungumzia kusaidia kuchangia wanafunzi wanaosoma katika Vyuo vya Ufundi na Sayansi kwa ujumla.

Nimefurahi kupitia ukurasa namba 29 mnasema kwamba mtaondoa ada/mnachopendekeza kuondoa ada katika vyuo hivi vya *DIT, MUST, ATC* kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawapongeza sana, lakini naomba kuongeza Chuo cha *NIT* hakiko hapa, nacho mkiangalie, sasa hivi tunatengeneza reli, tunafanya mambo ya usafirishaji *(logistics)* chuo hiki ni muhimu sana katika masuala hayo, naomba kama kilisahaulika kiongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ukurasa wa 38 kwenye sensa, matokeo ya sensa tumeyapata na hayo tumeambiwa kwamba idadi za watu zisaidie katika kuhakikisha kuwa mipango ya rasilimali inatumika vizuri. Mimi ninachoomba kuongezea isiwe idadi ya watu tu na umbali wa upatikanaji wa huduma uzingatiwe, ukubwa wa maeneo uzingatiwe, mambo yote tusiende tu kiurahisi rahisi kama yale ambayo tulikuwa tunayasikia pengine haya hapa pateni kumi na tano, kumi na tano ngapi hapana. Tuangalie na mambo mengi ya mapungufu yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo niwashukuru sana pia kwa suala hili la ujenzi wa reli ya Mtwara mpaka Mbamba Bay

ambayo iko kwenye hatua za manunuzi. Tunashukuru sana sisi wa ukanda ule, lakini hata Taifa kwa ujumla reli hii itakuwa na msaada mkubwa sana katika shughuli za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Serikali kwa kusikiliza Wabunge kupitia hoja ambayo niliitoa katika bajeti iliyopita juu ya changamoto ya watu kuhamisha ardhi, gharama kubwa za uhamishaji wa ardhi baada ya kununua. Lakini nimefurahi kupitia ukurasa wa 98 mpaka 99 kifungu (b) Sura 332 ya Sheria ya Kodi inazungumziwa kupunguza kodi hiyo kutoka asilimia 10 mpaka tatu na kwa wale ambao wametunza kumbukumbu zao vizuri asilimia 10 ya yale mauzo ambayo yalifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona hii itasaidia sana kufanya masuala ya kiuwekezaji yaende kiurahisi, lakini kuwa na taarifa sahihi ya wamiliki wa ardhi, ndiyo maana mara ya mwisho nimesikia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi anakilalamika kwamba kuna hati zimeshatengenezwa zaidi ya 2,000 lakini watu hawajachukua, hawajachukua kwa sababu yawezekana hayo majina hayapo sasa hivi, hayahusiki ndiyo maana watu walikuwa hawajaenda kuchukua. Lakini kwa mabadiliko haya ya sheria hii nayaunga mkono sana na napongeza sana na naamini yataleta mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda pia katika suala ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ulitoa *commitment* kipindi kile kuhusiana na kupata fedha maalum au tozo maalum kwa ajili ya kusaidia afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunahangaika kufanya masuala ya kidigitali ya tusaidie katika kufanya shughuli zetu na mifumo ya afya ni vizuri sana ikaongea, unaweza kukuta sehemu nyingine wanadawa sehemu nyingine hawana dawa, unaweza kukuta sehemu nyingine kuna watumishi wengi sehemu nyingine hakuna watumishi wa kutosha, lakini kupitia mifumo hii ya kidigitali tutaweza kupata mambo mengi ambayo yanatuunganisha na kuweza kuboresha katika hizi huduma za afya.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo nazidi kusisitiza eneo la afya ni muhimu sana labda pengine tulichelewa haijaingia katika bajeti hii, lakini ni muhimu ifikie mahali sasa wananchi hawa wapate matibabu yao vizuri, bila shida, mmefanya kazi kubwa sana kujenga vituo vya afya, zahanati na maeneo mbalimbali ambayo yanatoa huduma za kiafya, lakini changamoto ambayo imebakia ni hiyo ya kuimarisha huduma za msingi pamoja na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, wengine mpaka wanasema kwamba tumekosea, tumejenga vituo vya afya vingi sana, lakini ukiwafatilia wanaosema hivyo ni wale wanaoishi mjini ambazo huduma zote zipo. Haiwezekani mama mjamzito alazimike kusafiri kilometa 20 anaenda kupata sehemu ya kujifungulia, huyo mama lazima tu ataamua kubaki na kujifungua nyumbani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakati mwingine tunasema tupunguze vifo vya kinamama na watoto, tupunguze wanawake wengi wakajifungulie katika sehemu za huduma sahihi, lakini wamekuwa hawaendi kwa sababu tu kwamba kule mnakomlazimisha aende hawezi kwenda kutokana na changamoto kubwa za kiusafiri na wakati mwingine inabidi apande pikipiki, yuko barabara labda ina mashimo, anatembea huko mama wa watu anakaribia kujifungua, hatujui kwa sababu tu kwamba nini wengine akina baba mnatuonea huruma tunajua, lakini hamjaonja uchungu wa kujifungua, mngekuwa mmeonja mngejua kwamba hata kutembea kilometa moja wakati uchungu umeshakushika ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Sisi mama zenu tumejitolea sana, yaani tumejitoa kwa hali ya juu kwa kutaka tu kwamba tuwe na watoto na ndiyo tuongeze Taifa na ndiyo maana tunaona kwamba hata sasa hivi Mheshimiwa Rais anapofanya maamuzi yake mengine ni ya uthubutu wa hali ya juu, ni kwa sababu akinamama tumezoea kuthubutu ndiyo maana tunafikia hayo malengo na mafanikio tunayoyafanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwaombe sana, fanya hata kama itabidi kwa miaka miwili tupate hiyo tozo, tuboreshe hivyo vifaa ili kuwe na tiba kamilifu katika maeneo hasa kwa vituo hivi ambavyo tayari tumeishavijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo huo suala la watumishi wa afya jamani hili lisiwe ni suala la kuzungumza sana, tusaidieni, tusaidieni watu wanaotakiwa kutibu wawepo kwenye maeneo ili watu wapate huduma inayostahili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, muda umeisha.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlazwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, namimi nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia bajeti yetu ya Wizara ya Fedha na kama walivyosema wenzangu na mimi nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wetu wa Chama cha Mapinduzi, chama tawala na wazi kabisa ziara zake zinaonesha utofauti mkubwa sana wa chama tawala kilicho madarakani na vyama vya upinzani kwamba anakofika maeneo kuna kero ya maji basi anawaita Mawaziri na viongozi wanatatua kero hizo hilo ni jambo jema na jambo zuri la kuungwa mkono, tunaomba sana viongozo wote na watumishi wote wa Serikali kuhakikisha wanaenda sambamba na maelekezo ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dkt. Natu Mwamba amenisaidia na anaendelea kunisaidia kuhusu barabara yetu ya lami ya Ifakara – Kidatu. Barabara ile iko chini ya Wizara Fedha, amendelea kusaidia kutatua changamoto na mambo yanaenda vizuri na Mheshimiwa Waziri uliniahidi kwamba utatembelea barabara ile

ya lami ili ukaone ule mkeka unavyopendeza pendeza sasa hivi maana yake wanachora ile mistari ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niseme kabisa Mheshimiwa Mwigulu wewe katika kuwasilisha bajeti hatuna mashaka na wewe na ni wazi tu kwamba watozwa ushuru duniani hawajawahi kupendwa, kwa hiyo, kuna watu wengi wanaweza wasipende lakini kazi yako yenyewe hiyo ya kukusanya mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu ni kazi ambayo kwa vyovyote vile huweza kupendwa na watu wote. Mtu akitaka kukupima tu kwa kigezo rahisi ni kwamba tulikuwa na malengo ya kukusanya shilingi trilioni 41.4; ukikusanya shilingi trilioni 41.4 ni sawa sawa na 100% na mpaka unawasilisha bajeti yako ya Wizara yako hii kwa taarifa za Aprili, 2023 umekusanya shilingi trilioni 32.4 ukifanya *multiplication equation* hapo tu utapata ni karibu 78% mmeweza kukusanya mapato yetu, ina maana na bajeti utekelezaji wake ni kama 78%, nawapongeza sana, tunawashukuru sana lakini lazima tuongeze nguvu ya kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *TRA* walipanga kukusanya shilingi trilioni 23 lakini mpaka wanawasilisha walikusanya shilingi trilioni 18.8. Kwa hiyo ni imani yangu kwamba uwekezaji mkubwa unaendelea kufanyika utaongeza mapato katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yako nimejaribu kuipitia pitia ina mambo mengi mazuri na kwa haraka haraka labda niseme kwamba suala la kufanya *inflation* libaki katika *single digit* ni jambo zuri, suala la *VAT* kuanza kufikiria kadirio la *VAT* litaanza kuanzia milioni 200 mpaka milioni 500 ni jambo zuri sana, kuweka kodi na kuongeza kodi katika mashine za kamari ni jambo zuri, lakini haitoshi, ongezeni kodi katika mashine za kamari ili ku-*discourage* vijana wetu kushinda katika mambo haya ya kamari na Serikali itaendelea kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umezungumza katika bajeti yako kuna suala la kuboresha adhabu za *TRA* zisiende moja kwa moja katika mazingira ya kutengeneza rushwa, ni jambo zuri. Tunaomba kuwe na mifumo imara ambayo itawezeshesha kupunguza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyoandika kwenye bajeti yake kuhusu kuwezesha Ofisi ya *CAG* iende zaidi kwenye kuzuia taratibu kuvunjwa, kuliko kwenye kuona makosa na kuyaandika makosa ya Serikali. Tunapongeza kuhusu kupunguza riba kutoka *16.5% to 15%.* Tunaendelea kupongeza kama alivyosema Mbunge aliyetangulia kuhusu hiyo bilioni moja ya vifaa vya walemavu ni jambo zuri sana na Mwalimu Nyerere alishawahi kusema katika Taifa hili makundi ya watu yanayopaswa kutegemea watu wengine ni wazee sana, watoto na walemavu. Kwa hiyo, jambo hili ni zuri sana kwa walemavu wetu na nchi yetu itapata baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumza mchakato wa mikopo ya 10% ya Halmashauri. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ya kusimamisha mchakato ulivyokuwa awali, swali letu la msingi ukija kujumuisha hapa Mheshimiwa Waziri tusaidie, vijana, akinamama huko majimboni na kwenye halmashauri wanasubiri mchakato mpya wa Mheshimiwa Rais alioelekeza kuhusu mikopo ya 10% ya halmashauri utakuja kwa utaratibu gani, na utakuja lini? Kwa sababu sasa hivi wamekaa *dilemma* na wanasubiri na nimeona kwenye hotuba yako umesema kwanza jambo hilo litatolewa majibu, ni vizuri mkaanzisha mapema kwa mfano Ifakara tulishaanzisha kukopesha watu pikipiki, tumesimamisha zoezi hilo linaleta manung'uniko sana.

Mheshimiwa Spika, kilimo; mwaka jana tuliongeza bajeti ya kilimo kwa shilingi bilioni 954; mwaka huu naona Waziri Bashe umempa shilingi bilioni 970; ni mapato makubwa, lakini ushauri katika suala la kilimo na tunashauri safari hii Waziri Bashe watuwahishie mbolea sisi wakulima, mwaka jana nia ilikuwa njema, lakini kwa kweli mbolea ilichelewa kidogo kuna baadhi ya maeneo ikaleta manung'uniko. Tunaomba Wizara ya kilimo itazame Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Morogoro ni ghala la Taifa, Mkoa wa Morogoro hata ukipeleka mradi wa umwagiliaji hauna haja ya kuchimba kisima, vyanzo vya maji vipo.

Kwa hiyo, tunamuomba Waziri wa Kilimo atusaidie kuangalia Mkoa wa Morogoro ni ghala la Taifa na sisi tunaongoza nchi nzima katilka kilimo cha mpunga na miwa ya sukari.

Tunamshukuru Waziri Bashe ametutengenezea kitalu pale Illovo cha mbegu za miwa, nafikiri mbegu hizo zitaenda kwa wananchi na wakulima wa muwa watapata mbegu nzuri kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamuomba Waziri wa Kilimo, Waziri Bashe mpunga safari hii hautakauka kwa sababu hakuna jua la kutosha. Teknolojia ya kulima kwa mpunga kuanika kwenye majamvi ilishapitwa na wakati, Waziri wa Fedha tusaidie kuingiza mashine hizi kwa rahisi zikakaushe mpunga. Mpunga safari hii hautakauka, Ifakara kuna shida ya jua, tunaomba mashine hizi ziende kwa wakati.

Namshukuru sana Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe alinipelekea timu ya watu kuanza mchakatio wa uaratibu wa kununua mpunga kwa Ifakara pale utakaosababisha wakulima kuuza mpunga kwa Serikali kwa bei nzuri kabla ya walanguzi hawajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa kwenye kilimo na ushuru hapa nataka kusema vizuri. Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hapa nasisitiza vizuri sana naomba Mheshimiwa Spika na Mawaziri wawili wa Kilimo na wa Fedha wanisaidie.

Mheshimiwa Spika, kuna kero kubwa sana sasa katika Wilaya za Ulanga, Malinyi na Kilombero kwa maana ya Jimbo la Mlimba, Ifakara, Malinyi na Ulanga kuhusu tozo ya chini ya tani moja. Serikali ya Awamu ya Tano na Mheshimiwa Rais Samia akiwa Makamu wa Rais alizunguka kwenye kampeni akasisitiza tumeondoa tozo ya chini ya tani moja kwa wananchi. Katibu Mkuu wa CCM *Comrade* Chongolo amepita juzi ameulizwa na wananchi Ifakara akasema katazo hilo halijaondolewa, lakini wananchi wanatozwa geti la Idete, wanatozwa geti la Ulanga na mpaka mkaa wanapimiwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri semeni jambo hili, mwakani tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hili jmbo linatia hasira wananchi *message* zao wanazotuma huku ni hatari kabisa, naomba sana mlisemee jambo hili je, limefutwa na kama limefutwa toeni tamko

tumefuta, chini ya tani moja watu wanatozwa. Zamani wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano hakukuwa kuna mambo ya barua na urasimu, kwa nini sasa hivi unarudishwa urasimu mwananchi aje na barua, sijui aje na nini, mbona huko nyuma haikuwepo? Hili jambo linamchafua Mheshimiwa Rais na hapa nimelisema kwa kifupi linachafua kweli kweli, wachukue hatua waseme wamerudisha au wamefuta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nataka kusema kuhusu *TASAF*. *TASAF* mmekuja na mradi mzuri sana wa wazee wetu kujishughulisha kwenye barabara za mitaro. Kila siku Mbunge ukiamka unakutana na suala la *TASAF, TASAF* fedha zao pelekeni. Mtu akichimba mtaro anapata shilingi 3,000 kwa siku mtu, amefanya mitaro miezi mitatu fedha hazijaenda, watu wanalaumu, watu wanalalamika naomba sana Mheshimiwa Waziri tusaidie kupata majibu haya ili nia yako njema ya kuendelea kupunguza kero na tozo kero kwa wananchi iendelee kuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kusisitiza kuhusu madeni, mimi nipo kwenye Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Waziri tunakuomba bajeti yako tutaipitisha hapa vizuri kabisa, tunaomba wakandarasi katika Kamati ya Miundombinu tunaona kuna wakandarasi wa ndani na wa nje wanadai na madeni yenye riba, tunaomba sana myalipe. Kuna kampuni tumekutana nayo Dar es Salaam ya Mtanzania ESTEN inajenga barabara pale akina Mzee Giri, ni Tanzania hajalipwa, kuna kampuni tulikutana nayo ya *CHICO* lipeni makampuni haya ili yaweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kusema kuhusu ukurasa wa 42 alichosema Waziri. Jambo la msingi sana Mheshimiwa Waziri amesema anaomba viongozi wote katika nchi hii kuchukua hatua za haraka kuhusu uzembe wa miradi inayoiua fedha, watu wasisubiri taarifa ya *CAG,* wasisubiri mwenge, wala wasisubiri viongozi wakuu. Hili jambo tunataka tuliunge mkono. Kama tutakuwa tunapeleka fedha na Mheshimiwa Rais anatafuta fedha zinaenda kwenye halmashauri hakuna usimamizi wa kutosha, tunacheka na watu itakuwa hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi, wakuu wa idara na wote wanaodai madeni, iboreshe maslahi ya Madiwani iwape vyanzo vya kutembelea Madiwani wakakague miradi, tuwasikilize Madiwani wetu wanasemaje. Nasema katika Halmashauri ya Ifakara mmeleta pesa kibao pale lakini miradi hohe hahe, anasema *RC,* anasema *DC*, hatuna hata *engineer* wa ujenzi, mama kaleta shilingi bilioni moja hospitali ya Halmashauri, kuna shilingi milioni 500 za Kituo cha Afya Mbasa, kuna shilingi milioni 500 za Kituo cha Afya *Msolla Station,* madarasa 120. Sisi na wenzetu waliopewa pesa hapaeleweki. Kwa hiyo, tutaendelea kusisitiza, atakayekasirika akasirike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWEMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hoja ya bajeti ya Serikali iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kunshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutuwezesha wote kwa pamoja tukawepo hapa mpaka siku ya leo tunajadili mipango yetu na tunaiweka katika tafsiri ya fedha.

Napenda pia nipende kuchukua nafasi hii kuukupongeza wewe kwa kuendesha Bunge hili vizuri. Umekuwa imara na kitu kinachofanya mimi nikuheshimu sana, hauna upendeleo kusema kweli pamoja na ile *tree line whip,* lakini umejitahidi sana kutuweka wote kwa pamoja ili tuweze kutoa mawazo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo mchango wangu nitaulelekeza katika Wizara ya Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kwanza nipende kumshukuru Rais ambaye aliona umuhimu sasa wa kurejesha Wizara hii ambayo kwa miaka

fulani tuliteleza kidogo na sasa hivi ameirudisha upya na anaipa uwezo na tumepata Waziri ambaye anajitahidi kuonesha ni namna gani anaweza kuleta ustawi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya maendeleo ya wanawake, watoto na jinsia ina idara tano; ina idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jinsia na mambo mengine. Mimi nitaongelea mbili; Maendeleo ya Jamii, ukitatazama Wizara hii tunaangalia vitu viwili, watu wanaangalia maendeleo ya jamii na ndio imetoka Wizara hii. Lakini watu wa maendeleo ya jamii kazi yao wale ni walagabishi. Wale wanahamasisha maendeleo katika ngazi za chini ili watu waweze kujiletea maendeleo, lakini mimi nitaongelea kuhusu ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa watu wa ustawi wa jamii ndio wamepewa mamlaka ya kisheria ya kuweza kusimamia ustawi wa jamii ya watu yaani kwa niaba ya Serikali. Wanapaswa wao kufanya kazi ya kuhakikisha nchi pamoja na mipango tuliyonayo tutajenga shule, tutajenga madarasa, tutajenga hospitali, tutajenga barabara, lakini ni lazima malengo yetu ni kuhakikisha kwmaba jamii inastawi na inakaa katika utulivu wa aina fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa hivi inapitia katika mmomonyoko wa maadili. Tunajipanga ili tuweze kurudisha maadili katika mstari. Ili tuweze kufanikiwa Wizara hii inapaswa kupata nguvu ya kibajeti ili iweze kufanya kazi yake, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliandaa vyuo vya ustawi wa jamii, ikasomesha wataalam ambao kazi yao wanatoa ushauri nasaha na siyo kila mtu anaweza kufanya hiyo, wako wataalamu ambao wanaandaliwa na nchi kupitia vyuo vya ustawi wa jamii ili waweze kusaidia watu. Tunaangalia akili sijui zimekuwaje wanasema akili na zenyewe zimepotea potea, watu wanafanya mambo machafu katika nchi, watu wanabaka watoto, watu wanafanya ulawiti, yaani nchi imevurugika, na hata wazazi wanafanya mambo machafu dhidi ya watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nani ambaye anaweza kusaidia ili watu wetu waweze kurudi katika mstari. Ni watu wa ustawi wa jamii,

kama kuna vyuo na kama kuna wataalamu ni kwa nini hawaajiriwi? Na kwa kweli hawa watu wanatosha kukaa ngazi ya kaya. Hawa ndio wanaweza kuangalia zile tunaziita *home based violences* huku chini, kama wanawake wanaonewa, kama watoto wanaonewa, hawa ni wataalam wakiwa ngazi ya kata ngazi ya vijiji, wataweza kujua na kuleta taarifa iliyo sahihi ni kwa nini, watafanya utafiti ni kwa nini nchi inakuwa hivi? Ni kwa nini watu wanamong'onyoka namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali inaonekana inapendelea Idara ya Maendeleo ya Jamii peke yake. Ukitizama katika kitabu cha bajeti. Hata zile ajira 800 ambazo wataajiri wanaanjiri watu wa maendeleo ya jamii, ustawi jamii hakuna hata kidogo, yaani ni kama wamepuuzwa, lakini naomba Serikali isipuuzie jambo hili, lazima tuwaajiri watu warudi huku chini. Waende kusaidia watu katika ngazi ya kaya, waende kufanya utafiti, waweze…

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja amalize sentensi yake, waweze kufanya utafiti?

**MHE. CONCHESTA L. RWEMLAZA:** Waweze kufanya utafiti na waweze kuja na taarifa sahihi ni kwa nini mambo haya yanatendeka katika jamii? Ni kwa nini watu wanabaka? Ni kwa nini watu wanalawiti watoto? Ni kwa nini kuna ushoga? *Why?* Lazima kuwe na watu wa kufanya hivi, hatuwezi kufanya hapa kupata taarifa kutoka juu lazima...

**SPIKA:** Haya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mgaya.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nilikuwa napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge jambo analozungumzia ni la muhimu sana na Serikali itambue kwamba kuna tofauti kubwa kati ya Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii. Kwa maana ya *Social Worker* na huyo Afisa Maendeleo ya Jamii. Kazi ambayo inafanywa na huyo Afisa Maendeleo ya Jamii ambaye ni *Social Worker* ni kuangalia

maadili na kila kitu mambo ya *psychology* na vitu vya kijamii kwa ujumla na kwa hali mbaya tuliyokuwanayo sasa hivi ulimwenguni na kwenda na mambo ya ushoga na nini, ni muhimu sana wakaajiriwa Maafisa Ustawi wa Jamii wa kutosha ili kuweza kunusuru watoto wetu na vizazi vyetu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CONCHESTA L. RWEMLAZA:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, ni kweli lazima waajiriwe kwa sababu hawa ndio watu pekee ambao wanaweza kusaidia nchi kutoka mahali ilipo. Lakini ukitazama hata bajeti yao ukiangalia kwenye randama mimi nimepitia kwenye randama yao. Kile kifungu 5001 ambacho kinaonesha maendeleo, wamewapa shilingi bilioni mbili tu. Sasa nikawa najiuliza na zile wameziweka katika kutoa *service* ya *social welfare,* je, hapo wanapoajiriwa wanaenda kufanyaje? Wanakaa wapi? Hakuna hata hela za ajira.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata *development,* hata hiyo hela iliyopo ya maendeleo ni ya kurekebisha nyumba sijui ni nini, hakuna mahali ambapo wanaonesha hawa watu wanaweza kwenda kuzama vijijini ili waweze kusaidia jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo kama sisi watu wa zamani kidogo, wakati wa Awamu ya Kwanza lilikuwepo, *social workers* walikuwepo, walikuwa wanakwenda kata hadi kata, kijiji hadi Kijiji, wanakwenda ngazi ya familia kuangalia ni kwa nini hata mtu akigombana na mkewe. Ninachotaka kukwambia ni kwamba vijijini hakuna siri, ukimpiga mwanamke kijiji chote kinajua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ina maana *social welfare* huyu atakuja kufuatilia ni kwa nini hapa kuna ugomvi? Ni kwa nini mambo kama haya yapo? Na watu wanasema unauliza, kwa hiyo bila kuwa na watu hawa kusema kweli hatuwezi kuhakikisha kwamba kama tunataka mabadiliko tutayafanya mimi najua

kwamba Waziri amekuja na programu mbalimabli, lakini hii bado inampiga chenga kwa sababu hana nguvu ya kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemaliza hiyo sasa niongelee magereza kidogo kabla muda haujamalizika.

Kuna majeshi mbalimbali, kuna Jeshi la Polisi, Magereza, Jeshi la Wananchi lakini kuna malalamiko yanayotoka katika Jeshi la Magereza kwamba hawa watu wako chini ya Utumishi, lakini ni Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba unisikilize, hawa ni Jeshi wako chini ya Mambo ya Ndani lakini ajira zao na mienendo yao iko chini ya Utumishi. Lakini hawa wana-*standing orders* zao za Magereza ambazo zinaonesha ni namna wanavyoweza kupanda vyeo, namna wanavyoweza kulipwa, lakini hawafanyiwi hivi kwa sababu wao wako chini ya Utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwaje Jeshi linakuwa chini ya Utumishi na majeshi mengine yale yaliyobaki yako chini ya mfuko unaitwa *Consolidated Fund* wale wanahudumiwa huko, hawa wanashindwa kama Polisi, *TISS* na watu wengine wao wanakwenda na mfuko wa *Consolidated Fund,* lakini hawa wako chini ya Utumishi. *(Makofi)*

Mimi napenda kujua na nitoe ushauri kwa nini Serikali hailioni hili na ni kwa nini hawatoi watu wa magereza katika Utumishi? Sasa wanakuwaje Jeshi wa Magereza halafu huku wanaongozwa na Sheria za Utumishi, kwa hiyo mahali pengine hawatendewi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu posho zao za vyakula, posho za malazi, posho za mavazi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isikie au tuishauri kuwapandishia posho kutoka shilingi 10,000 kwenda shilingi 15,000 maisha yamepanda angalau. Wapewe *uniform* zao, wajinunulie wakati mwingine wanalaliwa wale na hawana mahali pa kulalamika. Kwa hiyo, wapewe pesa zao za mavazi, wapewe pesa zao za chakula, za umeme, za maji; wajilipie kila mtu kwa bajeti yake. Kwa sababu kipato cha Askari Magereza kwa kweli ni kidogo

sana. Ili waweze kufanikiwa na wenyewe waweze ku-*enjoy* kazi yao naomba Serikali, nakuomba Waziri wa Fedha kupitia kwa Spika wewe uende utazame hili, maana sasa hivi tunatoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi sina mengi kwa leo, nashukuru sana na ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bajeti hii tunayo kwa siku saba, lakini Wabunge waliokuwa wameomba kuchangia kwa siku ya kwanza, majina yao hapa yaliyobaki ni machache.

Kwa hiyo, nitaongeza muda ili tumalize hao kwa sababu hawa wengine wameomba kuchangia kuanzia kesho na hatuwezi kuwaita leo.

Kwa hiyo, naongeza nusu saa ili tuweze kukamilisha wale waliokuwa wameomba kuchangia Bajeti Kuu kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

Mheshimiwa Mchungahela kabla hujaanza kuchangia kuna mgeni hapa wa Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete ambaye naye ameingia baada ya kusoma tangazo la kwanza. Huyu ni Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rungwe, Ndugu Ambokile Mwang'umbe, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, lakini nikushukuru wewe pia kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu ningependa pia kutoa shukrani kwa Wizara ya TAMISEMI kwa

kunielewa baada ya kuwa nimelia muda mrefu humu ndani kutokana na changamoto za Halmashauri yangu. Namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuniletea mtu makini sana pale wilayani kwangu. Ni makini sana huyu mtu, huyu ni Mkuu wa Wilaya anaitwa *Mr. Kanuni,* hapa ni kanuni kweli kweli, na nafikiri vilio vyangu vilivyokuwa vikifululiza hapa kuhusiana na changamoto zinazojitokeza katika halmashauri yangu zitapungua kwa muda mfupi tu aliokaa Mheshimiwa huyu nimeona matunda yake makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo nianze moja kwa moja na mchango wangu, na mchango wangu utajielekeza katika maeneo mawili; eneo la kwanza litahusiana na masuala ya Wizara ya kilimo, na hapa moja kwa moja nitajielekeza kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ni zao la korosho? Ni kwa sababu zao la korosho limekuwa likituongezea sana pesa za kigeni ambazo ni muhimu sana katika muhimili wa uchumi wa nchi hii. Kwa mfano, mwaka 2017/2018 korosho ililiingizia pato la Taifa dola takribani milioni 500, pesa hizi ni pesa nyingi sana katika uchumi, na imekuwa ikifanya hivyo kwa wastani kiasi hicho hicho kama miaka mitatu minne mfululizo hivi, lakini ninazungumzia suala hili sasa hivi kwamba uzalishaji wa korosho umeshuka kwa kiasi kikubwa sana, jambo ambalo nafikiri tunahitaji kila sababu ya kujiuliza kwa nini kushuka kwa namna hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka takribani 2017/2018 kulikuwa na uzalishaji wa korosho wa tani 313,000 hivi, lakini kutoka hapo mpaka kufikia mwaka 2022 kumekuwa uzalishaji ukishuka kwa kiwango kikubwa sana kufikia kutishia amani ya lengo letu tulilojiwekea la kuzalisha tani 700,000 kwa mwaka. Kutoka tani 313,000 mwaka 2022/2023 korosho zilizalishwa kwa tani 186,000 hivyo kufanya mchango wa zao hili kwenye pato la Taifa kushuka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais kutaka kuboresha zao hili, lakini kumekuwa na mambo ya makusudi kabisa yanayoonekana kuwa ni uzembe unaosababisha kushuka kwa zao hili. Kwa mfano, hivi

ninavyokwambia tayari pembejeo zimeshafika ambazo Mheshimiwa Rais kwa jitihada yake kubwa sana aliifanya kuzileta hapa nchini. Nashukuru pia Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Bashe na wasaidizi wake wa karibu walifanya jitihada za kuhakikisha kwamba, pembejeo hizi zinaingia nchini, lakini cha kushanganza mpaka sasahivi hizi pembejeo bado hazijagawiwa. Jambo ambalo linatia shaka kwamba, ni kwa sababu gani hizi pembejeo hazigawiwi licha ya kuwa zimekuja hapa ni mwezi mzima sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanatakiwa kutoa pembejeo hii ni maeneo ambayo kwa sasa hivi wanatakiwa wajiandae na masuala ya kupulizia, kwa mfano katika Wilaya ya Masasi, Jimbo la Lulindi, takribani kata zote sasa hivi zinahitaji pembejeo, lakini *so far* ni kata chache sana wamepewa pembejeo na kuna maeneo mengine tunashangaa unapeleka mfumo uliotumika sasa hivi ambao ni mfumo bora wa kupata idadi halisi ya wazalishaji, lakini *coupon* zinakwenda, zile *coupon* hazina idadi ya pembejeo inayotakiwa apewe mzalishaji. Unakuta umeambiwa fulani utapewa pembejeo, unapewa *coupon,* ukienda pale hakuna chochote. Kwa hiyo, sasa tunashangaa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, ni uzembe kama nilivyosema kwa kweli, na hali hii inafanya kuwakatisha tamaa viongozi wetu wakubwa kwa sababu wao wana ndoto ya kuona kwamba zao hili linakwenda vizuri, liendelee kuzalisha, lakini pia liendelee kutoa mchango mkubwa kama ilivyokuwa ikifanya hapo mwanzo kwenye uchumi wa nchi hii. Ni muhimu kwa sababu inapunguza urari, *I mean* ile *deficit* ya urari wa biashara. Sasa kama hali itaendelea kuwa hivi kwamba, inashuka kila siku bila shaka hata hiyo faida hatutaiona.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka niongelee pia kwamba zao hili limekuwa tegemezi sana kwa baadhi ya taasisi katika hii nchi. Ni kwamba pesa nyingi zimekuwa zikitoka kwa mfano, kila kilo moja ya korosho imekuwa ikikatwa pesa kadhaa kwa maana ya tozo kwa ajili ya kuhudumia hizo taasisi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Korosho wanapata shilingi 30 katika kila kilo; Halmashauri wanapata shilingi 65 kwenye kila kilo; Chuo cha Naliendele wanapata shilingi 15 kwenye kila kilo; Chama Kikuu cha Ushirika wanapata shilingi 30 kwenye kila kilo; Chama cha Msingi wanapata shilingi 25 katika kila kilo; Halmashauri inachangiwa pia elimu shilingi 30 katika kila kilo; lakini cha kushangaza hata mfanyabiashara yule anayenunua korosho anachangiwa kwa kusafirishiwab korosho zake mpaka kwenye eneo anakotaka kuzipeleka.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa utakuta kwamba ni zao pekee lenye pesa nyingi sana za tozo, lakini licha ya umuhimu huu zao hili hawa wanaochangiwa wanalidharau kwa maana ya kwamba hawafanyi kazi inayostahili kuhakikisha kwamba zao hili linakuwa bora.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kuna shida hapo na uzalishaji imeshuka, lakini halikadhalika kuna shida ya bei. Mwaka jana ni mwaka ulikuwa *very worse,* bei ilishuka kwa kiwango cha ajabu kabisa na kama unakumbuka nilishauliza hapa kwamba taratibu gani zinafanyika na Serikali kuhakikisha ile bei inaimarika, lakini mpaka sasa hivi bado hakujawa na majibu yaliyokuwa yanaleta matumaini kwa wakulima kwamba, hizi bei zitapanda au huu uzalishaji utapanda. Kwa kweli ni jambo ambalo tunatakiwa tujitathmini sana kwa umakini kama kweli tunataka kuendeleza zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nililotaka kulizungumzia kwa siku ya leo ni kuhusiana na udhibiti wa mifumo; kumekuwa na mifumo mbalimbali ambayo imetengenezwa *so far,* ni jambo jema sana kwa Serikali kwa sababu ya nia nzuri ya kutaka kudhibiti mapato ya Serikali kwa namna moja au nyingine katika *level* mbalimbali, *level* ya Halmashauri, lakini hadi kwenye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mifumo iliyowekwa ni mizuri japo kwa kiasi kikubwa kuna changamoto kwamba tulikuwa tunategemea sana katika suala la uboreshaji paboreshwe katika mfumo wa *I mean internal control system,* mfumo wa *control system. (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30, muda wako umekwisha.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi pia ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata hii nafasi ya leo, lakini pia nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa yale ambayo ameyafanya kwenye nchi yetu, na pia tujipongeze sisi ma-baba wote kwa sababu, jana ilikuwa siku ya ma-baba duniani maana ingekuwa siku ya ma-mama ingekuwa hatari na mimi ni baba bora, naomba nijipongeze kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kidogo sisi Wana-Morogoro Vijijini tuna jambo letu, tuna malalamiko yetu, nikikumbuka wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alisimama akatoa ahadi kwamba mwezi huu wa sita watasaini mikataba kwa ajili ya barabara. Jana wananchi wa Morogoro Vijijini wote wameandamana kwamba Mheshimiwa ulisimama na ukaongea na tulimsikia Waziri akiongea kwamba barabara zinakwenda kusainiwa mwezi huu wa sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia tayari mwezi upo mkiani huu, unaondoka. Wenzetu jana wamesaini, sisi Wana-Morogoro Vijijini hatujasaini, lakini tunajua labda shida yake ipo kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, niangalie kijana wako, niangalie nilivyo mdogo, niangalie majukumu ya lawama ya barabara ya Bigwa – Kisaki ni makubwa sana. Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake ya dhati ametugawia kilometa 78 na nikinukuu maneno yako uliyoongea juzi jambo

jema ni la mama, mabaya ni ya kwenu. Sasa ikiwa hili halifanyiki wabaya ni ninyi, sio Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu naomba ungemwambia Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Mbarawa hili tatizo la kutokuwa na barabara ya Bigwa – Kisaki na mnakuja hapa mbele mnatuahidi mtasaini na hamfanyi, mnakwenda kumdhalilisha mama yangu na mimi nimesema juzi mimi ndio kipenzi cha Mama Samia, mnataka kunivunja moyo mama yangu asinipende jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi siwezi kupiga sarakasi humu ndani, siwezi kupiga msamba humu ndani, labda ni-*rap* tu ili wafurahi, mimi nitachana humu ndani kwa sababu hatuwezi kuwa tunazungumza jambo moja lilelile kila siku. Suala la barabara Mheshimiwa Rais ameshatoa na kama ni fedha Mheshimiwa Mwigulu unayo, tupatie tuanze kujenga barabara ya Bigwa - Kisaki, hii ni aibu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza barabara nizungumze kuhusu michezo kidogo. Rais wetu wa Awamu ya Sita ambaye…

Mheshimiwa Spika, kama anataka kuongea muache anijibu roho yangu ifurahi.

**SPIKA:** Kwa sababu mimi hupenda kutenda haki, nikishamruhusu akujibu wewe na Wabunge wengine watataka kujibiwa. Kwa hiyo, tumpe nafasi ayakusanye, atayajibu. Si ndio Mheshimiwa eeh? Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wasubirie kipenzi cha mama kinaongea. Ungemuacha ajibu.

Mheshimiwa Spika, turudi kwenye suala la michezo; Mama Samia ndio raia ambaye ametuonesha mapenzi ya dhati ya kuipenda michezo; Mama Samia ndio Rais ambaye ametuonesha mdau mkubwa na mwekezaji kwenye Wizara ya Michezo. Wiki mbili zilizopita nilivyochangia kwenye Wizara ya Michezo

nilizungumza kuhusu ile asilimia tano inayotoka kwenye michezo ya kubashiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliona kwamba hii Wizara inapewa pesa ndogo, shilingi bilioni 35 ni pesa mbuzi, basi akaona bora hii asilimia tano ya michezo ya kubashiri inayopatikana iende kwenye Wizara ya Michezo. Mimi nikizungumza nipo kwenye Kamati ya Michezo, hii Wizara imepata shilingi milioni 900 mwezi wa pili mwaka huu na hiyo shilingi milioni 900 iliyopata ni ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kunukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri; mazuri ni ya Mheshimiwa Rais mabaya ni ya kwao. Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mwigulu Nchemba wewe nchi inatambua mema yako, nchi inatambua mapenzi yako na michezo, mimi nina hofu kubwa sana ukiondoka kwenye hiyo Wizara tutatetereka zaidi. Kama ikiwa leo hii wewe uko hapo tu asilimia tano ya Mama Samia haiendi kwa wakati, kama leo hii uko hapo tu, Mheshimiwa Waziri nimemuhoji juzi kwenye hii asilimia tano mnayopata mchanganuo ukoje? Hajui.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waziri anayepelekewa huo mchele wa shilingi milioni 900 hajui mchanganuo upoje. Na hiyo shilingi milioni 900 mliyopeleka ya mwaka jana huko, mwaka huu mwaka mzima, hii miezi sita, sio kama watu wanaochezesha michezo ya kubashiri hawapeleki hela kwako, *bro (brother)* mimi nakufahamu wewe ni mchumi, unatazama pesa zaidi, lakini hii Wizara ili tuweze kujibeba inahitaji kuwa na pesa vilevile.

Mheshimiwa Spika, mimi niombe kitu, tunapozungumza kuhusu michezo ya kubashiri ni michezo. Mheshimiwa umekumbatia mzigo mwingi, tunaomba huu mzigo wa michezo ya kubashiri uupeleke kwenye Wizara ya Michezo na ukishindwa kufanya wakati uko hapo, hakuna anayeweza kufanya. *Bro (brother)* mimi naamini wewe umeikuza *Singida Big Star,* leo hii una nuru kubwa, basi kaikuze michezo, wapelekee huu mfuko wa michezo ya kubashiri uende kwenye Wizara ya Michezo wawe wana uwezo wa kuamua jambo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kitu kimoja na ninachokiongea naongea kwa *fact* kwa sababu mimi nimeishi kwenye michezo, maisha yangu nimeyapata kwenye michezo, mbebeshee huu mzigo. Najua wewe ni mtaalamu wa kodi unafikiria nikiwapa Wizara ya Michezo kodi yangu wataniletea?

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake Mwana FA hawawezi kukuangusha kwenye hilo. Wapelekee michezo ya kubashiri kama ilivyo, hutasikia vilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaona wenzetu, nchi za wenzetu zinafanya vizuri. Nilikuja na mafano hapa wa nchi kama Senegal imefanya vizuri kwenye michezo ya ndani kwenye timu zote za Taifa kwa sababu Wizara yao inapata pesa nzuri; nimetoa mfano wa nchi kama Uingereza, michezo ya kubashiri yote inaenda kwenye Wizara ya Michezo; nimekuja na mfano wa nchi kama ya Japan, michezo ya kubashiri pesa zote zinakwenda kwenye Wizara ya Michezo; nchi ya Tanzania michezo ya kubashiri iko kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunakufahamu wewe ni mchumi, lakini hebu kata hili kidogo ndugu yangu wape Wizara ya Michezo wajiendeshe. Mkikaa kwenye vikao vyenu mnapanga mipango ya kuwagawia shilingi bilioni 35, hiyo shilingi bilioni 35 waendeleze michezo yote.

Mheshimiwa Spika, tunawaona *TFF* wanateseka kujenga viwanja. Tumeona juzi Tanga pale wakati tunawaangalia kwenye siku ya tuzo, wametuonesha uwekezaji wao, lakini ule uwekezaji unatakiwa kufanywa na Serikali, kufanywa na Wizara. Sasa Mheshimiwa Waziri, kaka yangu na mwanamichezo tunayekutegemea ingawa timu yako imeshapoteza kocha na hivi karibuni za ndani Mayele harudi, kwa hiyo, naona wazi kabisa utaenda kutusaidia, utaenda kusaidia Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri haya maneno nayarudia mara mbilimbili kwa sababu najua siku ya wewe kufungua moyo, siku ya kubeba michezo ya kubashiri kuipeleka kwenye Wizara ya Michezo ndio siku ya Wizara hii ya Michezo kwenda kuisaidia michezo na sanaa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo siwezi kusema naunga mkono hoja mpaka nione anasema nini. Nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, tutamalizia na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi nichangie. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa hili, ni ukweli usiopingika Mheshimiwa Rais amepokea miradi mikubwa na ameiendeleza vizuri na tunaona anaibua miradi mingine mikubwa, kwa kweli tuna kila sababu ya kumpongeza, tuna kila sababu ya kuendelea kumuombea ili Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, aendelee kufanya kazi vizuri, lakini haya mazuri yote tunayoyaona tunaamini ni pamoja na wasaidizi wake hasahasa akiwemo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa unayoifanya ya kusimamia Wizara inayokusanya fedha. *(Makofi)*

Ninakupongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu, unafanya kazi kubwa nzuri, songa mbele tuko pamoja na wewe na ninaamini Mungu atakusaidia kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee mikoa hii ambayo ni mikoa masikini. Ukiangalia kwenye bajeti zilizopita bado sijaona mkakati na mipango maalum ya Serikali kuweka nguvu kwenye hii mikoa maskini na miongoni mwa mikoa maskini, nisikitike mkoa wangu wa Kagera ni miongoni mwa mikoa maskini.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo ambalo linasikitisha ukija kuangalia hii mikoa ambayo ni maskini ndio mikoa ambayo zile fursa za kiuchumi haziko sawasawa. Ukija kuangalia mimi

napakana na nchi ya Uganda, ukiangalia kwa majirani zetu pale, ukiangalia barabara wamekuja wameleta mpaka mpakani tena wakavuka wakaingia kwetu kidogo kutuonjesha, kwetu ukiingia hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, nimeongelea barabara ya Mgakorongo kwenda mpaka Murongo, nimeongelea barabara ya Murushaka kwenda mpaka Murongo, barabara hizi zimeshatangazwa *tender* lakini shughuli ni kusaini barabara hizi ili ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Kagera tuna fursa nyingi sana, lakini shida iliyopo miundobinu ya barabara siyo rafiki. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, mimi ninaamini kazi unayoifanya ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kufuatilia sana baada ya kuona Waziri ananiambia baada ya wiki mbili tutakwenda kusaini, baada ya wiki moja tutasaini. Sasa nikafuatilia, taarifa za ndani nilizozipata wanasema shida ni fedha. Sasa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wewe ndiye mwenye fedha, nikuombe sana barabara hii ambayo ni ya Murushaka kwenda mpaka Murongo, barabara ya Mgakorongo, barabara hizi zisainiwe ili tuweze kuinua uchumi wa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kyerwa sisi tunalima kahawa nyingi sana, lakini nguvu tunayotumia kuisafirisha kahawa hii kwenye barabara hizi mbovu unakuta tunatumia gharama kubwa wakati tungeweza kutumia gharama kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini mikoa hii ambayo ni maskini ndiyo mikoa ambayo hata umeme wa uhakika hakuna. Umeme kwa siku unaweza ukakatika zaidi ya mara kumi, kweli hapo tunategemea hawa wananchi wanaweza wakaendelea? Tunaweza tukainua uchumi wao?

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu nina vitongoji 617, kati ya vitongoji hivyo vitongoji 400 havina umeme; mnategemea hawa wananchi watainuka kweli? Lakini mikoa hii ambayo ni maskini

fuatilia muangalie miradi ya maji, ni midogo sana. Hata hiyo iliyopo bado fedha inayoletwa kwangu mimi nina mradi wa Nkwenda mpaka Chanya, nina mradi wa Isingilo, nina mradi wa Mabila, miradi hii inavyokwenda inakwenda kwa kusasua kwa sababu fedha haiji kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mikoa hii ambayo ni maskini uweke mpango maalum namna gani ya kuboresha miundombinu, namna gani ya kuipelekea miradi ya maji, namna gani ambayo mnaweza mkaipelekea umeme wa uhakika ili tuone kama hii mikoa inaweza ikainuka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee ni kahawa; kahawa ni zao la kimkakati, lakini zao hili, mimi nipongeze kwa sehemu Serikali imejitahidi ndani ya miaka hii miwili ya mama yetu Samia, kahawa tulikuwa tunauza bila utaratibu, lakini angalau tuemeweza kuipeleka kwenye mnada bei angalau inaweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado niiombe sana Serikali ifanye utafiti kwa nini nchi jirani ya Uganda kahawa bei iko juu kuliko Tanzania? Tunafanya kazi kubwa ya kupambana na watu wanaofanya magendo. Hebu tufuatilie; hawa Uganda wanauza wapi? Mimi ninaamini soko la kahawa dunia nzima ni moja, sasa hawa Uganda wanauza wapi?

Mheshimiwa Spika, tufanye utafiti wa uhakika ili tuweze kuwapa wakulima hawa bei nzuri tuondoe hii biashara inayoendelea ya magendo na kuanza kukimbizana na watu, kuwapiga na kufanya mambo mengine, kwa sababu hatuwezi kuzuia, kama huna bei nzuri jirani yako ana bei nzuri, watu watakimbia. Mimi Mbunge siungi mkono biashara ya magendo, lakini unazuiaje? Kwa hiyo, niombe sana Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kahawa kuna hii biashara ya butura inayoendelea. Biashara hii lazima tuje na mpango wa kuwawezesha hawa wakulima angalau waweze kupata fedha ambayo itawasaidia pale wanapoanza kuhudumia hii kahawa mpaka wanapofika kipindi cha kuvuna, awe na fedha

ya kumsaidia kuhudumia kahawa mpaka anaipeleka kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri umeongelea suala la makusanyo na kwenye hotuba yako ukaeleza mwamko mdogo wa watu kulipa kodi.

Ndugu zangu, mimi nilikuwa namwomba sana Mungu, ni kwa nini Watanzania hatutaki kulipa kodi na hatutaki hata kudai risiti tu. Unatoa fedha yako mfukoni unakwenda kununua kitu lakini unaona haikuhusu. Ni kwa sababu hatuna upendo na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, na nianze na sisi humu ndani, leo tumekuja hapa kila mmoja anaeleza anataka barabara, anataka maji, lakini wewe umewajibika vipi kuhamasisha wananchi wako, kuhamasisha wafanyabiashara ulionao, lakini wewe mwenyewe binafsi unapokwenda kununua vitu ni mara ngapi umedai risiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wengi mko humu ndani, ni mara ngapi mmeiibia Serikali? Halafu tunakuja hapa tunataka barabara. Kila mmoja awajibike kwenye nafasi yake. Tulitangulize Taifa mbele, tuwe na upendo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii tunayoidai siyo kwa faida ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wala siyo kwa faida ya Mama Samia tu, ni kwa faida ya Watanzania wote. Wote tuiwa na moyo wa upendo kwa Taifa, tukalitanguliza Taifa, unapokwenda kununua kitu ukadai risiti, mimi hata kama ni shilingi 5,000 lazima unipe risiti, vinginevyo utarudisha hela yangu. Hebu tuwe na moyo wa kulitanguliza Taifa, tudai risiti tukalipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina uhakika Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, hela mnayoikusanya na hili jambo ninalowaambia nimemwomba Mungu na nina uhakika Mungu alichosema na mimi ni sawa, Watanzania hatuna upendo na Taifa letu. Nina uhakika Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kama kila Mtanzania akisimama kwenye nafasi yake, akalipa kodi sawasawa, akadai

risiti anapokwenda kununua, hela tunayoweza kukusanya peke yake inaweza ikakamilisha miradi yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu kila mmoja awajibike. Wafanyabiashara wanapodai Serikali iwahudumie na wao wawe tayari kuhakikisha wanalipa kodi kwa uaminifu. Sisi Wabunge tunapokwenda tunasema tunataka barabara, tunataka miradi ya maji, tunataka umeme, na sisi tuwajibike tuwe waaminifu kulipa kodi, tuwe waaminifu kuhakikisha tunadai risiti tunaponunua bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bilakwate, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza nami nachangia bajeti ya Serikali, lakini siyo kwa mara ya kwanza kabisa, bajeti hii Kuu ya Serikali siku ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, natamani nisome kipande kidogo cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kabla sijaanza kuchangia kwa sababu lengo langu leo nataka nichangie zaidi kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 12 Waziri wa Fedha alituambia; "Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi vijijini ambapo kilimo ndiyo msingi wa ustawi wa maisha, Serikali ya CCM chini ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea na dhamira yake ya kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294.0 mwaka wa fedha 2021/22 hadi shilingi bilioni 954.0 mwaka wa fedha 2022/23 na kufikia shilingi bilioni 970.8 mwaka huo ambao tunauanza. Kuongezeka kwa bajeti ya kilimo kumewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo; kuanzishwa kwa kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja; kuimarisha tafiti na huduma za ugani; kutolewa kwa ruzuku ya mbolea kwa wakulima; kuanza kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji na miundombinu…" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma kipande hiki ili kukumbusha tu maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, dhamira njema ya Serikali kuhusu kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Mikoa ya Singida, Simiyu na Dodoma tulipewa kazi ya kuzalisha alizeti kwa wingi ili kupunguza pengo la mafuta katika nchi yetu. Lakini leo ni majuto makubwa sana kwa wakulima wetu. Majuto yanakujaje? Badala ya kuongeza kodi ya mafuta yanayoingizwa nchini sasa inakwenda kupungua.

Mheshimiwa Spika, lakini leo tunapozungumza kilo ya alizeti sasa ni shilingi 500. Hapa Mjini Dodoma tulipo ukitaka kununua galoni ya mafuta ya kula ya alizeti ni shilingi 18,000, ikizidi 20,000. Hivi leo tunazungumza nini juu ya mkulima wetu wa Tanzania? Ananufaikaje na kilimo hiki ambacho Serikali ilitoa mbegu, ikatoa ushaiwishi mkubwa kwa wananchi ili walime alizeti, leo imeshuka sana.

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kupunguza kodi za mafuta ghafi yanayotoka nje, tunakwenda kuwaua wakulima wetu. Ninaomba Serikali iache uthubutu huo inaotaka kufanya. Tusaidie wananchi wa Tanzania, wakulima wetu ambao walitumia nguvu kubwa na ushawishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda Singida akafanya mkutano kushawishi wananchi walime sana

alizeti. Wizara ya Kilimo ikaleta mbegu, wananchi wakachukua na wamelima, leo alizeti imeshuka sana, wananchi wana majonzi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali, namwomba Waziri wa Fedha, mwana-Singida mwenzangu, awaangalie wananchi wa Mkoa wa Singida. Wasipunguze kodi za mafuta ghafi yanayotoka nje ya nchi ili angalau alizeti ipande kidogo, ili Watanzania waliolima mwaka huu kwa ushawishi wa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi waweze kunufaika na mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ya Tanzania ili tutoke katika umaskini na kama alivyosema hapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba uti wa mgongo wa nchi hii ni kilimo, na wakulima ndiyo asilimia kubwa ya Watanzania, kilimo cha umwagiliaji ndiyo suluhisho. Leo tunapozungumza hatujafikia asilimia kumi ya ardhi ambayo inafaa kwa kilimo kulimwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna eka zinazopungua milioni moja za umwagiliaji. Tumeona bajeti ilivyoongezeka kwa asilimia 300 ya bajeti iliyokwisha, lakini hatujaona mafanikio kwa asilimia 50 ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yetu. Mimi ninapozungumza hapa sina skimu hata moja iliyo kwenye mpango kwa bajeti iliyopita. Kama Mbunge wa Jimbo, Halmashauri yangu ya Itigi katika Halmashauri 184 haimo katika mipango ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama tuna nia ya kuisaidia nchi hii tutokane na umaskini na watu wetu, tutoke katika kilimo cha kutegemea mvua. Hatuwezi kutoka moja kwa moja, lakini tusaidie wananchi wetu, tuongeze skimu za umwagiliaji katika maeneo yetu. Ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mujibu wa maelezo ya kitaalam ni ekari milioni 22. Leo ekari milioni moja hatuna Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyokwisha Wizara ya Kilimo ukiondoa kule kwenu Mbeya, ile Madibila maeneo mengine bado tunahangaika tu. Ninaomba sasa Serikali itie mkazo katika kilimo cha umwagiliaji, kitakuwa na tija na ni mkombozi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye ruzuku za mbolea kuna jambo ambalo tunashangaa ni kwa nini linatokea. Mmegawa wakulima kwa madaraja, wakulima wa pamba, wakulima wa tumbaku mbolea yao haina ruzuku. Maana yake ni nini; hawana faida, hawafai, hawatakiwi? Kwa nini mbolea isiwe na ruzuku kwa wakulima wote, uchague zao la kulima ili iwe tija kwa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, inapoongezeka bajeti ya Wizara ya Kilimo kwani hawa wakulima wa pamba hawajachangia katika mapato ya nchi hii? Hawajachangia kodi ambazo zimesababisha wao kuongezewa? Wakulima wa tumbaku ambao kule kwangu Itigi nao wanalima mbolea yao haina ruzuku.

Ninaomba Serikali iondoe huo ubaguzi wa kubagua wakulima wa aina ya mazao fulani. Twende kama wakulima ruzuku inayopewa mbolea nchi nzima wapate ruzuku ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, nina jambo lingine ambalo nataka kulichangia; mifumo ya TEHAMA. Mifumo ya TEHAMA katika Halmashauri zetu, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Mawaziri wake hawa wamepeleka miradi mingi katika maeneo yetu, lakini mifumo haifunguki, miradi haitekelezeki. Wanachukua bidhaa za watu, wanachukua mafuta kwenye *petrol stations,* namna ya kuwalipa inakuwa mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba mifumo ifunguke, lakini pia isomane. Mifumo ya Halmashauri haisomani na *TRA*. Mifumo ya Halmashauri haisomani na maeneo megine. Hata Bandari na *TRA* mifumo haisomani…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, tunatamani kuona mifumo hii iwe mifumo imara ambayo ili utekelezaji wa bajeti na hasa utekelezaji wa miradi hii kule vijijini kwenye Halmashauri zetu iweze kufanyika vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa msemaji kwamba sasa hivi leo ni siku karibu ya 25 Halmashauri zote zimesimama uendeshaji wake na mifumo imezimwa, na tunakwenda kumaliza bajeti, tunataka hili analolizungumza Mheshimiwa Yahaya ni la msingi shughuli za Serikali zimesimama, nini mustakabali wa hili jambo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, taarifa naipokea kwa sababu ni suala la ukweli. Mimi ninapozungumza hapa Halmashauri yangu ya Itigi vitu vimesimama. Serikali imetuletea, tunajenga Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya pale, lakini wale wanaotusaidia kuhudumia pale wamesimama na wamekwama kwa sababu mfumo umezima kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hata Madiwani wangu kule Itigi hawajalipwa kutokana na mifumo imesimama, imezimika, haifanyi kazi. Kwa hiyo, ni mambo ya kweli na nataka twende sasa tuwe na mifumo imara ambayo itafanya kazi kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa namna ilivyofanya hasa katika miundombinu, tumeona barabara kilometa zikisainiwa, majuzi tu, kwangu kule Itigi tunajenga barabara kwa kiwango cha lami, kilometa 56.6, ninaomba sasa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** …zimebaki kilometa 356 kuja Mbeya kule kwako pale Makongorosi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa basi Mheshimiwa Waziri aiweke katika mipango yake na mimi niingie katika utaratibu huo

wa barabara ya lami. Ahsante sana kumalizia barabara ya Makongorosi – Mkiwa hadi Itigi, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja hizi za Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu, na nianze kwanza kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyofanya kazi na ambavyo amejitahidi sana katika kutafuta rasilimali fedha katika kutekeleza miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu kwa ujumla, kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli mmeweza kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais na kuyatekeleza mambo mengi kwa kipindi kifupi. Kazi kubwa mmeifanya, mnastahiki kwa kweli kupongezwa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Wizara kwa sababu ya mambo yafuatayo ambayo yamejitokeza kwenye bajeti, sitaweza kuyasema yote, lakini machache naweza kuyasema.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ongezeko la mapato yaani makusanyo yameongezeka kwa kipindi kilichopita mpaka sasa hivi. Mmefanya jitihada kubwa mapato yameongezeka, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bajeti za sekta za uzalishaji; kilimo, mifugo, uvuvi, bajeti imeongezeka kwa kiwango kikubwa. Haijawahi kutokea, kazi hiyo mmeifanya vizuri, hongereni sana na tunaona kwa mfano kilimo sasa hivi tena bajeti ya mwaka huu inaongezeka inakwenda kufikia shilingi bilioni 970. Kwa kweli hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mmeleta pendekezo la kuongeza shilingi 100 kwenye mafuta ili kuwa na vyanzo ambavyo

vinaeleweka katika kutekeleza miradi ya kimkakati, hili ni jambo la msingi sana. Tunayo miradi mingi ya kimkakati, tulikuwa hatuna vyanzo, sasa hiki tukikifunga yaani tuka-*ringfence* itasaidia sana katika kutekeleza hii miradi ya kimkakati, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TARURA* imeongezewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 370 zimeongezeka, lakini tumeshuhudia mapendekezo ya kwamba sasa vyuo vyetu vya ufundi, Chuo cha *Dar Tech,* Chuo cha *MUST* – Mbeya na Chuo cha Arusha, sasa watoto wote wanaosoma watapatiwa mikopo. Lengo tupate wataalamu katika nyanja mbalimbali, ni jitihada kubwa sana ambazo mmefanya, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mmesema mmetenga fedha kwa ajili ya kwenda kuchimba visima/mitambo ya kuchimba visima, hii kwa kweli itachochea sana maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha Tume ya Mipango; tulishauri Tume ya Mipango ianzishwe, mmesikia kilio, kwa usikivu huo Tume ya Mipango imekwenda kuanza, hii ni hatua kubwa ambayo kwa kweli tumeifanya katika kipindi hiki na mambo mengine mengi ambayo mnakwenda kuyafanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yako tunawapa hongera sana kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli mmefanya. Yapo mengi ambayo yapo, hatuwezi kuyasema yote yakaisha, lakini mmeyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie kwenye maeneo angalau mawili, kama muda utaruhusu nitaongezea labda la tatu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni suala la tija; tija kwenye kilimo, tija kwenye mifugo, tija kwenye uvuvi na maeneo mengine, lakini tija kwenye viwanda yetu. Tija bado iko chini sana, lazima tuweke mkakati wa kuongeza tija, tukiongeza tija ndipo pale tutaweza kupata ufanisi na ndipo uchumi wetu utaweza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kilimo chetu ukiangalia tija ni ndogo mno, uzalishaji ni mdogo mno. Ukienda kwenye ufedhaji tija haipo kabisa. Sasa lazima kama Serikali tuwekeze rasilimali namna tutakavyosaidia kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na katika eneo hili Mheshimiwa Waziri huko nyuma tulikuwa na Baraza la Taifa la Tija, sasa lile tuliliondoa. Sasa kwa kuwa Tume ya Mipango imerudi, basi napendekeza na hili Baraza la Taifa la Tija lirudishwe, lianzishwe ili lisaidie katika kuchochea na kuhamasisha kuongeza tija kwenye kilimo, mifugo, viwanda na huduma mablimbali na hii itatusaidia sana katika kujenga uchumi mzuri ambao utakuwa ni imara, naamini hili eneo mtalipa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha tatu ambacho nataka nichangie, sasa hivi sote tunazungumzia kilimo, mifugo na kadhalika, lakini hatuweki mkazo kwenye kuongeza thamani, *value addition* ya hizo. Hatuwezi kusema tuendelee kuzalisha malighafi, kuzalisha mazao tunauza nje, kufanya nini, sasa hivi dunia imetoka hapo, tujitahidi sasa uzalishaji wetu tuongeze thamani. Kwenye *value chain* hapa ndipo tunatakiwa tuwekeze sana. Tukifanya hivyo ndipo nchi yetu itaweza kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunazalisha mahindi tunapeleka kwenda kuuza mahindi yakiwa kama mahindi, tunazalisha kahawa tunakwenda kuuza kama kahawa, tuwekeze kwenye kuongeza thamani ya hivyo ili tukauze *final products* maeneo mbalimbali, na hiyo ndiyo itatusafanya kwamba tupate fedha nyingi, lakini pia uchumi wetu uwe imara na ajira mbalimbali ziongezeke na umaskini katika nchi yetu uweze kupungua. Kwa hiyo, mimi napendekeza hebu tuangalie sana *value addition* katika *products* zetu, tukiwekeza hapo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka kuchangia na nilitaka kuongeza, kwamba nimeona katika jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali na nimeona kabisa kwamba kwa kweli jitihada ni nyingi zinachukuliwa. Lakini mimi nataka tulipendekeza hapa kipindi kilichopita kwamba katika ufufuaji na uimarishaji wa bandari zetu, tukasema tunataka na

Bandari ya Bagamoyo sasa tuijenge, tulipendekeza mwaka jana tukasema ijengwe.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hili sijaona mkakati wa kusema sasa tunaanza mikakati ya kuijenga Bandari ya Bagamoyo, kwa sababu hii ni rasilimali tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Tunataka zile bandari ziweze kuhudumia maeneo mengine. Tukiimarisha miundombinu hii ya *SGR,* barabara na maeneo mengine, tunataka sasa bidhaa zisafiri vizuri tuwahudumie nchi za *SADC* zote, nchi za Kusini mwa Afrika ambazo sisi tuna lango hili kwenye bahari yetu tuweze kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nataka nione mkakati, tuna mkakati gani wa kuhakikisha tunatafuta kama ni mwekezaji, kama ni nini, tujenge Bandari ya Bagamoyo ili ishirikiane na bandari zilizopo katika kuweza kuchangia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo, pale Tunduma bado naendelea kilio changu, pale ndiyo lango la *SADC,* tunaomba pawe na bandari kavu, bandari kavu ile itasaidia sana katika kuweza kutoa huduma katika nchi za *SADC,* mizigo itasafirishwa kutoka kwenye Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine, ikifika pale basi wale wafanyabiashara watachukua kwa gharama nafuu kuliko namna sasa hivi inavyosafirishwa kwa kutumia magari na barabara zinaharibika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi hapo tunaomba mkakati mahususi wa kuimarisha reli ya *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* ilijengwa ni reli ya uhuru, reli ya siku nyingi, reli ambayo ni muhimu sana katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mlituahidi kuleta sheria hapa kwamba mtabadilisha sasa sheria ili ile *TAZARA* ambayo inamilikiwa na nchi mbili iweze kuboreshwa, tuweze kuwekeza, iweze kutoa mchango mkubwa. Sasa mpaka sasa hivi sijasikia nini kinaendelea kuhusiana na ufufuaji wa reli ya *TAZARA*. Tunataka tupate mwelekeo wa Serikali ni nini katika kuhakikisha kwamba kwa kweli tunaifufua *TAZARA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, *TAZAMA Pipeline* ya kusafirisha mafuta nayo ni ya nchi mbili. Tumekuwa tukisafirisha yanakwenda Zambia, sasa hivi wameanza kusafirisha mafuta safi. Sasa mkakati wa Serikali uwepo ili ile *TAZAMA Pipeline* tusafirishe mafuta kutoka Dar es Salaam, yakifika Mbeya iwepo *depot* pale, yakifika Tunduma iwepo pale tupunguze gharama za uzalishaji, gharama za ongezeko la mafuta, gharama zile zitapungua, tukiweka pale yatasukumwa kwa *TAZAMA,* yatafika pale, yatapakuliwa na wafanyabiashara mbalimbali watachukua mafuta katika yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naamini kwamba tukifanya hivyo itatusaidia sana katika kuweza kujenga uchumi wetu imara katika maeneo hayo, lakini pia tutapunguza gharama kwa watumiaji wa mafuta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, napendekeza kuanzisha Mfuko wa Kuchochea Ujenzi wa Viwanda. Hatuwezi kuendelea kuimba tu tukasema uchumi wa viwanda, lazima tuwe na *mechanism* namna tutakavyochochea. Maeneo mengine tunajenga viwanda tukivikamilisha ndiyo tunatafuta mwekezaji wa kuviendesha vile viwanda, na ndipo hapo tutakapoweza kuvutia watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, naiomba Serikali, kuhakikisha kwa kweli tunakwenda kwenye uchumi mpana, uchumi mkubwa, jitihada nzuri mmezifanya, tumeona. Sasa Mheshimiwa Waziri hapa utatusaidia kutupa majibu maana yake ukisoma kwenye taarifa yako, mwaka 2021 unasema pato la Taifa kwa nchi yetu kwa dola za Marekani ulikuwa bilioni 69.9, mwaka 2021; mwaka 2023 tunategemea itakuwa bilioni 85.5. Uki-*calculate* pale, ukipiga hesabu ukuaji ni zaidi karibu toka mwaka 2021 Serikali ilipoingia Awamu ya Sita hii toka wakati huo ni zaidi ya asilimia 22, ukitoa unakuta kwamba yaani kwa kweli *growth rate* ingekuwa ni kubwa zaidi ya pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hebu utatusaidia, ni nini hasa ambacho kipo katika *calculations.* Kwa sababu *IMF* ndiyo wametoa hizo takwimu kwamba uchumi pato limetoka hapa limekwenda hapa, sasa ku-*calculate* kwa kawaida haitupi hii

*figure* ambayo mnaisema, inaonekana nchi tumefanya vizuri zaidi kwenye uchumi kuliko ambavyo takwimu zinaonekana kwenye madaftari. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba ni suala la kujipongeza, ni suala la kusema tumefanya hapa tuongeze nguvu zaidi ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa orodha ya Wabunge ambao waliomba kuchangia siku ya leo. Kwa hiyo, tutaendelea na huu uchangiaji, kama nilivyosema wa Bajeti Kuu kwa siku saba, na wengine wataendelea kuchangia kuanzia kesho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa *3.00* asubuhi.

*(Saa 7.45 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 20 Juni, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*